# Nipashe

Jumatatu Machi 4, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579856

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper




## Msiba wa Ruge waleta neema barabara Bukoba

UKURASA 3




UKURASA 13

# Lowassa afunguka



**ATETA** na Nipashe na kuzungumza kilichomfanya "kurudi nyumbani"...

*Endelea ukurasa wa 2*



Magari yakiwa yanatumia barabara maalum ya mabasi ya mwendo wa haraka ikiwa ni sehemu ya kukwepa maji ya mvua yaliyokuwa yamefurika eneo la bonde la Kinondoni Mkwajuni, kutokana na mvua kubwa iliyonyesha jijini Dar es Salaam jana.
**PICHA: SELEMANI MPOCHI**

## JPM awapangua Kabudi, Mahiga

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**DED AENDA KUHOJIWA UBADHIRIFU MIL. 200/-**
MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe, Kazimbaya Makwega...

UKURASA WA 3

**SABA JELA MIAKA 3 KWA UVUVI HARAMU**
WATU saba wamehukumiwa kwenda jela miaka mitatu wilayani Ukerewe, mkoani Mwanza kwa kosa la...

## Watumia spika za masikioni waonywa

UKURASA 3

**MICHEZO** ZIJUE DAKIKA ZA HATARI UNAPOIVAA YANGA UK. 18

MAONI, KATUNI UK.6

## HABARI KITAIFA

# Lowassa afunguka

**Na Romana Mallya**

WAZIRI Mkuu mstaafu, Edward Lowassa, amesema ataweka wazi sababu zilizomwondoa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) na kurejea Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Ijumaa, Lowassa ambaye alikuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chadema, alitangaza kukihama chama hicho kikuu cha upinzani nchini na kurejea chama tawala akipokewa na viongozi wakuu wa CCM walioongozwa na Mwenyekiti, Dk. John Magufuli.

Muda mfupi baada ya kupokewa na uongozi wa CCM, Lowassa alipewa fursa ya kuzungumza, lakini alisema maneno machache tu kuwa "nimerudi nyumbani".

Hata hivyo, kumekuwa kukielezwa sababu nyingi zinazodaiwa na wadau wa siasa nchini kwama zimemsukuma Lowassa kurejea CCM.

Kutokana na hali hiyo, Nipashe jana ilimtafuta Lowassa kujua sababu za kukihama chama kilichompa nafasi ya kukiwakilisha kusaka kiti cha urais katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

Katika mazungumzo hayo na Nipashe, Lowassa hakuwa tayari kuweka bayana sababu zilizomsukuma kurejea CCM, lakini alisisitiza kuwa wakati wowote kuanzia sasa, atazungumzia suala hilo kwa kina atakapokutana na waandishi wa habari.

"Nimepanga wakati wowote kuzungumzia kitendo changu cha kuondoka kwangu Chadema na kurudi CCM, maswali yote uliyonayo, nitayajibu kupitia mkutano huo wa waandishi wa habari," Lowassa alisema.

Nipashe ilipotaka kujua siku ya kufanyika kwa mkutano huo wa Lowassa na waandishi wa habari, Mbunge huyo wa zamani wa Monduli alijibu: "Wakati wowote kuanzia sasa, mtaarifiwa kuhusu mkutano wangu, usiwe na wasiwasi utajulishwa, nitazungumza yote unayoyahitaji kuhusu mimi."

Lowassa alipokewa na viongozi wa CCM kwenye ofisi ndogo zilizoko Lumumba jijini Dar es Salaam, ikiwa ni takribani miaka minne tangu akihame Julai 2015, baada ya jina lake kuenguliwa kwenye mchakato wa kumpata mgombea wa urais katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 kupitia chama hicho.

Wengine waliokuwapo kwenye mapokezi hayo ya Lowassa ni pamoja na Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Mwenyekiti wa CCM (Bara), Philip Mangula.

Pia picha zilizokuwa zikisambaa kwenye mitandao ya kijamii Ijumaa, zilionyesha Lowassa akiwa ameongozana na mfanyabiashara maarufu nchini, Rostam Aziz.

Akitangaza uamuzi huo wa Lowassa kurejea CCM, Dk. Bashiru alisema mwanasiasa huyo mzoefu ameamua kurejea chama tawala kuanzia siku hiyo.

"Lowassa amerejea nyumbani, kwa hiyo tunaanza kazi ya kujenga taifa letu na kulinda uhuru wetu," Dk. Bashiru alisema na kuongeza kuwa: "Lowassa ameamua kuweka siasa pembeni na kuungana na Rais Magufuli kuliletea taifa maendeleo."

Katibu Mwenezi wa CCM, Humphrey Polepole, akihojiwa na kituo cha runinga cha ITV,

INAENDELEA UK. 8



Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Sima (kushoto), akiwa ameambatana na maofisa wa Halmashauri ya Mji wa Njombe, kukagua dampo la uchafu lililoko katika kijiji cha Maheve, Kata ya Ramadhani mkoani Njombe jana. **MPIGAPICHA WETU**

# JPM awapangua Kabudi, Mahiga

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli amefanya mabadiliko madogo ya Baraza la Mawaziri ambayo yamewagusa mawaziri wawili.

Taarifa iliyotolewa jana na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu, ilisema walioguswa na mabadiliko hayo ni Waziri wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Augustine Mahiga.

Katika mabadiliko hayo, taarifa hiyo ilisema Prof. Kabudi sasa anakuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, wakati Dk. Mahiga anakuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Kwa mujibu wa taarifa hiyo, wateule hao wanatarajiwa kuapishwa leo saa 3:30 asubuhi, Ikulu jijini Dar es Salaam.

Profesa Kabudi na Dk. Mahiga walikuwa miongoni mwa mawaziri tisa waliokuwa hawajaguswa tangu walipoteuliwa kushika nyadhifa zao.

Wengine ambao bado hawajaguswa na wizara zao kwenye mabano ni Dk. Hussein Mwinyi (Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa), William Lukuvi (Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi) na January Makamba (Ofisi ya Makamu wa Rais- Muungano na Mazingira).

Wengine ni Ummy Mwalimu (Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto), Dk. Philip Mpango (Fedha na Mipango), Jenista Mhagama (Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge, Sera, Uratibu, Kazi na wenye Ulemavu).

Dk. Mahiga amekuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki tangu Desemba 10, 2015, wakati Rais Magufuli alipotangaza baraza la kwanza la mawaziri baada ya kuingia madarakani Novemba 5, 2015.

Profesa Kabudi kwa upande wake, amekuwa Waziri wa Katiba na Sheria tangu Machi 23, 2017 baada ya Rais kufanya mabadiliko akichukua nafasi ya Dk. Harrison Mwakyembe aliyeteuliwa kuwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Aidha, mabadiliko ya jana yalifanyika ikiwa takriban miezi mitatu tangu Novemba 23, mwaka jana wakati Rais Magufuli alipofanya mabadiliko kama hayo.

Mabadiliko hayo ya Novemba yalisababisha Charles Mwijage (Viwanda, Biashara na Uwekezaji) na Dk. Charles Tizeba (Kilimo) kuondolewa kwenye nyadhifa zao.

Kutokana na kung'olewa kwao, aliyekuwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais (Tamisemi), Joseph Kakunda, aliteuliwa kuchukua nafasi ya Mwijage na Japhet Hasunga, aliyekuwa Naibu wa Maliasili na Utalii kuwa Waziri wa Kilimo.

Sambamba na uteuzi huo, Mbunge wa Ukonga, Mwita Waitara, aliteuliwa kuwa Naibu Waziri (Tamisemi), Innocent Bashungwa (Naibu Waziri wa Kilimo) na Constantine Kanyasu kuwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii.

Pia aliyekuwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mary Mwanjelwa alihamishiwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuendelea na wadhifa wa naibu waziri.

## DED Mbozi aenda kuhojiwa ubadhirifu wa milioni 200/-

**Na Mwandishi Wetu,** MBOZI

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe, Kazimbaya Makwega, ametii agizo la Naibu Waziri katika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mwita Waitara ya kutaka kwenda wilayani Lushoto kujibu tuhuma za ubadhirifu wa Sh. milioni 200.

Serikali ilipokea fedha Sh. bilioni 1.8 kutoka kwa mwekezaji mpya kampuni ya New Kimamba Fibres, iliyonunua shamba hilo la mnazi kwa fedha hizo na kati ya hizo halmashauri ilipata Sh. milioni 600 kwa ajili ya ushuru wa huduma.

Upatikanaji wa fedha hizo uliifanya halmashauri hiyo kuanza michakato ya kutangaza zabuni kumpata mkandarasi atakayepima viwanja hivyo vyenye ukubwa wa hekta 1,637 na kupatikana kampuni hiyo ya Geoplan East Afrika Limited ya jijini Dar es Salaam ambayo ilipewa tenda ya Sh. milioni 300 kupima viwanja hivyo.

Hata hivyo, upatikanaji wa kampuni hiyo ulizua utata baada ya kudaiwa leseni yake ilikwisha muda na jinsi fedha zilivyotoka kabla ya kuanza kazi tayari kampuni hiyo ilipewa Sh. milioni 200 kinyume na taratibu za manunuzi.

Wakati suala hilo linafanyika wilayani humo, huku baadhi ya wakuu wa idara akiwamo ofisa ardhi wakisaini fedha za zaidi ya siku 30 bila kwenda kwenye tukio, wametakiwa kurejesha fedha hizo, huku Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mbozi akitakiwa kurudishwa Lushoto kujibu tuhuma hizo.

Ubadhirifu wa matumizi hayo ya fedha uliibuka baada ya Waziri Wait-

INAENDELEA UK. 8


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
March 3, 2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya jumapili Tarehe 3/03/2019 kampuni ya **EFFCO SOLUTION LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka DAR ES SALAAM kuelekea **NGAKA COAL MINING,** gari hilo lenye namba za usajili:

   **T875CZT/T364DCF**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **16.80** |
| **Upana** | - | **mita** | **3.55** |
| **Kimo** | - | **mita** | **4.50** |

3. Njia itakayotumika: **DAR ES SALAAM hadi NGAKA COAL MINING** Kupitia LINDI, gari litasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

XXXXXXX

# HABARI KITAIFA



Mtaalamu wa Magonjwa ya Masikio, Pua na Koo wa Hospitali ya Mloganzila, Dk. Godlove Mfuko, akimpima masikio Waziri Ummy Mwalimu jana, katika hospitali hiyo. **BEATRICE SHAYO**

## Msiba wa Ruge waleta neema barabara Bukoba

**Na Salome Kitomari**

MWILI wa aliyekuwa Mkurugenzi wa Vipindi wa Clouds Media Group (CMG), Ruge Mutahaba, utaagwa katika Viwanja vya Gymkhan mjini Bukoba leo, na baadaye kupelekwa Kijiji cha Kiziru wilayani Bukoba kwa ajili ya mazishi.

Vilevile, msiba huo umekuwa neema kwa wakazi wa Kijiji cha Kiziru walikotoka wazazi wa Ruge baada ya barabara kukarabatiwa kwa muda mfupi ili gari lililobeba mwili na yale ya waombelezaji yafike kijijini huko kirahisi.

Ratiba ya mazishi inaonyesha mwili huo utatoka kijijini Kiziru leo asubuhi na utapitishwa Barabara za Mweyanjare, Rwakagongo, Katoma, Kyakailagwa, Rwamishene Center, Kituo Kikuu cha Mabasi na Ofisi ya Mkoa na kuingia kwenye Viwanja vya Gymkana.

Mwili wa Ruge uliowasili mjini Bukoba jana saa 4:55 asubuhi kwa ndege ya Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) yenye namba 5H-TGF iliyotolewa na Rais John Magufuli, ulilala nyumbani

INAENDELEA UK. 8

## Saba wahukumiwa jela miaka 3 kwa uvuvi haramu

**Na Rose Jacob,** MWANZA

WATU saba wamehukumiwa kwenda jela miaka mitatu wilayani Ukerewe, mkoani Mwanza na mahakama ya kutembea (mobile court) kwa kosa la kufanya uvuvi haramu, huku wengine 14 wakifikishwa katika mahakama hiyo kwa kosa hilo.

Watu hao wamefikishwa mahakama hiyo kufuatia opereshani maalumu iliyoanza Februari 18 hadi 28, mwaka huu, katika kisiwa cha Ukerewe.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa operesheni hiyo, Ofisa Mfawidhi wa Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi, Kanda ya Ziwa Didas Mtambalike, alisema wameamua kuboresha utendaji kazi dhidi ya kudhibiti uvuvi haramu kwa kutembea na mahakama ikiwa ni sehemu ya kurahisisha hukumu kwa wahalifu na kuondoa msongamano wa kesi mahakamani.

Aidha, Mtambalike alisema ndani ya siku 10 wamefanikiwa kuwatia mbaroni watuhumiwa 14 na kati yao saba wameshasomewa hukumu yao ya kufungwa miaka mitatu jela kila mmoja au kulipa faini ya shilingi milioni tatu na wote walishindwa kulipa fedha hiyo na kwenda kutumikia kifungo gerezani kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi namba 22 ya mwaka 2009.

Aidha, alisema kikosi chake kimekamata makokoro ya sangara 60, vipande vya makila vilivyounganishwa 1,385, nyavu za dagaa 60, ndoano 4,700, pikipiki 35 na injini 17, huku kikosi cha halmashauri hiyo kikiwa kimekamata makokoro 48 ya sangara, 41 ya dagaa, nyavu za makila 870, ndoano 3,200, baiskeli 20 na pikipiki tano, jumla vikiwa na thamani ya zaidi ya Sh. milioni 500.

Mtambalike alisema operesheni hiyo imeanzia mkoani Mwanza kwenda Kagera, Geita, Simiyu na maeneo yote yanayojihusisha na shughuli hizo, huku akitoa wito kwa wavuvi kufuata sheria.

Ofisa Mfawidhi wa Rasilimali za Uvuvi Mkoa wa Kagera, West Allen, alisema kwa mujibu wa tathmini zilizofanyika zinaonyesha utumiaji wa nyavu za makila na zilizounganishwa umepungua, changamoto zimebaki kwa wale wenye makokoro na timba kutokana na mazingira ya ufanyaji kazi wao.

Aidha, Allen alisema kwa sasa nguvu kubwa itaelekezwa kwa matajiri wanaotengeneza na kuagiza nyavu hizo kutoka nje ya nchi na kuwa na mahakama kwenye operesheni inasaidia utunzaji wa vielelezo vya mshtakiwa.

Naye Ofisa Uvuvi Wilaya ya Ukerewe, Mussa Poland, alisema halmashauri iko tayari kuendelea kuunga juhudi za serikali kwa kuhakikisha wanaboresha vikosi vyao vya doria ili malengo yatimie katika kuelekea kwenye uchumi wa kati ifikapo 2025 na kutimiza azima ya Tanzania ya viwanda.

## Watumia spika za masikioni waonywa

**Na Beatrice Shayo**

SERIKALI imesema wanaotumia spika za masikioni kwa muda mrefu wako hatarini kupata matatizo ya usikivu, hivyo kuna haja kuachana na matumizi makubwa ya vifaa hivyo ili kuepuka ugonjwa.

Tahadhari hiyo ilitolewa jana na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alipozungumza kuhusu Siku ya Usikivu Duniani kwenye Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Tawi la Mloganzila.

Alisema wananchi wanatakiwa kupunguza matumizi ya spika masikioni ili kujikinga na tatizo la kukosa usikivu.

"Utakuta kijana akiamka yupo na 'earphones' (spika za masikioni) muda wote, tupunguze hii tabia, tusipokuwa makini, tunaweza kuwa na taifa lisilosikia kwa sababu ya matumizi ya simu za kisasa," alisema.

Waziri Mwalimu pia alisema atawasiliana na Shirika la Viwango (TBS) kuhakikisha spika zinazoingizwa nchini zinakuwa na ubora unaotakiwa kwa kuwa amepatiwa taarifa kuwa kuna spika feki, ambazo zinaongeza tatizo la usikivu.

"Mtoto hadi wa miaka mitatu anawekewa earphone masikioni, siyo

INAENDELEA UK. 8


## HALMASHAURI YA MJI WA BARIADI

**(Barua zote zijibiwe kwa Mkurugenzi Halmashauri ya Mji)**

Simu. Na. 028 2700554
Fax: 028 2700554
***Unapojibu tafadhali taja:***
Kumb.Na.JB.37/330/01/43

Ofisi ya Mkurugenzi wa Mji,
S.L.P 526,
BARIADI.
Tarehe: 1/3/2019

### TANGAZO LA KUITWA KWENYE USAILI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Bariadi anapenda kuwataarifu waombaji kazi wote walioomba kazi ya Utendaji wa Mtaa daraja la III,Watunza kumbukumbu Daraja la II na Madereva II kuwa usaili unatarajiwa kuendeshwa kuanzia tarehe 16 hadi 18 March 2019. Wasailiwa wanaoitwa kwenye usaili wanapaswa kuzingatia maelekezo yafuatayo:

1) Wasailiwa wanatakiwa kufika na vyeti vyao halisi yaani cheti cha kidato cha nne au Sita, Cheti cha Astashahada, Transcript na cheti cha kuzaliwa.

2) Wasailiwa wanatakiwa kufika na vitambulisho vinavyokubalika kama vile Kitambulisho cha Utaifa/Uraia, mpiga kura au Hati ya kusafiria.

3) Kila msailiwa atajigharamia kwa chakula, usafiri na malazi.

4) Kwa wale waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika ambayo ni NECTA.

5) Wasailiwa wote watatakiwa kufika ofisi ya Mkurugezi wa Mji saa moja na nusu asubuhi kwa tarehe tajwa hapo juu.

6) Orodha ya waombaji walioitwa kwenye usaili inapatikana kwenye tovuti ya Halmashauri ya Mji wa Bariadi ambayo ni www.bariaditc.go.tz pamoja na mbao za matangazo za Halmashauri ya Mji wa Bariadi, Halmashauri ya Wilaya ya Itilima na Bariadi Vijijini.

Tahadhari usaili utafanyika kwa mujibu wa Sheria Taratibu na Kanuni za Utumishi wa Umma. Kuna matapeli wanaotumia majina ya watu na vyeo vya watu kwa lengo la kujipatia fedha, kuweni makini na matapeli hao.

Suzana Bumbuni
Kaimu Mkurugenzi
Halmashauri ya Mji
BARIADI
MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MJI
BARIADI

XXXXXXXX

## Wahamiaji haramu 54 wakamatwa

**Na Renatus Masuguliko,** GEITA

WAHAMIAJI haramu 54 wamekamatwa mkoani Geita katika kipindi cha Januari na Februari, mwaka huu na kufukuzwa nchini huku 24 wakitiwa hatiani na wengine 43 kutozwa faini ya Sh. milioni 55.

Ofisa Uhamiaji Mkoa wa Geita, Naibu Kamishna wa Uhamiaji Wilfred Marwa, aliyasema hayo juzi alipokuwa akitoa ufafanuzi kuhusu malalamiko yaliyotolewa na wananchi juu ya kuwakamata na kuwahoji watu wanaodhaniwa kutokuwa raia.

Kamishna Marwa alisema katika kipindi cha Januari hadi Februari, watu 122 walikamatwa wakihusishwa na makosa tofauti yanayohusiana na sheria za uhamiaji na 24 kati yao walifikishwa mahakamani na kutiwa hatiani.

Alisema watuhumiwa 43 walikamatwa kutokana na kuingia nchini kufanya kazi bila kutimiza masharti ya kulipia vibali vyao vya kuwapo nchini na kufanya kazi. Alisema watu hao kwa pamoja walitozwa faini ya Dola za Kimarekani 25,800 sawa na Sh. milioni 55 za Kitanzania.

Kuhusu malalamiko yaliyotolewa na wananchi ya kupigwa na kutozwa fedha wakati wa utekelezaji operesheni hiyo, Marwa alikanusha kuhusika na kuomba waliotendewa kuthibitisha, wawasilishe ushahidi ili hatua zichukuliwe.

Aliwaondoa hofu wananchi waliohojiwa ambao wamekuwapo nchini kabla ya mwaka 1972 kuwa sheria inawatambua na hawatafukuzwa kwa kuwa operesheni hiyo inalenga kuwatambua wanaodhaniwa kuwa si raia wa Tanzania.

Kamishna Marwa alikiri kuyapokea malalamiko ya Wapi Mabala Nsongoma na Masumbuko Lwakubomwa wakidai kutendewa hivyo na ameomba kama wanaweza kuthibitisha madai hayo, wawasilishe ushahidi ili yafanyiwe kazi kwa kuwa hiyo inaweza kuwa mbinu ya kudhoofisha operesheni hiyo.

Akizungumzia malalamiko hayo, Diwani Dotto Joseph Kaparatus wa kata ya Lwamgasa wilayani Geita, anakoishi Nsogoma, alisema hapingi operesheni hiyo isipokuwa utumiaji nguvu katika kamatakamata hiyo umeathiri shughuli za kiuchumi na uzalishaji.

Nsongoma, mkazi wa kijiji cha Buziba na Rozaria Dotto Mabuga, Masumbuko Lwakubamwa wakiwa ni baadhi ya waliokumbwa na kamatakamata hiyo, wamedai walipewa kipigo wakati wakihojiwa na kujitetea kuwa wao na wazazi wao wamezaliwa Tanzania.

# Viwavijeshi vyavamia Kilindi vyaharibu mazao

**Na Dege Masoli,** KILINDI

ZAIDI ya hekta 2,000 za mashamba ya mahindi zimeshambuliwa na kuharibiwa na viwavijeshi, wilayani Kilindi, mkoani Tanga.

Wadudu hao wamesababisha hasara hiyo kwa wakulima wa vijiji vilivyomo kwenye Kata ya Pangwi, wilayani Kilindi, iliyoko umbali wa zaidi ya kilomita 60 kutoka makao makuu ya wilaya hiyo.

Akithibitisha kutokea kwa janga hilo, Ofisa Kilimo wa Kata ya Pagwi, Dustan Emmanuel, alieleza kuwa wastani wa ekari 2,500 zimeshambuliwa na mazao yake na kukitaja kijiji cha Nyamaleni kuwa ndicho kilichoathiriwa kwa kiwango kikubwa na wadudu hao.

Mmoja wa wakulima hao, Alex Mhando, alieleza kuwa uvamizi wa wadudu hao umekuwa tishio kwao kwa kuwa mahindi yaliyoshambuliwa ndiyo tegemeo la maisha yao.

Naye Cosmas Chingwaba, alieleza kuwa viwavijeshi hivyo vimeleta janga kubwa kwa wao la kukumbwa na njaa na kuingia kwenye maisha magumu ambayo watatokana na kukosa mahitaji ya chakula na mengine ya kijamii. Chingwaba aliiomba serikali kuingilia kati sakata hilo ili kuinusuru jamii na janga la njaa.

Hata hivyo, Emmanuel alisema taarifa za mlipuko huo na athari zake zimeshafikishwa kwenye ngazi husika kwa ajili ya hatua zaidi za kukabiliana na uvamizi huo na kudhibiti usisambae maeneo mengine wilayani humo.

Aidha, kutokana na tukio hilo wataalamu kutoka kituo cha kudhibiti magonjwa ya mimea cha Tengeru, mkoani Arusha wamewasili katika kata hiyo kutoa elimu ya kuwafanya wakulima hao kukabiliana na viwavijeshi hivyo.

Mmoja wa wataalamu hao, Grece Matiku, alieleza kuwa baada ya kupata taarifa za uvamizi huo kwenye Kijiji cha Nyamaleni wamelazimika kuchukua hatua ikiwamo kutoa elimu na kudhibiti wadudu hao kutosambaa maeneo mengine.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora, Emmenuel Nley, akitoa ufafanuzi kwa wajumbe wakati wa kikao Kamati cha Ushauri ya Mkoa wa Tabora (RCC) cha kupitia mapendekezo ya bajeti ya mkoa huo jana. **PICHA: VICENT TIGANYA**

# Waziri: Plastiki zisichanganywe na taka nyingine

**Na Gwamaka Alipipi**

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira, Mussa Sima, ameziagiza mamlaka zinazohusika na ubebaji taka ngumu kuhakikisha zinatenganisha chupa za plastiki na taka nyingine, kwa kuwa zikitupwa pamoja kwenye dampo, zinachangia uharibifu wa mazingira.

Aliyasema hayo mkoani Njombe mwishoni mwa wiki alipotembelea moja ya madampo ya Halmashauri ya miji ya Njombe na Makambako.

Sima alisema kuchanganya chupa za plastiki kwenye uzoaji taka na kwenda kuzitupa katika madampo, kuna athari kubwa ya kimazingira kwa kuwa haziozi.

"Changamoto nyingine ni hizi chupa za plastiki, zinakusanywa na kuzihifadhi mahali kwa kuwa kuna biashara inafanyika ya hizi chupa za plastiki, sasa tunatoa uchafu nje tunauleta mahali ambapo tunajua tunauteketeza, wapo wengine wanakuja wanautoa ule uchafu kwa kupitia hizo chupa za plastiki," Sima alisema.

Aliongeza kuwa serikali kupitia Baraza la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), itaratibu na kusimamia utekelezaji wa agizo hilo kwa kuwa kuna sheria na kanuni zinazowaongoza kutekeleza majukumu yao.

Mratibu wa NEMC Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Godlove Mwamsoje, alitoa wito kwa Watanzania kuhakikisha wanasimamia vyanzo vya maji na kuvitunza ili kulinda ikolojia ya mazingira kwa manufaa ya viumbe na wananchi wenyewe.

Alisema NEMC imekuwa ikisisitiza wananchi kutunza mazingira ipasavyo ili kuokoa vyanzo vya maji vinavyotiririsha maji kwenye mito.

"Katika Nyanda za Juu Kusini, changamoto ambazo tunazo za suala la mazingira, ni usimamizi wa vyanzo vya maji, tumebarikiwa kuwa na maeneo yenye mwinuko ambayo vyanzo vingi vya maji ndivyo vinavyolisha mabonde muhimu kwa maisha ya wananchi," Mwamsoje alisema.

"Wito wangu kwa wananchi ni kuhifadhi vyanzo vya maji, serikali sasa hivi ina mpango wa kusambaza maji kila kijiji, kama tutakausha hivi vyanzo, hakuna mahali serikali itapata maji ya kuwapelekea wananchi."



Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, akionyesha kadi yake ya ATM baada ya kufungua akaunti yake kwenye hafla fupi ya uzinduzi wa tawi la benki ya TPB wilayani Nzega. Kulia ni Mbunge wa Nzega, Hussein Bashe na kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa benki hiyo, Dk. Edmund Mndolwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwanri aagiza wanaotoza nauli za juu kukamatwa

**Na Tiganya Vincent**

KAMATI cha Ushauri ya Mkoa wa Tabora (RCC), imeiagiza Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (Sumatra) mkoani humo, kuanza kuwakamata wasafirishaji wanaowatoza abiria nauli ambazo sio halali.

Tamko hilo limetolewa jana na Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, kwa niaba ya wajumbe wakati wa kikao cha kuwasilisha mapendekezo ya bajeti ya Mkoa wa Tabora ya mwaka ujao wa fedha.

Alisema kumekuwapo na malalamiko kutoka kwa abiria kutozwa nauli zaidi ya iliyoandikwa kwenye mabasi kinyume cha utaratibu.

Mwanri alisema vitendo hivyo havikubaliki na ni uvunjifu wa sheria na kuwaibia wanyonge fedha zao, hivyo aliiagiza Sumatra kuweka mtego ambao utasaidia kuwanasa wasafirishaji wanaoendesha vitendo hivyo.

"Sio lazima msubiri hadi abiria walete malalamiko ...wekeni mtego wa kujifanya mnasafiri mtawapata na kuwachukulia hatua kwa mujibu wa sheria...ni vema abiria alipe nauli halali na apatiwe tiketi ili kuhakikisha hakuna uwepaji wa kodi za serikali," alisema.

Aidha, Mkuu wa Mkoa huyo aliwataka abiria kutokubali kutoa fedha zaidi ya iliyoandikwa ubavuni mwa magari na kama watatozwa zaidi wahakikishe wanapewa tiketi na kuipeleka kwa askari wa usalama barabarani ama Sumatra ili wahusika wachukuliwe hatua.

Awali, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Sikonge, Peter Nzalalila, alisema kuna unyanyasaji wanaofanyiwa abiria wa kutozwa nauli ambayo sio halali na kusema kuwa kutoka Tabora kwenda Sikonge wamekuwa wakitozwa Sh. 4,000 badala ya Sh. 3,100.

Aliongeza kuwa katika njia hiyo hiyo, wanaoishia Tutuo wamekuwa wakitozwa

**INAENDELEA UK. 8**

# Shirika lajitosa ajira kwa vijana

**Na Dege Masoli,** TANGA

SHIRIKA la Konrad Adenauer linalofanya kazi chini ya Ujerumani, limepanga kupunguza changamoto mbalimbali ikiwamo kutoa elimu ya uchumi jamii yenye lengo la kuwawezesha Watanzania kujiajiri.

Akizungumza katika kongamano la elimu ya uchumi jamii lililoshirikisha wanafunzi wa vyuo mbalimbali jijini Tanga, Ofisa Miradi wa shirika hilo, Mary Tagalile, alisema lengo kuu ni kubadilisha mtazamo katika sekta ya ajira hususan kwa vijana ambao wamekuwa wakilalamika kukosa nafasi serikalini.

Tagalile aliwataka vijana kujitambua na kuachana na dhana ya kutegemea kuajiriwa pindi wanapohitimu masomo na badala yake wawe wabunifu katika kukabiliana na changamoto za ajira kwa kujiajiri kwa kuwa sekta hiyo ndio pana na yenye uwezo wa kuwafikia watu wengi zaidi.

"Shirika limeona ni vyema kutoa elimu kwa vijana kujitambua lakini pia kuwapa elimu ambayo itawajenga katika kukabiliana na changamoto ya ajira, huku lengo likiwa ni kupata maendeleo kupitia sekta binafsi," alisema.

Naye Richard Jackson, Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, alisema vijana wengi wanakata tamaa ya maisha kutokana na kukosa ajira, hivyo kupitia kongamano hilo watapata mbinu za kukabiliana na changamoto za ajira.

"Mnajua hakuna mtu ambaye anaweza kuwaletea maendeleo zaidi ya ninyi wenyewe, hivyo mnatakiwa kuwa na uthubutu, mfungue masikio yenu na muwe na jicho la kuona namna ambavyo mnaweza kutengeneza misingi bora ya maisha yenu bila kusubiri kuajiriwa," alisema Jackson.

Wakizungumza baada ya kongamano hilo, baadhi ya wanachuo walisema elimu waliyoipata imewasaidia kutambua tatizo linalofanya kuwapo kwa ongezeko la vijana mitaani kuwa ni pamoja na kushindwa kuwa wabunifu na kuahidi kuwa mabalozi wazuri kwa wenzao.

"Tumejua mbinu mbalimbali za kujiajiri, hivyo kupitia elimu hii tuliyopewa leo (juzi) tutaweza sasa kufanya uamuzi mzuri wa kujiajiri baada ya kumaliza chuo lakini pia tunaahidi kuwa mabalozi kwa wenzetu ambao hawajapata fursa ya kufika hapa," alisema Musa Mahenge, mwanafunzi kutoka Chuo cha Elimu Sahare.

# Vitendo vya ukatili vyashamiri Songwe

**Na Ibrahim Yassin,** MBOZI

UKATILI dhidi ya watoto umeelezwa kuongezeka mkoani Songwe na taarifa zinaonyesha kuwa kati ya Januari, 2017 na Desemba, mwaka jana, zaidi ya watoto 150 walifanyiwa vitendo hivyo ikiwamo ubakaji.

Ofisa wa Jeshi la Polisi anayeshughulikia masuala ya jinsia mkoani humo, Clara Ndyamakana, alisema mwaka 2017 matukio 87 ya ubakaji watoto yaliripotiwa, huku mwaka jana 2018, matukio 72 yaliripotiwa.

Ndyamakana pia alisema kwa siku huripotiwa wastani wa matukio sita ya wanawake kupigwa na kujeruhiwa na waume zao katika mkoa huo, hali inayowalazimu kuendelea kutoa elimu kwa wanandoa hasa wanaume kuacha vitendo hivyo.

Kuhusu mimba za utotoni, Ndyamakana alisema takwimu za mwaka 2017 zinaonyesha wanafunzi katika shule za msingi na sekondari waliopata mimba ni wane, wakati mwaka jana walikuwa 37 kati ya hao, watatu waliozeshwa na wazazi wao. Alisema idadi hiyo ni kubwa na kwamba kwa sasa wanatakiwa kupambana kudhibiti hali hiyo kwa kushirikiana na wanahabari na wananchi kwa ujumla kwa kuwa watoto wanatakiwa kusoma ili watimize ndoto zao kimaisha.

Naye Mratibu wa Huduma za Afya ya Uzazi wa Mtoto, Elida Machungwa, aliwataka watu wanaofanyiwa vitendo hivyo vya ukatili, kuripoti vituo vya afya na hospitali ili kupatiwa tiba na kuepuka kupata ujauzito pamoja na maambukizi ya kingono ikiwamo virusi vya Ukimwi (VVU).

Hata hivyo, wadau mbalimbali wamepongeza hatua hiyo iliyofanywa na viongozi hao kwa kuwashirikisha wanahabari na kusema kwa kutumia kalamu zao wanaweza kuandika matukio haya na kufanikisha kutoweka.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba malizieni kazi Caf kwa JS Saoura

**WAWAKILISHI** pekee wa Afrika Mashariki na Kati katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba wanaondoka jijini Dar es Salaam kesho kuelekea Algeria kwenye mechi yao ya hatua ya makundi dhidi ya JS Saoura.

Mechi hiyo ya marudiano ya Kundi D, itakayopigwa Jumamosi Machi 9, mwaka huu, inatarajiwa kuwa na upinzani mkali kutokana na nafasi ya timu hizo katika kundi lao hilo linalozijumuisha pia Al Ahly ya Misri na AS Vita ya DR Congo.

Simba iliyopo nafasi ya pili ikiwa na pointi sita, moja nyuma ya vinara Al Ahly na moja mbele ya JS Saoura, endapo itashinda mechi hiyo inaweza ikawa imefunzu robo fainali kutegemeana na matokeo dhidi ya timu hiyo ya Misri na AS Vita inayoburuza mkia ikiwa na pointi nne.

Kimahesabu endapo AS Vita, itapoteza nyumbani dhidi ya Al Ahly ama kutoka sare na kisha Simba ikashinda, moja kwa moja timu hiyo ya Tanzania itakuwa imefuzu kutokana na kufikisha pointi tisa ambazo zinaweza kufikiwa na timu hiyo ya Misri pekee. Ikumbukwe katika hatua hii ya makundi, kila kundi kutoka manne, linatoa timu mbili zitakazotinga robo fainali, hivyo Simba inatakiwa kushinda, huku ikiombea AS Vita ipate matokeo mabaya dhidi ya Al Ahly.

Aidha, kushinda kwa Simba kutaiondolea kucheza kwa presha katika mechi ya mwisho nyumbani dhidi ya AS Vita, hivyo kinachotakiwa sasa ni kumaliza mchezo huo ikiwa ugenini, Algeria.

Tunaamini kama Simba itacheza kwa kiwango ilichokionyesha dhidi ya Al Ahly Uwanja wa Taifa na kisha kwenye Ligi Kuu dhidi ya Yanga, African Lyon, Azam FC, Lipuli na Stand United, inaweza kushangaza kwa kushinda mechi yake ya kwanza ugenini katika mashindano hiyo.

Kinachotakiwa kwa viongozi wa Simba na benchi la ufundi ni kuwaandaa wachezaji kisaikolojia zaidi kwa kuwaaminisha kwamba inawezekana kushinda ugenini.

Hata hivyo, kinachoonekana kwa wachezaji wa Simba ni kucheza pasipo kujiamini pindi wanapokuwa ugenini kwenye michuano hiyo yenye utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu barani Afrika. Hivyo, wakati huu benchi la ufundi likiwa limeongezewa nguvu kufuatia uongozi kumleta Denis Kitambi kuwa msaidizi wa Kocha Mkuu, Mbelgiji Patrick Aussems, tunaimani watashirikiana vema kuleta matokeo chanya.

Tanatambua tangu ilipofungwa mabao 3-0 dhidi ya Simba, JS Saoura haijapoteza tena mechi yoyote ile ikicheza nyumbani au ugenini. Imevuna jumla ya pointi tano kutokana na kutoka sare ugenini dhidi ya AS Vita na kisha kuichapa ikiwa nyumbani, huku pia ikitoka sare dhidi ya Al Ahly nyumbani.

Lakini hilo, halitutii hofu kwa Simba, kwa kuwa ilishacheza na timu hiyo na kuifunga, hivyo tunaamini inajua uchezaji wao na haina sababu ya kuwaogopa wapinzani wao hao.

Viongozi wa Simba, benchi la ufundi na wachezaji wanapaswa kusahau matokeo yaliyopita na kuichukulia mechi hiyo kama fainali ya wao kutinga robo fainali ya michuano hiyo.

Katika mechi hiyo, pamoja na Simba kutakiwa kumheshimu mpinzani wake, inatakiwa kuingia uwanjani ikitambua kuwa inahitaji matokeo mawili tu kwenye mechi hiyo, kushinda au ikishindikana kabisa angalau sare.

Ni kweli tunatambua katika michuano hii hutawaliwa na fitina nyingi nje na ndani ya uwanja, hivyo viongozi na benchi la ufundi wanapaswa kujiandaa kwa kila kitu.

Hata hivyo, hatuna shaka sana katika hilo kutokana na ukweli kwamba klabu ya Simba wanatambua kuwapo kwa mbinu hizo chafu, ila tunasisitiza umakini zaidi ikiwa ni pamoja na wachezaji kuaswa kucheza kwa kutomtegemea zaidi mwamuzi. Tunaitakia Simba kila la kheri katika kuipeperusha bendera ya Taifa katika michuano hii.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# TFF imulike hili la Mbaga lisitokee na Ligi Kuu Bara

Na Adam Fungamwango

**KAMATI** ya Maadili ya Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), imemfungia maisha Mwamuzi wa zamani wa Kimataifa na Katibu wa Chama cha Waamuzi Tanzania (FRAT), Oden Charles Mbaga, baada ya kutiwa hatiani kwa rushwa na upangaji matokeo.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Cliford Ndimbo, amesema leo jijini Dar es Salaam kwamba baada ya uchunguzi uliofanyika kuanzia Julai 11, 2018, Mbaga amekutwa na hatia ya kuhusika kwenye upangaji wa matokeo ikiwa ni kinyume cha Kanuni za Maadili za FIFA.

Mbaga amevunja Ibara ya 11 ya Kanuni ya Rushwa ya Fifa ya mwaka 2009. Anafungiwa maisha kutojihusisha na shughuli zozote za mpira wa miguu katika ngazi ya kitaifa na kimataifa kwa mujibu wa Ibara ya 7J ya Kanuni za Maadili za FIFA za mwaka 2018 pamoja na Ibara ya 22 ya Kanuni ya Nidhamu ya FIFA.

Anatakiwa kulipa faini ya kiasi cha fedha za Uswisi Faranga 200,000 ndani ya siku 30, vilevile anatakiwa kulipa gharama za shauri hilo kiasi cha Faranga za Uswisi 1,000 ndani ya siku 30 tangu alipopata taarifa.

Mbaga ambaye ni Katibu wa Chama cha Waamuzi Tanzania (FRAT), anapoteza sifa ya nafasi hiyo kutokana na adhabu ya kufungiwa maisha kutojihusisha na masuala ya mpira wa miguu.

Hii iliyotokea siyo aibu tu kwa soka la Tanzania, bali ni kwa nchi yote kwa ujumla.

Inalishushia heshima soka la Tanzania na kuonekana kuwa lina waamuzi wa aina hiyo wengi, ila huyo ni mmoja tu kati yao.

Hili linaweza kusababisha hata Shirikisho la Soka Afrika (Caf) na (FIFA) kutowaamini au kuwatizama kwa jicho la tatu waamuzi wa Kitanzania.

> **Huenda zile tuhuma ambazo klabu mbalimbali zimekuwa zikilalamika kuonewa na waamuzi zikawa ziko karibu na ukweli, kwa kuwa kama katibu mwenyewe ana matatizo, anaowaongoza watakuwaje?**

Kilichoniacha mdomo wazi ni kwamba Mbaga alikuwa ndiye katibu wa FRAT ambacho ndicho chama kinachotoa waamuzi wanaokwenda kuchezesha mechi mbalimbali nchini.

Huenda zile tuhuma ambazo klabu mbalimbali zimekuwa zikilalamika kuonewa na waamuzi zikawa ziko karibu na ukweli, kwa kuwa kama katibu mwenyewe ana matatizo, anaowaongoza watakuwaje?

Tunaona hata kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara baadhi ya mechi zimekuwa hazichezeshwi vema na waamuzi, lakini kimbilio kubwa ni kwamba yalikuwa ni makosa ya kibinadamu.

Kuna baadhi ya wachezaji wanapigwa viwiko hawaonyeshwi kadi, baadhi ya timu 'zinanyongwa' waziwazi, waamuzi wakitoa adhabu upande mmoja ukifanya, lakini ukifanya upande mwingine wanapeta inawezekana tatizo likawa ni lile lile kama waliloweka wazi FIFA.

Ni wajibu sasa kwa TFF kuwajibika kwa hili na si kukaa kimya. FIFA tayari imeshatukumbusha kuwa kuna waamuzi wala rushwa kwenye soka la Tanzania, hivyo isijifanye kama haioni tatizo, kwa kuwa hilo linaonekana kwa macho tu hata kwenye baadhi ya mechi za Ligi Kuu.

Kinachotakiwa ni TFF kupanga mpango mkakati kwa ajili ya kufanya uchunguzi pamoja na ushahidi wakihusisha vyombo husika, ikiwamo hata vya kiserikali Takukuru kwa ajili ya kuwanasa wote wenye tabia hiyo na kubakisha waamuzi wenye maadili.

Hii siyo tu itafanya soka letu liendelee na kutoa mabingwa na washindani bora, lakini pia itawafanya hata Caf na FIFA kuwaamini waamuzi wetu na kuwateua kuchezesha kwenye michuano mbalimbali mikubwa barani Afrika kama vile fainali za AFCON na hata Kombe la Dunia.

BARUA/MJADALA

## Tuwarekebishe vijana kimila

**Mhariri,**

*HIVI sasa ndani ya jamii kuanzia shuleni na nje ya shule kuna mijadala ya kina kuhusu sababu na mazingira ya watoto wa kizazi hiki kuwa mbali na utamaduni wao.*

*Wanaelezwa sasa, wako zaidi katika utamaduni unaoendana na yanayojitokeza katika mazingira na teknolojia mpya, inayotawala sasa.*

*Wazazi na walezi tumekuwa wakali na walalamishi kuhusiana na mabadiliko hayo ya kiutamaduni na mila.*

*Sijui ni watoto wangapi leo wanaojua michezo kama goroli, 'tiyari bado' na mingine mingi katika jamii zao. Haishangazi kukuta kundi la watoto hao, wanahesabika.*

*Kama mtazamo ni huo kuna haja ya kujiuliza zaidi, nini sababu za msingi? Hapana shaka ni mabadiliko kwamba, mifumo ya mawasiliano imekamata maisha yao.*

*Namna ilivyokamata inawahamasisha kutawaliwa na hayo ambayo ni matokeo ya teknolojia kwa jumla, kukiwapo mabadiliko makubwa katika teknolojia ya mawasiliano ya umma.*

*Hivyo, sisi tulio na umri ambao umeshuhudia vipindi tofauti vya ukuaji, kabla ya teknolojia na baada ya hapo, tuna mengi ya kueleza na tunaowajibika nayo, katika sura ya ukubwa na wajibu wa ulezi.*

*Tunapaswa kukifanya hicho katika mtazamo wa uzazi kwa maana tunawajibika kusimamia mwelekeo kiimani na kimaadili, pia katika elimu ya wanachopaswa kukifahamu kimaadili.*

*Hivyo, tusiishie katika kuwalamu 'kwa nini wamekuwa hivi' bali na kuwatengenezea mwelekeo.*

**Abbas H. Abbas,**
**Pangawe, Morogoro.**

# Kichuya kaondoka, Ajibu unasubiri nini?



Ibrahim Ajibu akishangilia moja ya mabao yake aliyoifungia Yanga msimu huu. Nyuma ni mshambuliaji mwenza wa timu hiyo, Heritier Makambo. **PICHA: MAKTABA**

**Na Adam Fungamwango**

KUMEKUWA na wimbi la wachezaji wa Kitanzania kwenda kucheza soka la kulipwa nje ya nchi kwa miaka ya hivi karibuni.

Kwa bahati nzuri ni kwamba wachezaji wengi wa Kibongo kwa sasa wanakubali hata kwenda kucheza soka la kulipwa kwenye ligi mbalimbali barani Afrika.

Zamani wachezaji wa Kitanzania walikuwa wakijidanganya kuwa wanataka kucheza soka la kulipwa Ulaya kwenye klabu kubwa za Manchester United, Arsenal, Chelsea.

Hizo ndizo zilikuwa ndoto zao. Walidhani kuwa wanaweza kutoka kwenye klabu za Simba na Yanga na kwenda moja kwa moja Liverpool.

Kwa sasa wamejua ukweli. Ni kazi ngumu sana. Kama Mbwana Samatta hadi leo hajakanyaga England, iweje wao?

Pia huyo huyo Samatta wamemwona alipotoka Simba kwanza akaenda zake TP Mazembe na huko ndiko alikopikwa zaidi.

Hilo limekuwa funzo kwa wachezaji wa Kitanzania. Kwa kutokana na kutokukubali kwenda kucheza ligi humu humu Afrika.

Kina Himid Mao, Abdi Banda na wengineo ni moja kati ya wachezaji walioondoka nchini kwenda kucheza soka la kulipwa ndani ya Afrika hii.

Hivi karibuni kuna wachezaji kama Eliud Ambukile wa Mbeya City, amekwenda kujiunga na klabu ya Black Leopards ya Afrika Kusini, Habib Kyombo akiwa ameshafanya majaribio na vipimo vya afya tayari kujiunga na Mamelodi Sundowns, huku Shiza Kichuya kwa sasa akiwa nchini Misri akichezea ESPN FC.

Kati ya wachezaji hawa wote, hayupo mmoja mwenye kipaji cha juu kwenye soka la Tanzania, Ibrahim Ajibu.

Ilitegemewa kuwa Ajibu angekuwa mmoja ya wachezaji ambao kwa sasa wameshapata timu japo hapa hapa Afrika.

Kama kina Kyombo, Ambokile na Kichuya wamepata timu na sasa wanacheza soka la kulipwa, sidhani kama Ajibu angekosa.

Pamoja na kipaji chote kile alichonacho mchezaji huyo ameendelea kubaki nchini, huku wachezaji waliokuja nyuma yake wakiondoka na kumuacha.

Ikumbukwe wakati yupo Simba, Kichuya alikuwa bado hajajiunga na klabu hiyo. Tatizo ni nini? Huenda mwenyewe Ajibu hataki au hajaamua. Akiamua sidhani kama kuna kizuizi chochote kinaweza kumfanya asipate timu ya kuichezea nje ya nchi.

Ajibu ana kipaji cha hali ya juu na adimu sana kwa wachezaji wengi nchini Tanzania. Lakini mwenyewe anaonekana amekuwa 'akikichukulia poa'. Ni vitu vichache tu anavyotakiwa kufanya ambavyo vinaweza kumfanya kuwa mmoja wa wachezaji bora kabisa kutoka barani Afrika.

Kwanza kabisa ni kufanya mazoezi kwa bidii. Inaelezwa hata na kocha wake, Mwinyi Zahera kuwa Ajibu ana tatizo la kutojituma.

Kutojituma ni tatizo la wachezaji wengi ambao ni wavivu wa mazoezi, kwa kuwa wanachoka mapema.

Pia kama angeamua kuutengeneza mwili wake na kuwa na utimamu wa kutosha, sidhani kama mpaka sasa angekuwa hata Afrika, achilia mbali Tanzania.

Hivyo ndivyo vitu vichache vinavyomkwamisha mchezaji huyo, na kumfanya mpaka sasa awe anaichezea ligi ya Bongo, huku kukiwa na wachezaji ambao hawana vipaji vikubwa sana kama yeye, lakini wana nia na wanajituma, hivyo kufikia malengo yao ya sasa na ya baadaye.

Inawezekana kwa sasa ameridhika na hali iliyopo, lakini baadaye akija kuzinduka atajikuta amechelewa na umri umekwenda.

Wapo baadhi ya wachezaji walikuwa kama yeye ambao walisita au kukacha kwenda nje, tena wakiwa fiti, lakini kwa sasa wanajuta kwa kuwa umri hauwaruhusu tena.

Huu ndiyo muda sahihi kwa Ajibu kwenda kusaka malisho nje kwa sababu muda hausubiri mtu, vinginevyo atakuja kubaki na kipaji chake, lakini umri ukiwa haumruhusu tena.

KABWELA NA FADHIL MOHAMMED




## WASILIANA NASI:

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

HABARI KITAIFA

# Msiba wa Ruge waleta neema

INATOKA UK.3

kwao Kiziru kwa ajili ya taratibu za kimila.

Uongozi wa Mkoa wa Bukoba uliwapokea waombelezaji na kuwapa pole na baadaye viongozi hao waliongoza uchukuaji wa mwili kutoka kwenye ndege kwenda na kuuweka kwenye gari maalum ambalo badala ya kuwa na namba za usajili, lilisomeka R.I.P Ruge (Pumzika kwa amani Ruge).

Katika eneo ambalo gari hilo lilikuwapo mamia ya wananchi walijitokeza wakiomboleza kwa kulia na kutaka kuligusa gari hilo.

Mwili ulitolewa kwenye uwanjani wa ndege kwenda nyumbani ukipitishwa Barabara za Kashai, Sido, Kituo Kikuu cha Mabasi, Hamgembe, makutano ya Barabara ya Rwamisheje, Kibeta, Magoto, Kalabaine na hadi kijijini Kiziru.

Kila barabara ambayo mwili huo ulipitishwa, mamia ya wananchi walijitokeza kuuaga.

"Kwa kweli nilikuwa sikufahamu vizuri zaidi ya kukuona kwenye vyombo vya habari, ila kupitia historia yako kwa niliyoasikia jana (juzi), kwa kweli nimekupenda sana na nakuombea Mungu akupe kauli thabiti," ulisomeka ujumbe wa Grace Mkapa uliorushwa na vituo vya runinga vilivyokuwa vinarushwa moja kwa moja usafirishaji wa mwili wa Ruge jana.

Ujumbe mwingine ni wa Nyamaronge Mwita aliyesema: "R.I.P mzee wa fursa, ulitufungua kifikra wadogo zako na vijana waelewe wanapambana siyo kulalamika. Mungu awatie nguvu wazazi na watoto wako. Mwanga wa milele umwaangazie, apumzike kwa amani."

Ujumbe wa Meya wa Manispaa ya Kigoma, Hussein Ruhava, ulisomekwa: "Pumzika kwa amani Ruge Mutahaba, hakika umetuachia jukumu kubwa la kuyaenzi maono yako, daima tutakukumbuka."

Baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Kiziru walisema barabara ya kutoka vijijini kwao kwenda mjini imekarabatiwa kwa kipindi kifupi kutokana na msiba huo.

Wakiwa kwenye msiba huo jana, Nyamwiza Kagara na Cuthbert Mugisha, walisema kuwa awali barabara hiyo ilikuwa ikisumbua kupitika hasa nyakati za mvua.

Kagara alisema msiba umekuwa neema kwa wananchi kutokana na kukarabatiwa kwa barabara hiyo ndani ya muda mfupi, lakini akasisitiza hawakuomba utokee msiba wa "mtu mkubwa" ndiyo watengenezewe bali ni wajibu wa serikali.

"Tumebaki na kumbukumbuku kubwa kwa huu msiba hapa kijijini, tumetengenezewa barabara ambayo siyo leo wala kesho kuharibika japo imetengenezwa kwa kiwango cha vumbi," Kagara alisema.

Mugisha alisema matengenezo ya barabara yalifanyika Machi 2, yaani juzi na sasa wataachana na usafiri uliokuwa ukitumika zaidi wa pikipiki na kuhamia kwenye magari ambayo awali yalikuwa hayafiki maeneo yao kutokana na barabara kutopitika.

"Shughuli kubwa hapa kijijini ni kilimo cha mazao mchanganyiko, ilikuwa kazi ngumu kusafirisha mavuno yetu kwenda sokoni," alisema.



Mkuu wa Wateja Wakubwa na Serikali wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi (kushoto), akimkabidhi vifaa tiba Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu, Bunge, Ajira, Kazi, Vijana na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, vyenye thamani ya Sh. milioni 10 kwa ajili ya Kituo cha Afya Mirerani Wilaya ya Simanjiro, Mkoa wa Manyara. **MPIGAPICHA WETU**

## DED Mbozi aenda kuhojiwa

INATOKA UK. 2

ara kufanya ziara wilayani humo katika kikao chake na watumishi na kubaini kuwapo kwa matumizi hayo yasiyofuata taratibu za manunuzi na kutoa maagizo ya kusimamishwa watumishi watatu, huku akimtaka Mkurugenzi Makwega, kufika kuhojiwa.

Mkurugenzi Makwega ametii agizo kwa kufika wilayani Lushoto akiendelea kuhojiwa na maofisa toka Tamisemi, huku wenzake watatu wakisimamishwa kazi kufuatia matumizi hayo ya fedha Sh. milioni 200 kati ya 300.

Akizungumza na gazeti hili jana ofisini kwake, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Lushoto, Lucas Shendolwa, alikiri kuwapo na matumizi ya fedha hizo akidai kuwa serikali baada ya kupokea fedha Sh. 2,808,240,000 kutoka kwa mwekezaji mpya wa shamba la mnazi na kusema kuwa Sh. milioni 600 walipewa kwa ajili ya ushuru wa huduma.

Alisema baada ya magizo ya Waziri Mkuu, madiwani wanatakiwa kurudisha fedha walizolipana posho walipoketi vikao ambazo ni Sh. 9,075,000 na kwamba mkurugenzi na timu yake wanatakiwa kurejesha Sh. milioni 200, na baadaye hatua zitachukuliwa.

Watumishi waliosimamishwa kufuatia tuhuma hizo ni Mhasibu wa Halmashauri ya Lushoto, Lenatus Mkasiwa, Meneja wa Mradi, Rehema Shimliwa, Ofisa Manunuzi, Deogratus Lwamtawe na aliyekuwa Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, aliyehamishiwa Wilaya ya Mbozi, Kazimbaya Makwega yupo Lushoto akihojiwa.

Halmashauri ya wilaya hiyo jana imekaa kikao kujadili na kupata ukweli kuwa viwanja hivyo vimepimwa huku ikielezwa kuwa kampuni iliyopewa zabuni hiyo iliweka mawe ya mipaka kwenye maeneo ya vichaka kisha kuondoka.

Baadhi ya watumishi katika Halmashauri ya Lushoto walifurahishwa na kitendo cha mkurugenzi huyo kuitwa kujibu tuhuma hizo wakidai ni msumbufu, huku akikiuka maadili ya kazi kwa kutumia vibaya madaraka yake kwa kuwahamisha hamisha vituo vya kazi hasa wanawake.

## Mwanri aagiza

INATOKA UK. 5

Sh. 4,000 badala ya Sh. 2,300 na wanaoishia Pangale wanatozwa Sh. 3,000 badala ya Sh. 1,500 iliyoidhinishwa na Sumatra.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Tabora (Uyui), Said Ntahondi, alisema tatizo hilo lipo njia zote mkoani humo na kutoa mfano wa gharama ya nauli kutoka Tabora Manispaa hadi Goweko abiria anatakiwa kulipa nauli halali Sh. 3,000, lakini amekuwa akilipa Sh. 4,000.

Aliongeza kwa njia ya kwenda Ulyankulu abiria anatakiwa kulipa Sh. 4,100 na kwenda Chemba Sh. 2,500, lakini katika maeneo hayo yote wamekuwa wakilazimishwa kulipa Sh. 5,000.

Ntahondi alisema katika njia ya kwenda Urambo kutoka Manispaa hadi Ussoke abiria wanatozwa Sh. 4,000 badala ya 2,500 na Sh. 5,000 kwenda Urambo badala ya Sh. 4,100 zilizoidhinishwa na Sumatra.

Kwa upande wa Ofisa Mfawidhi wa Sumatra Mkoa wa Tabora, Nelson Mmari, aliwataka abiria wote wanaotozwa nauli zaidi iliyoandikwa wapeleke tiketi hizo ili wahusika wachukuliwe hatua za kisheria ikiwamo kufutiwa leseni ya usafirishaji.

Alisema abiria hapaswi kulipa nauli nje ya ile iliyotangazwa na Sumatra na msafirishaji anatoza zaidi anashiriki kitendo cha wizi.

Naye Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Tabora, Emmanuel Nley, aliwataka abiria wanaokuwa katika magari ya abiria kutoa taarifa kwa askari wa usalama barabarani pindi wanapokuwa wamezidishiwa nauli ili hatua zichukuliwe ikiwamo kurudishia fedha zao.

## Lowassa afunguka

INATOKA UK. 2

alidai Lowassa aliomba kurudi CCM na walimjadili kwa saa nne.

Alisema alifika kwenye Ofisi za CCM Ijumaa kwenye vikao vya uongozi vilivyokuwa vikiendelea na kueleza uamuzi wake na kwa kuzingatia taratibu alizoeleza, waliamua kumpokea.

Lowassa ambaye ni Waziri Mkuu wa kwanza kuhamia upinzani katika historia ya Tanzania, alitangaza kujiengua CCM Julai 28, baada ya jina lake kushindwa kupenya katika majina matano yaliyoteuliwa na Kamati Kuu ya CCM, kuwania urais katika uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba 25, 2015.

Katika uchaguzi huo, Lowassa aligombea nafasi ya urais kupitia muungano wa vyama vinavyounda Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa) ambavyo ni Chadema, CUF, NCCR Mageuzi na NLD na kupata kura 6,072,848 (sawa na asilimia 39.97) akiwa nyuma ya Dk. Magufuli aliyetangazwa mshindi kwa kupata kura 8,882,935 (asilimia 58.46).

Lowassa alitangaza kukihama chama hicho, alinukuliwa akisema: "Kikatiba, Kamati ya Maadili ya CCM iliyokata jina langu na majina mengine, haina madaraka ya kuchuja na kupendekeza majina miongoni mwa wale wanaoomba kugombea urais kupitia CCM, lakini ilifanya hivyo."

## Watumia spika za masikioni

INATOKA UK. 3

vizuri, tuwe makini katika hilo kwa kuwa linachangia ukosefu wa usikivu, hivyo tuchukue tahadhari," alisema.

Mwalimu alibainisha kuwa inakadiriwa zaidi ya asilimia tano ya watu dunia (sawa na watu milioni 466) wana ukosefu wa usikivu. Kati yao, milioni 432 ni watu wazima na milioni 34 ni watoto.

Alisema ifikapo mwaka 2050, zaidi ya watu milioni 900 watakuwa na changamoto ya ukosefu wa usikivu duniani.

Alisema wagonjwa waliohudumiwa katika Idara ya Masikio, Pua na Koo ya MNH kati ya Novemba mwaka jana na Januari mwaka huu ni 5,959 na kati yao, 454 (asilimia nane) walikuwa na ukosefu wa usikivu.

Alisema katika kukabiliana na changamoto hiyo, serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwamo tiba kwa wagonjwa wenye ukosefu wa usikivu.

Alisema mwaka jana, wagonjwa 117 walipatiwa vifaa vya kukuza mawimbi ya sauti na 43 walifanyiwa upasuaji wa kuziba tundu la ngoma ya sikio.

Mwalimu alisema kwa mwaka huu, kipaumbele chao ni kuboresha huduma za usikivu katika hospitali za rufani kwa kuwa bado zina changamoto.

"Hii changamoto tumeiona, tutahakikisha hospitali za rufani za mkoa zinakuwa na daktari bingwa wa masuala ya pua, masikio na koo na vifaa vinakuwapo ili viwasaidie katika utendaji wao wa kazi," alisema.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Makwaiya Makani, alisema kuwa juzi walianza kutoa huduma ya usikivu na jumla ya wananchi 264 walijitokeza. Kati ya 172 walihitaji uchunguzi wa kusikia na 64 walikutwa na matatizo ya usikivu na wamepatiwa rufani ya matibabu.

HABARI KITAIFA

# Viwanda 13 kujengwa Pwani

**Na Mary Geofrey,** PWANI

VIWANDA vipya 13, vikiwamo vya kutengeneza betri za magari, bidhaa za ngozi, saruji, mabehewa ya treni na vyombo vya plastiki, vinatarajiwa kujengwa katika Mkoa wa Pwani.

Mkuu wa Mkoa huo, Evarist Ndikilo, aliwaambia waandishi wa habari mwishoni mwa wiki kuwa, wawekezaji kutoka China wako tayari kuanza kazi na wakati wowote watakabidhiwa maeneo kwa ajili ya viwanda hivyo.

Alisema katika kikao walichoketi na viongozi wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Kituo cha Uwekezaji (TIC) na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, walikubaliana kuwapa wiki mbili wawekezaji hao ili kukamilisha taratibu za uwekezaji katika mamlaka nyingine za nchi.

"Kwa mara nyingine, mkoa wetu umewapata wawekezaji wapya ambao wanataka kuwekeza kwetu na tayari wamejipanga kuwekeza katika viwanda mbalimbali 13, mtaji wanao, wako tayari kuanza kazi hata kesho. Naagiza kila idara ifanye kazi yake ili hawa wawekezaji tusiwakose," Ndikilo alisema.

Alisema kuwa, katika kikao hicho cha zaidi ya saa sita, walikuwa wakijadili kuhusu ardhi itakayotumika kwa uwekezaji huo, akibainisha kuwa kuna eneo la Mlandizi lenye hekari zaidi ya 5,000 na halijaguswa, na eneo la Kibaha, ambalo watapewa wawekezaji hao.

"Vilevile, tumejadili mambo mengi kuhusu aina ya uwekezaji mkubwa unaotaka kufanyika, sote tumeridhia namna walivyojipanga, wamekuja na mitaji mikononi na aina ya bidhaa na huduma watakazozalisha, wanataka kuhamisha teknolojia kutoka China kuja Tanzania. Ndiyo maana nimetoa wiki mbili majibu yapatikane hawa wawekezaji waanze kazi," Ndikilo alisema.

Alisema serikali inataka kuipeleka nchi katika uchumi wa kati kwa kutegemea viwanda, hivyo mkoa huo hautawavumilia watendaji watakaojaribu kukwamisha juhudi hizo.

"Tukiona watu wenye nia ya kuanzisha viwanda wanasumbuliwa, hatuwezi kukaa kimya. Taratibu zote wamefuata, lakini ikionekana mkoa wangu ndiyo kikwazo sitakubali," Ndikilo alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa TIC, Geofrey Mwambi, alisema kazi ya kuleta wawekezaji ni ya serikali, hivyo haiwezi kuwakwamisha wanaosaidia juhudi hizo za kutafuta wawekezaji kuja nchini.

"Hawa ni wa mwanzo tu, wapo wengi, kati ya hao wawekezaji 13, tayari wawekezaji sita wameshakuja na vifaa vyao wanasubiri kupewa ruhusa waanze kazi. Kuna viwanda vya betri za magari, bidhaa za ngozi na mabehewa ya treni," Mwambi alisema.

# Michezo ya kubahatisha yaipa bilioni 80/- Hazina

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU kukiwa na pendekezo la kuzuia michezo ya kubahatisha nchini, imeelezwa kuwa sekta hiyo ilichangia Hazina ya Serikali Sh. bilioni 78 katika mwaka wa fedha uliopita (2017/18).

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha nchini, James Mbalwe, alisema Dar es Salaam jana, kuwa katika mwaka huu wa fedha, sekta hiyo inakadiriwa kuchangia zaidi ya Sh. bilioni 96 kwenye hazina ya nchi.

"Kwa hiyo, sekta hii ikisimamiwa vizuri, inaweza kutoa mchango mkubwa kwenye uchumi wa nchi yetu," Mbalwe alisema.

Mbali na mapato hayo ya mabilioni ya shilingi, kiongozi huyo wa bodi alisema kampuni mbalimbali za michezo hiyo zimewekeza mabilioni ya shilingi kama mtaji.

Alisema Watanzania takribani 20,000 pia wamepata ajira za moja kwa moja kutoka kwenye kampuni hizo.

Mbalwe alisema kuwa pamoja na uchanga wa sekta hiyo na bodi yenyewe, sekta hiyo imeweza kutoa mchango mkubwa kwenye mapato ya serikali.

Alisema bodi iko chini ya Wizara ya Fedha na Mipango na ni taasisi ya umma, hivyo muundo wake uko kama yalivyo mashirika mengine ya umma ikiwa na bodi ya wakurugenzi ambayo inateuliwa na Waziri wa Fedha na Mipango, huku Mwenyekiti na Mkurugenzi Mkuu wakiteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

"Hivyo, bodi hii iko kisheria, ni chombo kinachofanya kazi kwa mujibu wa sheria ya nchi na kwa maslahi mapana ya taifa," alisema.

Mbalwe aliongeza kuwa, katika jitihada za kuongeza ufanisi katika ukusanyaji mapato, bodi imeshaanza kujenga mfumo wa Tehama utakaotumika kukusanya mapato yatokanayo na uendeshaji wa biashara ya michezo ya kubahatisha.

Alisema bodi itakuwa na mfumo mmoja wa kielektroniki utakaounganishwa katika mifumo ya kielektroniki inayotumiwa na waendeshaji, hivyo kuongeza ufanisi na usimamizi katika kukusanya mapato ya serikali.

Bodi ya Michezo ya Kubahatisha ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 4 ya Mwaka 2003 (Gaming Act No. 4 of 2003) ambayo inarasimisha uwapo wa sekta ya michezo ya kubahatisha nchini.

Hivi karibuni, baadhi ya wadau wakiwamo viongozi wa dini, waliishauri serikali ipige marufuku michezo ya kubahatisha nchini kwa madai kuwa inachochea uvivu miongoni mwa vijana.

Tayari serikali ya Uganda imeshatangaza kuzuia michezo hiyo nchini mwake, ikibainisha kuwa wale wenye leseni za kuiendesha, hawataongezwa muda baada ya muda wa leseni zao kufika kikomo.



Meneja mradi wa kutokomeza mimba na ndoa za utotoni kutoka Shirika la Agape mkoani Shinyanga la Kutetea Haki za Watoto, Mustapha Isabuda, akizungumza na watoto katika kijiji cha Didia Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini, na kuwataka wayatumie vizuri mabaraza ya watoto kupaza sauti mapema juu ya matukio ya ukatili dhidi yao, ili yapate kuchukuliwa hatua za haraka kabla ya kuwaletea madhara. **PICHA: MARKO MADUHU**

# Wakatisha masomo kwa mimba

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANAFUNZI watatu wanaosoma katika shule za msingi za Kata ya Didia wilayani Shinyanga Vijijini (wawili darasa la saba na mwingine la sita) wamekatishwa masomo yao baada ya kupewa ujauzito.

Wanafunzi hao wamegundulika kuwa na ujauzito mwaka huu na kufukuzwa shule, wawili wakitoka Shule ya Msingi Mwanono na mwingine kutoka Shule ya Msingi Bugisi.

Mmoja kati ya wanafunzi hao alimtaja aliyempa ujauzito na ameshakamatwa, lakini wenzake wamekataa kuwataja wanaume waliowapa ujauzito.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Didia, Jackson Majenga, ndiye aliyeeleza kuwapo kwa changamoto hiyo katika eneo lake wakati wa uundaji wa mabaraza ya watoto ngazi ya vijiji kwenye kata hiyo.

Alisema mwaka huu umeanza vibaya kwa kuwa na mimba kwa wanafunzi hao watatu huku akitahadharisha kuwa huenda zikaongezeka ikiwa hakutakuwa na jitihada za kuzidhibiti.

Alisema wazazi ndiyo wamekuwa chanzo cha kukithiri kwa mimba kwa wanafunzi kwa kuzuia watoto wao kuwataja wahusika ambao wamewapa ujauzito wakiogopa lawama, hivyo kuikwamisha serikali kumaliza changamoto hiyo kwa kuwafunga jela wahusika.

"Wazazi wamekuwa kikwazo sana kutokomeza mimba hizi za wanafunzi kwa kutokuwa na ushirikiano, na hata huyu mtuhumiwa mmoja ambaye tumemkamata, tunahofia huenda hata asifungwe jela kwa sababu kumekuwa na changamoto ya wazazi kuharibu ushahidi," Majenga alisema.

Mtendaji wa Kijiji cha Mwanono, Masana Kayela, alisema wameanza kuitisha mikutano ya hadhara ili kutoa onyo kwa wanaojihusisha kingono na wanafunzi. Meneja Mradi wa Kutokomeza Mimba na Ndoa za Utotoni wa Shirika la Agape la Kutetea Haki za Watoto mkoani Shinyanga, Mustapha Isabuda, alisema wameamua kuunda mabaraza hayo ya watoto ili kuwasaidia kutoa taarifa mapema za matukio ya kikatili na kuchukua hatua za haraka kabla ya kuleta madhara.

Alisema watoto wanapokutana wenyewe, ni rahisi kuelezana changamoto ambazo huwa zinawakabili, hivyo mabaraza hayo yatakuwa chachu kubwa ya kutokomeza matukio ya ukatili dhidi yao zikiwamo mimba na ndoa za utotoni, ambazo taarifa zake zitakuwa zinawasilishwa na viongozi wao kwa watendaji wa vijiji na kushughulikiwa.

# Mradi wa Sh. milioni 500 watelekezwa, kisa ufisadi

**Na Ibrahim Yassin,** MOMBA

MAFUNDI wanaojenga kituo cha afya cha Kapele wilayani Momba mkoani Songwe, wameacha kazi hiyo wakidai kwanza kulipwa fedha zao.

Fundi mkuu wa ujenzi huo, Briton Mwita, alimweleza mkuu wa mkoa kuwa wameacha familia zao mikoani kwa lengo la kujenga kituo hicho, lakini wanashangaa hawajalipwa fedha zao.

Alisema kwa muda mrefu hawana malipo hali iliyowalazimu kugoma kuendelea na ujenzi.

Vedastus Simpasa, diwani kata ya Kapele, alisema mafundi wana haki ya kugoma na kuhoji kwanini hawalipwi wakati wanaendelea na ujenzi.

Anno Maseta Mganga Mkuu Wilaya ya Momba, alikiri mafundi hao hawajalipwa na kutaka ufumbuzi upatikane.

Kituo hicho kinachojengwa kwa nguvu za serikali iliyotoa Sh. milioni 500 na za wananchi wanaojitolewa nguvu kazi, kipo kwenye hatihati baada ya mafundi kugoma kuendelea na ujenzi wakishinikiza kulipwa fedha madai yao ya muda mrefu. Ujenzi wa kituo hicho cha afya unafanywa baada ya wananchi kuuanzisha kwa nguvu zao na serikali ikiweka mkono wake kwa kutoa milioni 500 ili wakazi wa eneo hilo waondokane na adha ya kufuata tiba Zambia.

Wanakijiji wanatembea kilometa 60 kwenda Zambia kufuata huduma ya matibabu.

Kata ya Kapele yenye wakazi zaidi ya 10,000 imekosa kituo cha kutolea tiba tangu ilipoanzishwa, hali iliyowalazimu wananchi kwa kushirikiana na viongozi wa vijiji na kata kuanzisha ujenzi wa kituo cha afya.

Mbele ya kamati ya ulinzi na usalama ya mkoa wa Songwe, Anneth Simkwai, mkazi wa Kapele, alisema kwa muda mrefu wamekuwa wakifuata huduma Zambia tena wakihatarisha maisha yao njiani.

Alisema taabu kubwa ni kwa wazee, watoto na kinamama wajawazito ambao wengi wao wamekuwa wakikumbwa na mikasa mingi wakiwa njiani kwenda nchi jirani.

Akiwa katika ziara ya kikazi kukagua maendeleo ya ujenzi wa kituo hicho, Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Generali mtaafu Nickodemas Mwangela, alikutana na mabango yaliyosomeka ujenzi umetelekezwa.

Mengine yalisema mafundi hawajalipwa pesa zao, Mkuu wa Mkoa aliwataka Mkuu wa Wilaya na Mganga Mkuu kutoa maelezo.

Mkuu wa Wilaya, Juma Irando, licha ya kukiri uwepo wa mgomo huo alimweleza mkuu wa mkoa kuwa atashughulikia ili ujenzi uendelea.

Brigedia Mwangela kutokana na kupewa maelezo hayo alisema atachukua hatua stahiki kwa wote waliohusika kuhujumu na kuukwamisha mradi huo na kuwataka wahusika kulipa fedha hizo ndani ya siku mbili.

"Nina masikitiko makubwa kutokana na uzembe unaofanywa na watendaji hawa, ngazi ya kata na wilaya, serikali imetoa fedha halafu ujenzi unasimama, lazima nitachukua hatua juu ya hili," alisema Mwangela.

Baada ya mazungumzo, mafundi wamemwahidi Mkuu wa Mkoa kuendelea na ujenzi wakati wakisubiri fedha zao baada ya kuridhishwa na agizo lake watalipwa fedha zao ndani ya siku mbili.



Wafanyakazi wa Kampuni ya Zantel wakifanya usafi katika Soko la Ilala jijini Dar es Salaam, ambapo pia walikabidhi msaada wa vifaa mbalimbali vya usafi kwa uongozi wa soko hilo mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Serikali yapongeza wawekezaji sekta ya elimu

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imewapongeza wawekezaji binafsi katika elimu kwa kuunga mkono juhudi za serikali ya awamu ya tano ambayo imedhamiria kutoa elimu bora kwa kila Mtanzania.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, (NEC), Dk. Athumani Kihamia, wakati wa mahafali ya 10 ya kidato cha sita ya sekondari ya Tusiime yaliyofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam.

Alisema serikali ya awamu ya tano chini ya uongozi wa Rais John Magufuli imedhamiria kuhakikisha vijana wanapata elimu bora kwa manufaa yao na kwa taifa kwa ujumla.

"Tunahitaji vijana wazalendo na wasomi watakaokuwa msaada kwa taifa na watakaosimamia rasilimali za nchi," alisema Dk. Kilahama.

Alieleza kuwa serikali imeweka mikakati muhimu kwa kuwa bila elimu, nchi haiwezi kufikia uchumi wa viwanda kama ambavyo taifa lina maono ya kuivusha Tanzania kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Dk. Kihamia alikumbusha kuwa bila elimu bora taifa haliwezi kuwa na vijana waadilifu wanatambua haki zao na za nchi yao na kwamba ili kulima kisasa na kupata mazao mengi na bora ya kulisha viwanda lazima elimu ipewe kipaumbele.

Mkuu wa shule hiyo, Emil Rugambwa, alisema shule hiyo haichagui wanafunzi ila hupokea watoto wote na kuwaandaa vyema kwenye mitihani.

# Wenye VVU watapata kituo cha tiba, matunzo

**Na Renatha Msungu**

KATIKA kuboresha afya za wananchi na matunzo kwa wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (VVU) katika mji wa Mirerani mkoani Manyara, Benki ya NMB imetoa misaada wa vifaa tiba mbalimbali vyenye thamani ya shilingi milioni 10.

Vifaa hivyo vimetolewa kusaidia kituo cha afya cha Mirerani kwa lengo la kuboresha huduma za afya katika eneo hilo.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Jenesta Mhagama, alivipokea vifaa hivyo wakati wa uzinduzi wa kituo hicho cha afya.

Kituo hicho kitatoa huduma za tiba na matunzo kwa wanaoishi na virusi vya Ukimwi Mirerani.

Waziri Mhagama alisema vifaa tiba hivyo ni muhimu kwa wananchi wakazi wa Mirerani ambao wanashughulika na biashara ya madini ya tanzanite.

Aidha, wanufaika wengine ni pamoja na wilaya jirani za Hai, Arumeru na Simanjiro.

"Tunawashukuru sana NMB kwa vifaa tiba mlivyotukabidhi naamini vitatumika kwa malengo yaliyokusudiwa na vitasaidia huduma za wagonjwa kuwa bora zaidi ikizingatiwa kituo hiki kinahusika katika mapambano dhidi ya Ukimwi," alisema Mhagama.

Mkuu wa Wateja Wakubwa na Serikali wa NMB, Filbert Mponzi, alisema changamoto za sekta ya afya nchini ni jambo linalopewa kipaumbele na benki.

"Tunatambua juhudi za serikali katika kusimamia sekta mbalimbali zikiwamo afya na elimu kwa nguvu zote ikiwamo kuboresha utoaji wa huduma za afya mijini na vijijini na pia mpango wa elimu bure.

Tunaipongeza sana serikali kwa juhudi hizo," alisema Mponzi.

Alisema licha ya serikali kutekeleza wajibu wake, wao kama wadau wanao wajibu wa kuunga mkono juhudi za maendeleo kwa kusaidia jamii kwa kuwa kupitia wao ndio imeifanya NMB kufikia hatua ya ufanisi iliyopo kwa sasa.

Mponzi aliongeza kuwa benki hiyo kwa miaka kadhaa imekuwa ikisaidia miradi mbalimbali ya maendeleo kwa wananchi kwa kujikita zaidi katika miradi ya elimu hasa ununuzi wa madawati na vifaa vya kuezeka na upande wa afya wamechangia vitanda na magodoro.

"Katika kituo hiki cha afya Mirerani tumechangia vitanda vitatu vya kujifungulia,vingine sita na magodoro yake. Vya wagonjwa wa kawaida, mashuka 70 pamoja na vifaa tiba vya kupima kasi ya moyo vikiwa na jumla ya Sh. milioni 10," alisema Mponzi.

# Huduma tiba za VVU kuboreshwa kwa 90%

**Na Mwandishi Wetu,**
ARUSHA

HUDUMA za tiba kwa watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi zimeanza kuboreshwa kufikia asilimia 90 ili idadi hiyo ijue hali zao za maambukizi, waanze kutumia dawa za kufubaza virusi (ARV), na wanaotumia dawa hizo wawe wamefubaza virusi.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, wakati wa ufunguzi kituo cha tiba na matunzo kwa watu wanaoishi na virusi ya Ukimwi (Waviu) katika Mji Mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mwishoni mwa wiki.

Akifafanua alisema hadi kufikia mwakani, asilimia 90 ya watu wawe wanajua hali zao za maambukizi, asilimia 90 ya wanaojua hali zao wawe wameanza dawa za kufubaza virusi (yaani ARV) na asilimia 90 ya wanaotumia ARV wawe wamefubaza VVU.

Alisema pia, Tanzania bila maambukizi mapya ya VVU, bila vifo vitokanavyo na Ukimwi na bila unyanyapaa inawezekana, na hilo ni lengo ifikapo mwaka 2030.

Kituo hicho kimejengwa na Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti Ukimwi (ATF), uliotoa pamoja na mchango wa serikali kupitia bajeti inayoidhinishwa na Bunge na michango ya wadau mbalimbali wanaochangia kupitia mfuko huo. ATF ilitoa Sh. milioni 200 kwa ajili ya ujenzi wa jengo hilo na Sh. milioni 50 kwa ajili ya ununuzi wa samani na vifaa tiba, wakati Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro imechangia Sh. milioni 51.5 katika ujenzi wa kituo hicho.

Aidha, kwa mujibu wa Mkuu wa wateja wakubwa na Serikali wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi, wamechangia vitanda vitatu vya kujifungulia na sita vya wagonjwa pamoja na magodoro yake, mashuka 70 yenye ubora pamoja na vifaa vitano vya kupimia kasi ya moyo vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 10.

"Vifaa hivi tunavyokabidhi ni moja ya ushiriki wetu katika maendeleo ya jamii na sisi kama benki inayoongoza Tanzania tunahakikisha jamii inayotuzunguka inafaidika kutokana na faida tunayopata.

"Kwa maana hiyo tumeamua kushirikiana na kituo hiki cha afya pamoja na jamii yote inayozunguka kituo hiki kuchangia vifaa hivyo," alisema.

Alisema mwaka huu, NMB imetenga zaidi ya Shilingi bilioni moja kwa ajili ya kuchangia maendeleo ya jamii ikiwamo kusaidia sekta ya afya na elimu, kiasi ambacho kinaifanya benki hiyo kuwa ya kwanza katika kuchangia maendeleo kuliko benki yoyote nchini.

"Kiasi hiki kinaweza kuonekana kuwa siyo kikubwa sana, lakini kimekuwa msaada mkubwa kwa jamii hasa katika sekta ya afya na elimu kwa kuwa vifaa vya afya na elimu vimekuwa ni changamoto kubwa katika hospitali na vituo vya afya vingi na shule zetu nchini.

Alisema NMB itaendelea kuunga mkono juhudi za wadau wake wakubwa katika kuhakikisha kuwa changamoto za jamii zinapatiwa ufumbuzi katika kujenga afya bora na elimu bora kwa jamii ya kitanzania.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu, Bunge na Watu wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, akipiga makofi baada ya kuzindua kituo cha huduma za matunzo na matibabu (CTC) Mji mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wanawake CCT wafanya maombezi ya amani

**Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WANAWAKE kutoka Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT), Mkoa wa Arusha wamefanya maandamano na sala maalum kuombea amani ya nchini.

Maandamano hayo yaliyojumuisha makanisa tisa yanayounda CCT mkoani hapa, yalianzia Kanisa la Anglikana la St. James lililopo Kaloleni hadi Kanisa la Christ lilipo Mtaa wa Uzunguni jijini hapa.

Mwenyekiti wa Wanawake CCT mkoani Arusha, Joyce Malima, alisema wanaadhimisha siku hiyo (Ijumaa) ya amani duniani kwa maombi.

"Leo tupo hapa kuadhimisha siku ya maombi ya dunia, ambayo inafanyika kila siku ya Ijumaa ya kwanza ya kila mwezi Machi kwa njia ya kuomba. Wanawake wote tunaungana duniani kote kuomba kwa ajili ya amani na upendo kwa taifa, jamii, familia na kanisa," alisema.

Hata hivyo, alisema ingawa Tanzania ni nchi ya amani, lakini hawawezi kuacha kuiombea ili amani iliyoko iendelee kuwapo daima ili wasijekujitokeza watu wenye hila mbaya ya kutaka kuharibu amani iliyoko.

"Katika maombi yetu hapa tutatoa sadaka ambayo itatumika kwa ajili ya watoto yatima," alisema. Kwa upande wake, Happiness Chale, ambaye ni kiongozi wa Idara ya Wanawake kutoka Kanisa la St. Steven Ngarenaro, alisema wamefanya maandamano hayo kuombea amani ya nchi, wananchi na serikali.

Maadhimisho hayo kwa ngazi ya kitaifa yameadhimishwa katika kanisa la Christ ili kuwajenga wanawake kutoka madhehebu mbalimbali ya Kikristo.

Alisema kwa kuwa wanawake ni walezi wazuri wa watoto na hata kinababa, wanatumia fursa hiyo kuwaombea watoto ili wawe na tabia njema.

Alisema umoja huo utaendelea kuwaimarisha na kuwafanya kuwa wamoja zaidi na hivyo kuliombea taifa na viongozi wake amani ya kudumu na utekelezaji bora wa amani ya nchi.

Akiwasilisha mada katika kongamano hilo, Ofisa Maendeleo ya Jamii kutoka Idara ya Afya ya KKKT, Nosim Peter, alisema kimsingi wazazi ni waelimishaji wa watoto katika masuala ya afya ya uzazi na haki za watoto.

Hata hivyo, alisema kwa hali ilivyo wazazi wengi wanashindwa kutekeleza jukumu hilo ipasavyo kutokana na mambo kadhaa yakiwamo ya kitamaduni, mapokeo, kutokuwa na muda wa kukaa na watoto au wakati mwingine kutokujua.

Alisema ukimya katika masuala ya afya ya uzazi unatoa athari mbaya kwa vizazi vya sasa ambao wapo katika hatari ya kukumbwa na maambukizi ya magonjwa kama vile Ukimwi, mimba za utotoni na utoro shuleni.

Idara ya Afya ya KKKT inatekeleza mradi wa 'Vunja Ukimya' unaolenga kurahisisha upatikanani wa taarifa kuhusu elimu ya afya ya uzazi na huduma mbalimbali kwa watoto na vijana katika hospitali 10 za Selian na Nkoaranga za Arusha, Machame na Marangu mkoani Kilimanjaro, Orkesmet na Haydom za Manyara, Bunda mkoani Mara, Izimbya, Ndolage na Nyakahanga mkoani Kagera.

# Wataalamu wa kilimo wanolewa zao la alizeti

**Na Jaliwason Jasson,**
BABATI

KATIKA kuhakikisha wakulima wanainuliwa kiuchumi kupitia kilimo cha alizeti, Shirika la Farm Africa mkoani Manyara limeanza kuwanoa wataalamu wa kilimo waweze kwenda kwa wakulima na kuwapatia elimu ya kutumia mbegu za kisasa kwa ajili ya matokeo chanya.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki mjini hapa na Meneja Ufundi wa Kilimo kutoka Farm Afrika, Anastasia Mbatia, wakati akizungumza na Nipashe baada ya kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo maofisa kilimo wa kata mbalimbali za Babati na Hanan'g.

Alisema wameamua kuwapatia mafunzo wataalamu hao ili nao waende kuhamasisha kilimo cha zao la alizeti ili wakulima watumie mbegu mpya ya alizeti aina ya Hysun 33 ambayo wanadai inatoa mavuno mengi kuliko mbegu ya zamani ambayo haina tija kwa mkulima.

"Tumeamua kuwapa mafunzo ya kuwajengea uwezo wataalamu wa kilimo kwa kuwa ndio wanaowaamini kuliko mtu yeyote hata kama anauza mbegu wao hawamsikilizi kama wanavyofanya kwa wataalamu wa serikali," alisema.

Aidha, alisema katika uhamasishaji huo wa zao la alizeti hasa mbegu mpya ya Hysun 33, wanaamini wataalamu wakienda wakatoa elimu kwa wakulima itawasaidia kulima kilimo biashara na mkulima atakapopanda eka moja atavuna magunia 16 tofauti na mbegu za asili ambazo walikuwa wanapanda eka moja wanavuna magunia mtatu mpaka manne.

Alifafanua wakulima watakapohamasika na wakalilima zao hilo kwa kuzingatia kanuni bora za kilimo watakuwa wamejihakikishia soko kwa kuwa mahitaji ya alizeti kwa ajili ya kupata mafuta bado ni makubwa na nchi inazalisha asilimia 40 ya mafuta ya kula kutokana na alizeti na bado inaagiza mafuta kwa asilimia 60.

Akizungumza na wataalamu hao mwishoni mwa mafunzo, Meneja Mradi, Tumaini Elibariki, kutoka Farm Africa, alisema wanatarajia kuwafikia wakulima 10,000, Wilaya ya Babati itakuwa na wakulima 3000, Kiteto (3,500) na Hanan'g (3,500).





# DC, wanawake kuienzi familia wenye ulemavu

**Na Godfrey Mushi,** SAME

MAMIA ya wanawake wa Wilaya ya Same mkoani Kilimanjaro, wataadhimisha Siku ya Wanawake Duniani kwa kungana na familia ya Nirenjigwa Joseph, inayoishi katika Kijiji cha Gwang'a, Kata ya Chome, ambayo ina watoto watano wenye ulemavu wa viungo na mtindio wa ubongo.

Kinamama hao wamepanga kwenda kumfuta machozi mama mzazi Nirenjigwa Joseph ambaye ni mwanamke shujaa nchini, kwa miaka zaidi ya miongo mitatu anaishi na watoto wake watano wenye ulemavu huo. Kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, mamia ya wanawake katika wilaya hiyo wamepanga kwenda kumfuta machozi shujaa huyo ambaye kwa miaka mingi amewatunza watoto wake bila ya kuwadhuru wala kusikitika.

Nirenjigwa ni shujaa wa Tanzania, kwa sababu ya utu wake na imani aliyonayo dhidi ya watu wenye ulemavu hasa kutokana na desturi ya familia nyingi za Kiafrika kuwa na mawazo potofu kwa walemavu ambao ni waathiriwa wakubwa wa mateso, unyanyasaji, ubakaji na wengi wao hawathaminiwi, baada ya kuzaliwa ikilinganishwa na wasiokuwa na ulemavu.

Mkuu wa Wilaya, jana alithibitisha kwamba moja ya shughuli za kijamii ambazo zitafanyika kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani ni kuifariji familia hiyo na kukabidhi jiko la kisasa lenye miundombinu yote kwa ajili ya kuwahudumia vijana hao wenye ulemavu.

"Jumamosi Machi 9, tutakwenda katika Kijiji cha Gwang'a, Kata ya Chome mahali pale tutakwenda kwa mama mwenzetu, mwanamke shujaa ambaye alijaliwa kupata watoto watano wenye ulemavu na amewalea mpaka wamekuwa watu wazima bila kuona huzuni, kwa furaha zote na upendo kamili."

Aliongeza: "Huu ni ushujaa wa ajabu, wakati fulani mwanamke akipata mtoto mmoja wa namna hiyo tu anapata shida, anasononeka, anamhuzunikia Mungu lakini yeye hayuko hivyo, tunatamani kwenda kumtia moyo." Alisema kutakuwa na matukio mbalimbali na mojawapo ni kukabidhi jiko ambalo Isabela Mwampamba kwa kushirikiana na ofisi yake ya Upendo Foundation watalikabidhi.

Vijana hao watano wenye ulemavu waliozaliwa na Nirenjigwa ni Joseph Amini (38), Nafikahedi (33), Wedieli (30), Gadson (28) na Julius (25) ambao wote ni walemavu wa viungo wanaotembea kwa kutambaa.

Kwa mujibu wa Senyamule, wakiwa katika familia hiyo, watakabidhi vifaa kwa ajili ya kujenga uzio wa nondo kwa ajili ya vijana hao wanapocheza, wasicheze wakadondokea nje ya nyumba yao. Pia kutakuwa na kazi ya kujengea ngema zisidondokee nyumba yao na kuipamba nyumba yao kwa rangi za kupaka.

"Tunawakaribisha wadau wa maendeleo kwa michango ya rangi, saruji, mchanga, nondo na vifaa vingine vya ujenzi ili tuweze kuweka mazingira rafiki ya kuishi kwa vijana hao. Tunataka kuifanya siku kuu ya wanawake kuwa ya kihistoria namna inavyoadhimishwa na wengine," alisisitiza Mkuu huyo wa Wilaya. Mara kadhaa jamii ya watu wenye ulemavu imekuwa ikipaza sauti ikitaka serikali kuu itoe maelekezo kwa halmashauri za wilaya nchini kufanya zoezi la utambuzi wa watu wenye ulemavu kila kijiji au mtaa.

Familia hiyo ilianza kupata kupata matumaini mapya mwaka 2012, baada ya baadhi ya wadau kuanzisha kampeni maalum ya kuwajengea uzio kwenye makazi yao ili kuwaepusha na ajali mbalimbali wanazozipata kutokana na mazingira wanayoishi na ulemavu walionao.

Mama wa familia hiyo, amejaliwa kupata watoto wanane, lakini watano kati yao wana ulemavu wa mtindio wa ubongo na viungo, huku wakitegemea huduma kutoka kwa mama pekee na kwa muda mrefu wamekuwa wakikosa huduma za msingi, lakini wakijeruhiwa mara kwa mara kwa kuanguka kutoka mlimani ilipo nyumba yao.



Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, akiongoza wananchi kuvunja choo kilichojengwa katika eneo la chanzo cha maji cha Shiri-Njoro, kinachodaiwa kuuzwa kinyemela kwa mwekezaji ambaye ameanza kufanya shughuli katika eneo la hifadhi ya chanzo cha maji. DC huyo aliagiza Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (Takukuru) wilayani humo kuwachunguza. **PICHA: JAMES LANKA**

# Benki yawatunuku wamachinga wenye vitambulisho vya serikali

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

WAFANYABIASHARA wadogo waliochukua vitambulisho vilivyoandaliwa na serikali kwa ajili ya kuwatambua na kuhakikisha wanafanya shughuli zao bila kubughudhiwa 'wamelamba dume' baada ya Benki ya CRDB kutangaza itashusha neema ya mikopo ya masharti nafuu kwao.

Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema benki hiyo kwa sasa iko kwenye hatua za mwisho kuhakikisha wafanyabiashara wote waliopewa vitambulisho vya wajasiriamali wanapatiwa mikopo ya masharti nafuu, ili kukuza mitaji yao na kuwasukuma kutoka walipo kuelekea kwenye mitaji ya kati.

Alikuwa akizungumza jana katika kongamano la siku moja lililowashirikisha wafanyabiashara wa Mkoa wa Kilimanjaro na wataalamu kutoka benki hiyo.

"Tupo kwenye hatua za mwisho za kuhakikisha wafanyabiashara wote waliopewa vitambulisho na Rais John Magufuli wanapewa mikopo yenye masharti nafuu ili kuzipanua biashara zao," alisema Nsekela.

Aidha, CRDB inaamini kuwa baada ya kuzisikiliza changamoto zinazowakabili wafanyabiashara hao, wamegundua hata hivyo bado wanahitaji elimu ya kitaalamu ya manna bora ya kufanya biashara zao ili kuongeza kipato.

Wakati anafungua kongamano hilo, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Ana Mghwira, alisema umefika wakati watendaji wa taasisi za kifedha kuwa msaada wa kwa jamii katika kutoa huduma bora na kwa uharaka zaidi.

Uamuzi wa kutoa vitambulisho hivyo kwa kila mkoa na kila mfanyabiashara mdogo nchini, ulifanywa Desemba 10 mwaka jana na Rais John Magufuli, wakati wa mkutano wake na watendaji wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na wakuu wa mikoa yote nchini.

## Kanda zaidi wazalisha kahawa zaibuliwa

**Na Mary Mosha,** HAI

BODI ya Taasisi ya Utafiti wa Kahawa nchini (TaCRI), imeridhia kuongezwa zaidi kwa kanda tano za kisekta za utoaji wa miche bora ya mibuni katika mikoa yenye uhitaji mkubwa wa uzalishaji wa kahawa.

Mwenyekiti wa bodi ya taasisi hiyo, Aloyce Mdalavumaili, alisema lengo ni kuhakikisha tatizo la uhaba wa mbegu za mibuni linakwisha na kwamba wameongeza idadi ya kanda kutoka sita hadi kufikia 11.

"Lengo letu ni kuweza kumfikia mkulima kwa ukaribu zaidi, tumepokea changamoto ya kuwapo kwa uhitaji mkubwa wa miche na katika mkutano wetu mkuu, tumejadiliana namna ya kukidhi hitaji hilo la mkulima," alisema.

Mdalavuma alisema kama ilivyo kwa mazao mengine ya kimkakati, serikali haina budi kuingiza nguvu zake katika utafiti ili iweze kubadilisha aina ya miche na kuachana na ya zamani.

"Tayari tumefanya mazungumzo na serikali kuu na imeshatoa maelekezo juu ya kila halmashauri kuzalisha miche 200,000 itakayosaidia wananchi kupata miche bora yenye tija na ubora, lakini ubora haupatikani bila kuimarisha utafiti," alisema.

Katika mkutano huo, mwakilishi wa wakulima wa kahawa katika Mkoa wa Kigoma, Yahaya Omary, alisema licha ya wananchi wengi kupata elimu ya kutosha juu ya ujio wa mbegu bora ya zao la kahawa, lakini bado wanakabiliwa na changamoto ya kukosekana kwa miche hiyo.

"Kule kwetu Kigoma imefikia hatua ukiotesha miche unailinda shambani, kwa sababu baadhi ya watu wasiowaaminifu wamekuwa waking'oa na kwenda kuiotesha mashambani mwao. Hali hii inaonyesha kila mmoja alivyoelimika, kwa hiyo tunaiomba serikali kuunga mkono jitihada hizo kwa hali na mali," alisema Omary.

Taasisi hiyo tayari imegundua mbegu mpya za zao hilo ambazo ambazo zinavumilia ukame na zile zinazovumilia magonjwa yatokanayo na mazingira ya kilimo cha kahawa.

Nipashe
# Spotika
NIPASHE JUMATATU MACHI 4, 2019



ZIJUE DAKIKA ZA HATARI UNAPOIVA YANGA UK.18

## WAMEKUBALI...



Ivan Rakitic akiifungia Barcelona kwenye mechi ya El Clasico, huku Sergio Ramos akijaribu kuokoa bila mafanikio katika mechi hiyo ya La Liga iliyopigwa katika Uwanja wa Santiago Bernabeu juzi na Real Madrid kulala kwa bao 1-0. Hiyo ni mechi ya pili mfululizo kuchapwa ndani ya wiki moja nyumbani baada ya Jumatano kukubali kipigo cha mabao 3-0 kwenye Copa del Rey [Kombe la Mfalme]. **HABARI UK. 29**

### ISIKUPITE

LICHA ya Arsenal kushinda 5-1 dhidi ya Bournemouth Jumatano iliyopita, bao hilo moja ililoruhusu ni la 1,000 kwao kufungwa tangu ianze kushiriki Ligi Kuu England, na linaifanya kuwa timu ya nane kuruhusu idadi hiyo ya mabao baada ya Everton, Tottenham, West Ham, Newcastle United, Aston Villa, Southampton na Liverpool.

MICHEZO



Alisson

# USAJILI MPYA ULIOLIPA ENGLAND MSIMU HUU

**LONDON,** England

TAYARI tumeshapita nusu ya pili ya msimu wa 2018/19 kwenye Ligi Kuu ya England, na hapa tunaangalia jinsi usajili wa wachezaji wapya ulivyozisaidia klabu zao.

Kwa sasa fedha nyingi zimetumika kwenye Ligi Kuu England, kuna wengine wameshindwa kufikia malengo. Lakini tumewaona wachezaji wazuri zaidi waliosajiliwa msimu huu, wote katika klabu sita bora na zile zilizopo katikati ya msimamo.

Hivyo, hapa tunaangalia usajili wa wachezaji watano bora kwenye Ligi Kuu ya England msimu huu ambao wamekuwa msaada mkubwa kwa klabu zao hadi sasa.

**5. Raul Jimenez**

Raul Jimenez alisajiliwa na Wolverhampton Wanderers kwa mkopo kutoka Benfica kipindi cha majira ya joto. Jimenez ameonekana kuwa msimu huu ni mzuri zaidi kwake, lakini bado hapewi nafasi kubwa. Yeye amekuwa akizidiwa kete na wachezaji kama Ruben Neves, Diogo Jota na wengineo, wakati Jimenez amebakia kutokuwa muhimu kwa kikosi hicho cha kocha, Nuno Espirito Santo.

Kwenye Ligi Kuu msimu huu, Jimenez amefunga mabao 10 na kutoa pasi za mwisho tano. Uwiano wake ni kwamba amefunga bao katika kila dakika 221.

`Fabinho alisajiliwa na Liverpool kutoka Monaco kwa ada ya uhamisho ya euro milioni 45. Mwanzoni mwa msimu huu, alikuwa akipewa nafasi nyingi zaidi ya kucheza, lakini mambo yamebadilika na ameizoea ligi Kuu ya England. Anacheza vizuri kwa sasa na inaonekana ni usajili mzuri zaidi kwa kocha, Jurgen Klopp.

Fabinho ni mchezaji kiraka anayeweza kucheza kwenye nafasi nyingi. Anaweza kucheza kulia, katikati na sehemu yeyote kwenye nafasi ya kiungo na hilo linamfanya kuwa mchezaji muhimu kwa Liverpool. Amekuwa na mfanano na Jordan Henderson kwa jinsi anavyocheza na kutawala mpira kwa kutoa pasi nyingi. Kwa umri, nyota huyo wa timu ya Taifa ya Brazil atakuwa na nafasi zaidi ya kuichezea Liverpool msimu huu.

Kwa takwimu kwenye Ligi Kuu msimu huu, Fabinho amefunga bao moja na ametoa pasi za mwisho mbili. Amegusa mpira kwa usahihi mara 87 kwa mchezo na pasi za uhakika kwa asilimia 85.

**3. David Brooks**

David Brooks alisajiliwa na Bournemouth kutoka Sheffield United kwa euro milioni 10. Usajili huu umeonyesha jinsi gani Bournemouth walivyopata mchezaji bora. Kwa euro milioni 10, Brooks ameonekana kuwa mchezaji muhimu zaidi kwa kikosi hicho.

Brooks alitokea kwenye ligi ya daraja la chini na ilionekana kwamba angepata wakati mgumu wa kuzoea ligi hiyo, lakini hakuhitaji kupata muda zaidi wa kuzoea. Kwa sasa ni mchezaji muhimu zaidi kwa kocha, Eddie Howe ambaye ameitengeneza vizuri safu ya ushambuliaji.

Katika umri wake wa miaka 21, amekuwa mchezaji muhimu wa Bournemouth na amekuwa mmoja wa wachezaji muhimu na kucheza soka la burudani msimu huu.

Brooks amefunga mabao sita na kutoa pasi za mwisho nne kwenye Ligi Kuu msimu huu. Ana uwiano wa kugusa mpira mara 51 kwa mchezo na amekuwa na pasi za uhakika kwa asilimia 72.

**2. Lucas Torreira**

Lucas Torreira alisajiliwa Arsenal kutoka Sampdoria kwa ada ya uhamisho ya euro 26. Na usajili huu umeonekana kuwa muhimu zaidi kwa Arsenal, kwa kuwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay amekuwa mmoja wa wachezaji muhimu zaidi katika safu ya ulinzi kwenye Ligi Kuu. Ameizoea haraka ligi hiyo ya England na ni aina ya mchezaji ambaye Arsenal ilikuwa ikimhitaji.

Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 23, amekuwa mfano mzuri kwa wachezaji wenzake hasa kutokana na uwezo wake dimbani. Uwezo wake wa kutoa pasi kwa safu ya ushambuliaji umemfanya kuwa mmoja wa wachezaji muhimu zaidi hapo kwenye dimba la Emirates. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay anaonekana kufiti kwenye mfumo wa kocha, Unai Emery.

Torreira msimu huu amefunga mabao mawili na kutoa pasi za mwisho mbili. Uwiano wake wa kugusa mpira ni mara 79 kwa mchezo na uhakika wa pasi zake ni kwa asilimia 88.

**1. Alisson Becker**


Alisson Becker alisajiliwa na Liverpool kutoka AS Roma kwa ada ya uhamisho ya euro milioni 67. Mchezaji huyu wa kimataifa wa Brazil aliwasili hapo Anfield kwa matarajio makubwa na hadi sasa amelionyesha hilo dimbani. Amekuwa mchezaji muhimu kwa Liverpool msimu huu.

Mchezaji huyu amecheza mechi nyingi zaidi bila nyavu zake kutikiswa kwenye Ligi Kuu msimu huu. Ingawa amefanya makosa mengine, katika mchezo dhidi ya Leicester City na Manchester United, lakini hayo yote yanaweza kusamehewa kutokana na ukweli kwamba amekuwa msaada mkubwa zaidi kwa Wekundu hao wa Anfiled msimu huu.

Alisson msimu huu ameokoa hatari 56 na kucheza mechi 15 bila kufungwa. Ana uwiano wa kuokoa hatari kwa asilimia 2.1 kwa mchezo.

**JE, WAJUA?**

ARSENAL ni timu pekee Ligi Kuu England ambayo imeshindwa kumaliza mechi bila kutoruhusu bao ('clean sheet') ugenini hadi sasa msimu huu.



# MICHEZO

## NJE YA UWANJA




## IBRAHIMOVIC AMWONYA MBAPPE

**PARIS,** Ufaransa

Zlatan Ibrahimovic amemwonya mshambuliaji wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe, kutobweteka na sifa zinazozidi kumzunguka kwa sasa.

Mbappe, 20, amefurahia kukua kwa kiwango chake katika misimu ya hivi karibuni, akiwa sehemu ya mafanikio makubwa ya Ufaransa kutwaa Kombe la Dunia nchini Urusi mwaka jana, huku akishinda tuzo ya Kinda Bora ['Kopa Trophy'] Desemba mwaka jana – ambayo hutolewa kwa mchezaji bora duniani mwenye umri chini ya miaka 21.

Ibrahimovic, ambaye alifurahia miaka minne ya mafanikio akiwa PSG kati ya mwaka 2012 na 2016, amekuwa akivutiwa na mafanikio ya Mbappe hadi sasa, lakini amemwonya namna ya kutoridhika na tuzo ambazo bado zitaendelea kuja kwake.

"Mbappe ni wa kushangaza," mshambuliaji huyo wa LA Galaxy aliambia tuvuti ya klabu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu ya Marekani, MLS.

"Bado ni kinda, ametwaa mataji mazuri hadi sasa na bado anaendelea. Anafanya kazi nzuri na ataendelea kuifanya kazi.

"Anatakiwa tu kuendeleza mtazamo wake, hata kama sifa zinamzunguka na kila kitu kinatokea. Endelea tu kuwa na mtazamo, jifue sana na atafanya vizuri zaidi."




Straika wa Simba, Emmanuel Okwi (jezi Na. 7), ambaye misimu miwili mfululizo yumo kwenye orodha ya wachezaji waliofunga 'hat-trick' Ligi Kuu Tanzania Bara.

# HAT-TRICK YA NNE YATIKISA LIGI KUU

**Na Adam Fungamwangwo**

STRAIKA wa Ruvu Shooting, Fully Maganga, ameingia kwenye kitabu cha kumbukumbu za Ligi Kuu Tanzania Bara kwa wachezaji waliofunga mabao matatu kwenye mechi moja, maarufu 'hat-trick', alipofanya hivyo Jumamosi katika Uwanja wa Mabatini, Mlandizi mkoani Pwani.

Maganga, straika wa zamani wa JKT Ruvu (sasa JKT Tanzania) na Mgambo Shooting, alifunga mabao hayo dakika 12, 28 na 69, akiisaidia timu yake kuichapa timu ngumu ya Mwadui mabao 6-2 kwenye moja ya mechi za Ligi Kuu.

Mabao mengine ya Ruvu yalifungwa na mchezaji wa zamani wa Yanga, Emmanuel Martin na Tumba Swedi.

Mabao ya Mwadui yalifungwa na straika wake hatari, Salum Aiyee na Wallace Kiango.

Rekodi zinaonyesha kuwa hii ni 'hat-trick' ya nne kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa msimu huu.

Hata hivyo, bado haijafikia rekodi ya msimu uliopita, kwa kuwa msimu mzima zilifungwa 'hat-trick' tano.

Kinara wa 'hat-trick' msimu uliopita alikuwa ni Obrey Chirwa akiwa anaichezea Yanga, akifunga mara mbili kwenye mechi dhidi ya Mbeya City, timu yake ikishinda mabao 5-0, pia Njombe Mji, akiibeba timu yake kushinda mabao 4-0.

Mwingine ni Marcel Kaheza akiwa Majimaji kwa sasa akiichezea AFC Leopards ya Kenya akitokea Simba kwa mkopo, alifunga 'hat-trick' akiifanya timu yake kuichapa Ruvu Shooting mabao 3-0.

Shaaban Idd, straika wa Azam ambaye kwa sasa anacheza soka la kulipwa nchini Hispania alifanya hivyo wakati Azam ikiifunga Prisons mabao 4-0.

Emmanuel Okwi pia alifanya hivyo kwenye mechi dhidi ya Ruvu Shooting Simba ikishinda mabao 7-0.

Wafuatao ni wachezaji waliofunga 'hat-trick' mpaka sasa kwenye Ligi Kuu.

**1. Alex Kitenge-Stand United**

Straika huyu wa Stand United raia wa Burundi alikuwa wa kwanza kufunga 'hat-trick' msimu huu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Alifanya hivyo Septemba 16 mwaka jana kwenye mechi ambayo alicheza dhidi ya Yanga dakika ya 15, 58 na 90 kwenye Uwanja wa Taifa dhidi ya Yanga. Hata hivyo, timu yake ilichapwa mabao 4-3 kwenye mechi hiyo.

**2. Emmanuel Okwi-Simba**

Okwi ndiye mchezaji pekee mpaka sasa ambaye alikuwamo kwenye orodha ya waliofunga 'hat-trick' msimu uliopita, lakini pia msimu huu.

Rekodi zinaonyesha kuwa msimu uliopita 'hat-trick' yake aliipata kwenye mechi dhidi ya Ruvu Shooting, na msimu huu pia aliipata kwenye mechi dhidi ya timu hiyo hiyo Oktoba 28 mwaka jana, dakika ya nane, 53 na 77, akiisaidia timu yake ya Simba kupata ushindi wa mabao 5-0 kwenye Uwanja wa Taifa.

**3. Salum Aiyee-Mwadui FC**

Huyu ni straika chipukizi anayekuja juu kwa sasa akiwa kinara wa upachikaji mabao mpaka sasa akiziona nyavu mara 13.

Alifanya hivyo Januari 6, mwaka huu, kwenye mechi dhidi ya Kagera Sugar timu yake ikishinda mabao 4-0, akitupia dakika ya 48, 68 na 83.

**4. Fully Maganga-Ruvu Shooting**

Ameingia kwenye orodha hiyo baada ya kufunga 'hat-trick' Jumamosi dhidi ya Mwadui FC na kufanya Ligi Kuu ya Tanzania Bara kuwa na 'ha-trick' nne mpaka sasa msimu huu.

# Timu 5 zinazoweza kubeba Uefa msimu huu

**LONDON,** England

LIGI ya Mabingwa Ulaya imefikia kwenye hatua ya mtoano wa timu 16-bora, na sasa zimebaki mechi za pili kwa timu zilizofuzu.

Fainali ya michuano hii itapigwa jijini Madrid nchini Hispania Mei mwaka huu. Mwezi huu wa Machi na Aprili ndio utakuwa unaonyesha timu zitakazoweza kufuzu kwa hatua ya robo fainali.

Katika mechi za kwanza za raundi hii, tumeshuhudia mambo mengi ya kushangaza. Juventus ilikumbana na kipigo pale Madrid na Dortmund ikichapwa kule England, hivyo nafasi zao za kufuzu hatua inayofuata ni finyu.

Baada ya kushinda mara tatu mfululizo Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya, Real Madrid walianza vibaya msimu huu, lakini sasa wanaonekana kurudi kwenye mstari wao.

Michuano ya Ligi ya Mabingwa msimu huu inaonekana kuwa na ushindani wa hali ya juu, na makala haya yanakuchambulia timu ambazo zinaonekana kuwa na nafasi kubwa ya kulibeba taji hilo msimu huu.

**5. Liverpool**

Bila shaka yoyote, Liverpool inacheza soka la kuvutia katika historia yake pale Anfield. Vijana hao wa kocha Klopp wamewapa matumaini makubwa mashabiki wao kwamba wanaweza kupigana na kufika mbali, kuanzia kwenye Ligi Kuu hadi kwenye michuano hii ya Ulaya. Kwa sasa wapo kwenye mbio moja za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu ya England pamoja na vijana wa Manchester City wanaonolewa na kocha Pep Guardiola.

Lakini je, changamoto za mbio za ubingwa wa Ligi Kuu England zitaathiri kiwango chao kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya? Mwaka jana walikuwa washindi wa pili nyuma ya Real Madrid waliolitwaa taji hilo.

Ingawa kiufundi Liverpool wana nafasi angalau ya kufuzu hatua ya robo fainali.

**4. Paris Saint-Germain**

Kwa miaka mingi sasa, PSG imeanza kampeni ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa uimara zaidi msimu huu na kuwa na matarajio makubwa ya kufika mbali au kulibeba kabisa kombe hilo. Lakini mara zote huwa haipewi nafasi kubwa kama ilivyo kwa miamba wengine wa Ulaya kama, Madrid, Barcelona, na Bayern. Kipigo cha mabao 6-1 kutoka kwa Barcelona na kichapo kutoka kwa Real Madrid msimu uliopita ilitakiwa kuwa mfano kwa PSG kwamba hawapo kwenye 'levo' moja na timu kubwa kwenye mashindano ya Ulaya.

Lakini mwaka huu, wachambuzi wengi wa soka wamekuwa wakiipa nafasi kubwa PSG hasa baada ya kuanza mchezo wake kwa kuifunga Manchester United.

Huku wakiwa na nafasi kubwa ya kufuzu kwenye hatua ya robo fainali baada ya ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Manchester United mwezi uliopita. Uwapo wa wachezaji kama Neymar Jr na Edinson Cavani, wanaweza kuifikisha mbali PSG, ingawa vijana wa kocha Ole Gunnar Solskjaer wana nafasi pia.

**3. Real Madrid**

Haijalishi Real Madrid wameanzaje msimu huu, lakini bado wana nafasi ya kuweza kuushangaza ulimwengu na kulitwaa taji hili. Hawa wana uzoefu mkubwa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na uzuri ni kwamba wametoka kushinda taji hilo mara tatu mfululizo.

Mchezo wao wa kwanza wa hatua ya mtoano wa timu 16-bora walipata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Ajax pale Amsterdam na sasa wamejiweka kwenye mazingira mazuri.

Ingawa kwa sasa mabingwa hao watetezi wanamkosa Cristiano Ronaldo ambaye alikuwa chachu kubwa ya ushindi wa timu hiyo, lakini bado wana nafasi nzuri ya kuweza kufanya maajabu.

Real Madrid kwa sasa inatafuta rekodi ya kulitwaa taji hilo kwa mara ya nne mfululizo na bila shaka wanaweza kufanya hivyo, kama wakijihakikishia ushindi kwenye mchezo ujao dhidi ya Ajax.

**2. Manchester City**

Vijana hawa wa Pep Guardiola kwa sasa wana safu imara zaidi ya ushambuliaji. Mwaka jana walitolewa na Liverpool waliotinga fainali. Lakini msimu huu Man City inaonekana kuwa na wakati mzuri zaidi wa kufunga mabao. Msimu huu wamefunga mabao 70 kwenye ligi na pia waliwafumua Schalke mabao 3-2.

Bahati kwa Schalke walipata penalti mbili, lakini uwezekano wa kuwazuia kwenye mchezo wao wa pili ni mgumu.

Ingawa Guardiola mwenyewe anaweza asilitambue hili, lakini timu yake inabakia kuwa ni moja ya inayopewa nafasi kubwa zaidi ya kulibeba taji hilo msimu huu.

**1. FC Barcelona**


Wakati Leo Messi mwenyewe aliposema atajaribu kwa hali na mali kuhakikisha wanalibeba taji la Ligi ya Mabingwa msimu huu na kulipeleka pale Camp Nou, baada ya kuishuhudia Real Madrid ikishinda mara tatu mfululizo, ni wazi kwamba Barcelona inabaki kuwa na nafasi kubwa zaidi ya kulitwaa taji hilo msimu huu.

Katika mchezo wa kwanza nchini Ufaransa dhidi ya Lyon, Barcelona ilibanwa kwa kulazimishwa sare ya bila kufungana. Hata baada ya kupiga mashuti 25 kwenye lango la timu hiyo, lakini walishindwa kufunga. Lakini kwa namna yoyote mchezo wa pili utakaopigwa Camp Nou utakuwa mgumu zaidi kwa Lyon.


Yote kwa yote, Barcelona inabakia kuwa timu yenye nafasi kubwa zaidi ya kulitwaa taji hili msimu huu.

## NUKUU


"Lakini tunahitaji wachezaji katika benchi wenye mawazo mazuri na kiwango kizuri, wakati tunapohitaji wachezaji wakutusaidia kipindi cha pili, ama panapotokea majeruhi au wakati wachezaji wanapochoka kwa kubeba majukumu ama kuendelea na uwezo wetu. Na kwa Mesut Ozil, Jumapili (Februari 24, mwaka huu) ilikuwa changamoto nzuri, kama tulivyozungumza kabla, kuwa katika benchi na kutusaidia kama alivyofanya katika dakika 30 za mwisho, ni muhimu zaidi akawamo na kucheza mara nyingine katika kikosi," **Kocha wa Arsenal, Unai Emery, akimzungumzia Mesut Ozil baada ya kuonyesha kiwango dhidi ya Bournemouth.**



"Kama ni klabu isiyo na mtazamo, siwezi kwenda. Nataka kufanya kazi na klabu yenye mtazamo wa juu zaidi, hicho ni kitu cha kwanza. Nataka kuwa na timu ninayoipenda na watu ambao ninaowapenda kufanya nao kazi. Nataka kufanya kazi na watu ambao nitafurahia kufanya nao kazi, ambao naweza kushirikiana nao na kuwa na mawazo sawa. Nilipata kile nilichokitaka nikiwa kule Inter Milan. Kuna klabu kama hizi. Kwa hakika hii ni kitu muhimu zaidi kwa mafanikio ya klabu," **Jose Mourinho akizungumzia klabu atakayoinoa.**



"Hii si nafasi yetu ya mwisho, hili ni jambo muhimu zaidi kwangu. Hii ni nafasi yetu ya kwanza. Huu si wakati wetu pekee wa kuwa mabingwa? Sina uhakika. Tukiwa na nafasi ya kwanza, unaruka na kuangalia namna kazi inavyofanywa. Kuna wakati mambo yanakuwa sawa na wakati mwingine hayawezi kuwa sawa. Hii haitakuwa nafasi yetu ya mwisho, hapana kwa asilimia 100," **Kocha wa Liver, Jurgen Klopp akizungumzia nafasi ya klabu hiyo kutwaa ubingwa.**



# Michezo



Fei Toto akipongezwa na wachezaji wenzake baada ya kuifungia Yanga katika moja ya mechi za Ligi Kuu msimu huu.

# ZIJUE DAKIKA ZA HATARI UNAPOIVA YANGA

**Na Adam Fungamwango**

BAO la dakika ya 75 lililofungwa na Amissi Tambwe, liliifanya Yanga kuondoka na ushindi wa 1-0 dhidi ya Alliance kwenye Uwanja wa CCM Kirumba Jumamosi iliyopita.

Mbali ya ushindi huo kuifanya Yanga kuendelea kuongoza Ligi Kuu ikiwa na pointi 64 na mechi 26 ilizocheza, lakini takwimu zinaonyesha kuwa timu hiyo huwa ni hatari zaidi inapofikia dakika ya 75 na kuendelea.

Makocha wa timu zote ambazo zitakwenda kupambana na Yanga inabidi wafanye kazi ya ziada kuwaambia wachezaji wao hasa mabeki kuwa makini mno inapofikia dakika hizo hadi mechi inapokwisha, kwa kuwa imeonekana kuwa mabao mengi inafunga kuanzia dakika hizo, hasa kwa mechi ambazo kwao zinakuwa ngumu.

Hizi ndizo mechi ngumu ambazo Yanga ilipata mabao yake kuanzia dakika ya 75 na kuendelea...

**1. Yanga 2-0 Mbao (dakika ya 90+2)**

Moja ya mechi ngumu ambazo Yanga iliwahi kukumbana nazo msimu huu ni dhidi ya Mbao kwenye Uwanja wa Taifa, Oktoba 7, mwaka jana.

Dakika ya 16, Rafael Daudi, aliipatia Yanga bao la kwanza. Hata hivyo, wanachama na mashabiki wa Yanga walikuwa roho juu kutokana na Mbao kulishambulia lango la wapinzani wao kama nyuki kiasi cha kurudi nyuma.

Dakika mbili za nyongoza, baada ya dakika 90, Yanga ilifanya shambulizi la kushtukiza na kupata bao la pili lililofungwa na Ibrahim Ajibu kwa 'tik-tak' na kuwa bao la pili lililofungwa mwishoni mwa mchezo na kushinda 2-0.

**2. Yanga 2-1 Kagera Sugar (dakika ya 75)**

Ilikuwa ni Novemba 25, mwaka jana Yanga ilipocheza dhidi ya Kagera Sugar kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba. Yanga ilishinda mabao 2-1. Heritier Makambo akiifungia bao dakika ya 21, lakini Kagera Sugar ilisawazisha kupitia kwa Ramadhani Kapera kwa mkwaju wa penalti dakika ya 32.

Kuanzia dakika ya 75 huwa ni dakika nzuri kwa Yanga, kwa kuwa dakika hiyo hiyo ilipotimia Rafael Daudi aliipatia timu hiyo bao la ushindi na kuifanya kuibuka na ushindi huo.

**3. Yanga 3-1 Prisons (dakika ya 75, 84, 90)**

Hii ni mechi ya aina yake iliyochezwa Desemba 3, mwaka jana kwenye Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya kati ya Prisons na Yanga.

Dakika ya 45, Jumanne El Fadhili alianza kuipatia Prisons bao kwa mkwaju wa penalti.

Ilionekana kama Yanga ingelala kwa bao 1-0 kwenye mechi hiyo, au ikijitahidi sana sare.

Dakika ya bahati kwa Yanga ikaja. Dakika ya 75 ilipata penalti kwa kuwekwa wavuni na Ibrahim Ajibu.

Dakika ya 84, Tambwe aliipatia Yanga bao la pili na straika huyo pia akafunga bao la tatu dakika ya 90, na kuipa ushindi wa mabao 3-1.

**4. Yanga 2-1 Biashara (dakika ya 80)**

Kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, Yanga ilicheza dhidi ya Biashara Desemba 8, mwaka jana na kuondoka na ushindi wa mabao 2-1.

Mazingira ni yale yale. Abdulmajid Mangalo aliipatia Biashara bao dakika ya 37. Hata hivyo, dakika ya 70, Abdallah Shaibu 'Ninja' akaisawazishia Yanga.

Dakika za bahati za Yanga zikafika. Dakika ya 80, Makambo akaipatia timu hiyo bao la pili na kuondoka na ushindi.

**5. Yanga 3-2 Ruvu Shooting (Dakika ya 79, 90+5)**

Ilikuwa moja ya mechi ngumu kwa Yanga, lakini ilitumia dakika zake za bahati kupata ushindi. Ilichezwa Desemba 16, mwaka jana kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Ilianza kwa Yanga kupata bao dakika ya 11 kupitia kwa Tambwe, kabla ya Fully Maganga kusawazisha dakika ya 32.

Feisal Salum 'Fei Toto' akaipatia Yanga bao dakika ya 79, ikiwa tayari dakika za bahati zimeshaingia, lakini Said Dilunga akawasazisha kwa penalti dakika ya 84.

Kwenye dakika ya tano ya nyongeza, huku mwamuzi akijiandaa kumaliza mechi, Makambo akaifungia Yanga bao la ushindi, ngoma ikawa 3-2.

**6. Yanga 1-1 Coastal (dakika ya 76)**

Deus Kaseke aliiokoa Yanga kufungwa dhidi ya Coastal Union kwenye Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga na kuifanya mechi hiyo kumalizika kwa sare ya bao 1-1.


Zilikuwa ni zile zile dakika za bahati za Yanga. Alifunga dakika ya 76, baada ya bao la Haji Ugando dakika ya 30, mechi ikichezwa Februari 3 mwaka huu.

**7. Yanga 1-0 Alliance (dakika ya 75)**

Tambwe aliendeleza bahati ya Yanga kuanzia dakika ya 75, alipofunga bao lililoipa ushindi dhidi ya Alliance Jumamosi kwenye Uwanja wa CCM Kirumba Mwanza.

**NAJUA WAJUA**

SOUTHAMPTON ni timu ya kwanza ya ugenini kuweza kufunga mabao mawili nje ya boksi kwenye Ligi Kuu England, katika Uwanja wa Old Trafford tangu Manchester City ilipofanya hivyo Septemba 2009.



## MAKALA



# SOLSKJAER HANA NJIA MBADALA MAN UTD

**MANCHESTER,** England

WAKATI natazama mechi kati ya Manchester United na Liverpool, kuna picha moja ilikuja katika akili yangu. Picha ya mechi kati ya Manchester United na PSG.

Mechi ambayo ilichezwa pale Old Trafford, ilichezwa kipindi ambacho Manchester United ilikuwa kwenye kiwango bora.

Michezo 11 mfululizo walikuwa wameenda bila kufungwa kwenye michuano yote ambayo Manchester United ilikuwa inashiriki.

Kwa hiyo, watu wengi walikuwa wanaipa nafasi kubwa sana Manchester United kufanya vizuri kutokana na sababu mbalimbali kwa wakati huo.

Ukiachana na kuwa Manchester United ilikuwa imeenda mechi 11 bila kufungwa, PSG iliingia uwanjani ikiwa bila wachezaji wao nyota wawili, Edson Cavani pamoja Neymar.

Kutokuwapo kwa wachezaji hawa wawili lilikuwa pigo kubwa sana kwa PSG kwenye mechi hii.

Na hii ni kwa sababu wachezaji hawa wawili kwa asilimia kubwa huwa ni ufunguo wa ushindi kwa PSG kwa misimu kadhaa.

PSG hii ambayo ilikuwa inaenda uwanja wa nyumbani wa Manchester United uwanja ambao ulianza kuonekana kama 'machinjioni'.

Asilimia kubwa ya mechi hii ilitazamika kwa Manchester United kushinda. Lakini matokeo yalikuwa tofauti kabisa na matazamio ya wengi.

Manchester United ilipoteza mechi hii, na mwanzo wa kupoteza ulianza baada ya Anthony Martial kuumia pamoja na Jesse Lingard.

Walipoumia wachezaji ambao walitakiwa kuja kuziba nafasi zao hawakuweza kufanya kitu ambacho kingekuwa na msaada mkubwa.

PSG waliingia bila ya Cavani pamoja na Neymar, lakini wachezaji waliokuwa wamepewa nafasi kwenye mechi ile waliisaidia PSG.

Pamoja na kwamba hawakucheza katika kiwango kikubwa cha kina Neymar na Cavani, lakini walikuwa na msaada mkubwa wa kuipa matokeo chanya PSG.

Hii yote unaweza ukaijumuisha na kuiweka katika sentensi moja tu, PSG walikuwa na mbadala sahihi kwenye timu kwa hawa wachezaji wawili.

Hiki ndicho kitu pekee na kikubwa ambacho unaweza ukakisema. Hata mahali pa Rabiot hapakuonekana kama kuna shida, kwa sababu tu walipata mbadala.

Wakati mechi inaendelea Martial na Lingard wakaumia, waliosimama kutoka benchini kuja uwanjani hawakuweza kuwa mbadala mzuri.

Mwisho wa siku Manchester United ikapoteza ile mechi tena nyumbani na kuweka mazingira magumu katika mechi ya mkondo wa pili itakayochezwa Paris.

Tuachane na hayo, turudi sasa kwenye mechi kati ya Manchester United na Liverpool. Hii ilichezwa pale pale, ambapo PSG alifanikiwa kupata matokeo chanya.

Na katika mechi ile kulitokea kitu kile kile ambacho kilitokea kwenye mechi dhidi ya PSG, lakini safari hii kikitokea kwa wengine.

Hakuwa Martial na Lingard walioumia kwenye ile mechi, safari hii ilikuwa zamu ya kina Rashford kuumia. Na walipoumia ukawa mwanzo wa Manchester United kutokuwa na uwiano mzuri.

Kwa sababu watu ambao walikuja kuziba pengo la hao wachezaji waliumia hawakuweza kuwa na msaada mkubwa sana wa kubadilisha matokeo kwa kiasi kikubwa cha hali ya juu.

Hawakuwa mbadala sahihi wa wachezaji waliokuwa wameumia kwenye mechi ile. Hii ni picha tosha kuwa kuna kitu kinakosekana.

Pamoja na kwamba Manchester United tangu aondoke Jose Mourinho, imekuwa na matokeo chanya, lakini imekuwa inakosa vitu vichache sana.

Moja ya vitu hivyo ni timu kukosa mbadala sahihi katika nyakati ngumu. Hiki kitu kinaweza kutengenezwa na kocha kwa kuleta watu ambao wanaweza wakawa mbadala sahihi katika maeneo muhimu ndani ya timu, jukumu ambalo anapaswa kulifanya kocha Ole Gunnar Solskjær anayekiongoza kikosi hicho cha United kwa sasa.

NDANI YA 18

MABAO matano kati ya sita Riyad Mahrez aliyoifungia Manchester City hadi sasa kwenye Ligi Kuu England, amefunga wakiwa ugenini.






LIGI ya Mabingwa Ulaya imefikia kwenye hatua ya mtoano wa timu 16-bora, na sasa zimebaki mechi za pili kwa timu zilizofuzu. Fainali ya michuano hii itapigwa jijini Madrid nchini Hispania Mei mwaka huu. Mwezi huu wa Machi na Aprili ndio utakuwa unaonyesha timu zitakazoweza kufuzu kwa hatua ya robo fainali.

**Uk. 16-17**



# REKODI 5 ZA MESSI, ZILIZOMSHINDA CR7

**BARCELONA,** Hispania

LIONEL Messi na Cristiano Ronaldo (cr7), wameonekana kuwa wapinzani wakubwa zaidi kwenye mchezo wa soka kwa kipindi cha muongo mmoja sasa.

Wachezaji hao wawili wamezua gumzo kubwa duniani kutokana na uwezo wao na kuleta mjadala wa nani bora zaidi kati yao.

Wote wawili Messi na Ronaldo wanaonekana huwa wanatengeneza rekodi kila wanapogusa mpira, na kuonekana kama ni wanaoshindana katika kuweka rekodi mpya.

Makala haya yanaangalia rekodi tano zilizowekwa na Messi ambazo zinaonekana haziwezekani tena kuvunjwa na Ronaldo...

**5. Kushinda mara nne mfululizo Ballons d'Or**

Kati ya mwaka 2008 na 2017 Messi na Ronaldo wote kwa pamoja walishinda mara tano tuzo ya Ballon d'Or.

Ingawa wote wawili kwa sasa wanashikilia rekodi ya kushinda mara tano tuzo hiyo, lakini rekodi iliyowekwa na Messi, Ronaldo hawezi kuifikia.

Tuzo zake nne kati ya tano za Ballon d'Or ambazo Messi alizoshinda alizitwaa kati ya mwaka 2009 na 2012, na kuweka rekodi ya kushinda mara nne mfululizo kuliko mchezaji mwingine yeyote.

Ronaldo ameweza tu kushinda mara mbili mfululizo kati ya mwaka 2013-14 na 2016-17 na ilionekana kama angeshinda mara tatu mfululizo mwaka 2018, lakini Luka Modric akampiku na kuitwaa.

Huku umri wa wachezaji hao ukizidi kusonga, ni wazi kwamba hawatakuwa na uwezo wa kuendelea kuzibeba tuzo hizo na hivyo uwezekano wa Ronaldo kuifikia rekodi ya Messi ni mgumu.

**4. Kufunga mabao 91 kwenye kalenda ya mwaka**

Mwaka 2012, Messi alivunja rekodi ya Gerd Muller kwa kufunga mabao 91 kwenye kalenda ya mwaka.

Messi alivunja rekodi hiyo ambapo Gerd Muller alifunga mabao 85 kwa kalenda ya mwaka.

Rekodi hii imemfanya Messi kuwa kwenye kilele cha juu akiwa na Barcelona na kuwa mfungaji wa wakati wote wa timu hiyo.

Ingawa Cristiano Ronaldo ni mashine ya ufungaji mabao, hajaweza kufunga mabao mengi kwenye kalenda ya mwaka.

Ronaldo alishindwa kufunga mabao 50 kwa mara ya kwanza mwaka 2018, kwa kuwa alishindwa kukaribia kufikia rekodi ya Messi ya kufunga mabao 91.

Kwa hiyo, rekodi hii inaonyesha wazi kwamba haitaweza kuvunjwa na Ronaldo.

**3. Kufunga mabao 50 kwa msimu mmoja La Liga**

Wakati wa msimu wa Ligi Kuu ya Hispania msimu wa 2011/12, Lionel Messi aliweka rekodi mpya kwa kufunga mabao mengi kwa msimu mmoja katika Ligi Kuu ya Hispania.

Alivunja rekodi iliyowekwa na Ronaldo ya kufunga mabao 40 msimu uliopita.

Ronaldo aliikaribia rekodi hiyo wakati akiichezea Real Madrid wakati alipofunga mabao 48 msimu wa 2014/15, lakini bado alishindwa kufikia rekodi ya Messi aliyoiweka msimu wa 2011/12 kwa zaidi ya mabao mawili.

Kwa sasa Ronaldo anacheza kwenye Ligi Kuu ya Italia, ni wazi kwamba rekodi ya Messi ni ngumu kuifikia ya kufunga mabao 50 kwa msimu.

Hii ni moja ya rekodi bora ya Messi ambayo ni vigumu kwa Ronaldo kuivunja tena.

**2. Pasi za mwisho 150 La Liga**

Wakati wa msimu wa 2018/19, Messi alikuwa mchezaji wa kwanza kwenye historia ya La Liga kutoa pasi za mwisho 150 kwenye La Liga.

Hadi sasa Messi anabakia kuwa ndiye mchezaji pekee duniani ambaye ametoa pasi za mwisho nyingi zaidi kwa wachezaji wenzake.

Hii ilikuwa ni mara ya kwanza kwa msimu huo wa 2018/19 wakati mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina akiweka rekodi hiyo kwenye La Liga, ambapo kwa mara ya kwanza iliwekwa mwaka 1990.

Na hilo linafanya kwamba, safu ya mshambuliaji anayocheza Messi ni bora zaidi kuliko Ronaldo, akiwazidi Ronaldinho, Thierry Henry, Luis Suarez, Samuel Eto'o, na Neymar.

Hata hivyo, rekodi ya Messi ya kutoa pasi za mwisho 150 kwenye La Liga kamwe haitaweza kuvunjwa na Ronaldo.

**1. Mabao 400 katika klabu moja**

Tangu alipoanza kucheza kwa mara ya kwanza kwenye La Liga mwaka 2004, Messi amekuwa ndiye mfungaji bora wa wakati wote wa klabu hiyo kwenye mashindano yote katika historia.

Amefunga mabao 405 kwenye Ligi Kuu ya Hispania, huku akifuatiwa na Ronaldo aliyefunga mabao 311.

**USILOLIJUA**

MSHAMBULIAJI wa Tottenham, Harry Kane, hadi sasa amefunga mabao tisa katika 'Dabi ya London' dhidi ya Arsenal, hivyo kuipiku rekodi ya mabao nane aliyokuwa amefunga Emmanuel Adebayor wakati akiichezea 'Gunners'.



## Wajasiriamali wahimizwa kumiliki vitambulisho vya wamachinga

**Na Nebart Mokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amewapa wiki mbili wachimbaji zaidi ya 100 wa mchanga walio katika eneo la machimbo la Iduda jijini Mbeya, kumiliki vitambulisho vya wajasiriamali vilivyotolewa na Rais John Magufuli ili kuepuka usumbufu.

Alitoa agizo hilo juzi alipotembelea machimbo hayo na kusema baada ya muda huo kuisha, serikali itatoa utaratibu maalumu wa kutosumbuliwa wachimbaji hao ambao watakuwa tayari wana vitambulisho.

Alisema kiutaratibu wachimbaji hao hawatakuwa wanatozwa chochote baada ya kuwa na vitambulisho hivyo isipokuwa wenye magari wanaonunua mchanga huo ndio watakaokuwa wanalipa ushuru.

Alisema wachimbaji watakaokuwa hawajanunua vitambulisho hivyo watakuwa wanatozwa Shilingi 3,000 kama kodi kwa kila lori la mchanga gharama ambayo ni sawa na anazotozwa mwenye lori anapopitisha getini.

"Kila mtu achague kununua kitambulisho hiki kwa shilingi 20,000 kwa mwaka mzima ama kutozwa shilingi 3,000 kwa kila lori analouza mchanga, lakini sisi tunajiandaa baada ya muda huo niliowapa kuisha tutatoa utaratibu mpya wa kutowasumbua," alisema Chalamila.

Alisisitiza kuwa endapo mtu atachagua kutonunua kitambulisho hicho kuna uwezekano kwa siku akawa analipa shilingi 30,000 kama atakuwa na uwezo wakuuza malori 10.

Wachimbaji hao waliomba watumie utaratibu wa kununua vitambulisho hivyo badala ya kutozwa kila lori kwa madai kuwa mfumo huo ni gharama nafuu zaidi na utawasaidia kuepuka kufukuzana na watoza ushuru wa Jiji.

Mmoja wa wachimbaji hao, Michael Samson, alisema watahamasishana kununua vitambulisho hivyo ili waepuke usumbufu kwa madai kuwa elimu iliyotolewa na Mkuu wa Mkoa inaonyesha wataepuka usumbufu mkubwa.

Alisema endapo wachimbaji hao wakatozwa gharama sawa na mchimbaji, hawawezi kupata kitu kutokana na kwamba watakuwa wanalipa mara mbili.

"Sisi hapa tunapochimba tunamlipa mwenye eneo, sasa tukitaka tuwe tunalipa na hiyo 3,000 basi itakula kwetu maana hakuna tutakachokuwa tunapata kutokana na kazi yetu, tutakuwa tunawafaidisha wenye magari," alisema Samson.

# Watano watumbuliwa kwa madai ya ufisadi

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

WATUMISHI watano wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, wametumbuliwa kwa tuhuma za kuisababishia halmashauri hasara ya Shilingi milioni 97 za makusanyo ya ushuru kutoka vyanzo mbalimbali.

Uamuzi wa kuwatimua watumishi hao ulifikiwa mwishoni mwa wiki, wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani ambacho madiwani walijadili mambo mbalimbali kuhusu nidhamu ya watumishi.

Watumishi waliotimuliwa kazi ni Josia Katende, Elias Lusese na Thobias Matthew ambao wote ni watendaji wa vijiji mwingine ni Undule Mwasyobe ambaye ni Ofisa Mtendaji wa Kata na Edmund Mwalukana aliyekuwa mhasibu wa halmashauri hiyo.

Akizungumza wakati wa Kikao cha Baraza, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Ezekiel Mwakota, alisema watumishi hao walisababisha hasara hiyo kuanzia Julai 2016 hadi 2018 kabla ya kushtukiwa.

Alisema baada ya kuhojiwa walikiri na wakaahidi kurejesha fedha hizo, lakini mpaka sasa hawajarejesha kiasi chochote na hivyo baraza likaamua kuwatimua kazi.

"Watumishi hawa walikiri na wakaahidi kuzirejesha fedha hizo na wakakubaliwa, lakini wamekiuka makubaliano hayo, hivyo baraza limekubaliana kwa kauli moja kwamba wafukuzwe kazi na hayo ndio maagizo kwa mamlaka zinazohusika," alisema Mwakota.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Loema Peter, alisema mchakato wa kuwatimua watumishi hao umepitia vikao mbalimbali vya kinidhamu kabla ya kuamuliwa na Baraza la Madiwani.

Alisema awali kulikuwa na ufujaji wa zaidi ya shilingi milioni 200, ambazo zilikuwa zimeliwa na watumishi 15, lakini baada ya uchunguzi kufanywa na tume iliyokuwa imeundwa ilibainika ni watumishi watano.

"Watumishi wengine wamesamehewa kutokana na utetezi walioutoa ikiwa ni pamoja na kurejesha fedha hizo kama walivyokuwa wameagizwa na baraza, sasa hawa watano ndiyo waliokaidi kurejesha fedha," alisema Peter.

Katika hatua nyingine baraza hilo lilimwagiza Mganga Mkuu wa Wilaya, Dk. Jordan Mlina, kuwachukulia hatua za kinidhamu baadhi ya watumishi wa Hospitali ya Wilaya ya Makandana kutokana na kuzorota kwa huduma.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Mwakota alisema walitakiwa wamwajibishe Mganga Mkuu huyo, lakini wakamwacha kutokana na kuwa mgeni.

Alisema kutokana na hali hiyo kiongozi huyo anatakiwa akafanye mabadiliko kwenye hospitali hiyo ili kurejesha nidhamu kwenye hospitali hiyo kwa madai kuwa kwa sasa watumishi wanatoa lugha chafu kwa wagonjwa.

Akizungumzia hali hiyo, Mganga Mkuu wa wa Wilaya hiyo, Mlina alisema ameshabaini tatizo hilo na ameshaanza kuchukua hatua kwa baadhi ya watumishi.

Alisema baadhi ya watumishi wameshushwa vyeo, wengine wameandikiwa barua za onyo.



Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya (Must), Pius Msekwa (katikati), akimkabidhi aliyekuwa Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Joseph Msambichaka, cheti cha kutambua mchango wake. Kulia ni Mwenyekiti wa Baraza la Chuo hicho, Zakia Meghji. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Chuo kikuu kuongeza matumizi ya sayansi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya (Mist), Pius Msekwa, amesema matarajio ya serikali ni kukifanya chuo hicho kuwa chachu ya ongezeko la matumizi ya sayansi na teknolojia, ili kukuza uchumi na maendeleo ya nchi.

Alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa hafla maalumu ya kumuaga aliyekuwa Makamu Mkuu wa chuo hicho, Prof. Joseph Msambichaka na kumsimika Prof. Aloys Mvuma, kushika wadhifa huo.

Msekwa ambaye ni Spika mstaafu alisema chuo hicho kinatakiwa kuwa mstari wa mbele katika kulifikisha taifa kwenye uchumi wa kati unaotegemea maendeleo ya viwanda ambayo yanahitaji utaalamu wa kisayansi na teknolojia.

"Tukidhamiria kwa dhati tutaweza kufikia malengo ya serikali na tunatakiwa tuwe na imani kama mwasisi wa taifa hili Mwalimu Julius Nyerere ambaye wakati wa vita ya Kagera alisema 'nia tunayo, uwezo tunao na nguvu tunazo' na kweli Tanzania ilishinda vita ile," alisema Msekwa.

Alimpongeza Profesa Msambichaka kwa utumishi uliotukuka ambao umeking'arisha chuo hicho kuanzia ilipokuwa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya (Mist) mpaka ikapandishwa hadhi na kuwa Chuo Kikuu mwaka 2012.

Alisema wakati wa uongozi wake Prof. Msambichaka amelisaidia taifa kwa kuzalisha wasomi wengi ambao wanaendelea kutumikia taifa kwenye maeneo mbalimbali ya utendaji.

Alisema zimeanzishwa kozi mbalimbali ambazo zinaendana na wakati ikiwamo kozi ya uhandisi vifaa tiba ambayo imeanza hivi karibuni na itaisaidia serikali kupunguza gharama za uagizaji wataalamu nje ya nchi.

"Tunatambua mchango mkubwa aliotoa Profesa Msambichaka katika maendeleo ya chuo hiki, tunaomba tutakapohitaji msaada wako wakati wowote, usisite kutusaidia," alisema Msekwa.

Alimpongeza pia Prof. Mvuma kwa kuaminiwa na kuteuliwa ili awe Makamu Mkuu wa Chuo hicho na hivyo akamshauri kufanya kazi kwa bidii na kuleta mabadiliko.


Mwenyekiti wa Baraza la Chuo hicho, Zakia Meghji, kwa upande wake alimsifu Prof. Msambichaka kuwa alikuwa kiongozi mwenye maono makubwa ya kukiboresha nchuo hicho na kutekeleza maono hayo kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

Alisema kiongozi huyo alikuwa karibu na watumishi wenzake na kwamba hata baada ya kuteuliwa na Rais Dk. Magufuli kuwa mwenyekiti, Prof. Msambichaka alimpigia simu na kumpongeza kwa kuteuliwa na akamkaribisha katika chuo hicho.

Akizungumza wakati wa kuaga Prof. Msambichaka aliwashukuru watumishi wa chuo hicho, pamoja na serikali kwa kumpatia ushirikiano wakati wa uongozi wake na akawataka waendelee kumpatia mrithi wake Prof. Mvuma ili naye atekeleze maono yake.

Aliwapongeza pia Mkuu wa Chuo hicho Msekwa pamoja na Mwenyekiti wa Baraza, Zakia Meghji kwa kuendelea kukiongoza chuo hicho kwa hekima na busara hali inayokifanya kiwe imara.

Kwa upande wake Makamu Mkuu wa Chuo Prof. Aloys Mvuma, aliahidi kuzingatia kanuni na taratibu za uongozi katika kukiongoza chuo hicho ili kukifanya kuwa bora.





## Vifungashio vya 'Tshishimbi' vyapigwa marufuku

**Na Elisante John,**
SINGIDA

BAADA ya serikali kupiga marufuku ujazo wa lumbesa, baadhi ya wafanyabiashara wa vitunguu mkoani Singida, wamebuni mbinu mpya ya vifungashio vya magunia ya neti, maarufu kwa jina la 'Tshishimbi' ili kuwanyonya wakulima.

Kufuatia hali hiyo, Serikali ya Wilaya ya Singida imepiga marufuku vifungashio hivyo ambavyo vinaujazo wa zaidi ya kilo 100.

Marufuku hiyo ilitolewa jana na Mkuu wa wilaya hiyo, Paskas Mragili, alipofanya ziara ya kushtukiza kwenye soko la kimataifa la Misuna lililopo Manispaa ya Singida, baada ya kupokea malalamiko ya wakulima na wafanyabiashara, ambao wanajishughulisha na zao la vitunguu.

Katika ziara yake, Mragili aliambatana na wataalamu wa vipimo na kuagiza magunia matatu tofauti yapimwe na kubainika kuwa gunia lenye vifungashio vya Tshishimbi kuwa na kilo 124.6, gunia la pamba kilo 84.4 na kifungashio cha neti halali kilo 74.

Baada ya hali hiyo, mkuu huyo aliagiza kuanzia sasa kuacha kutumika gunia lolote la aina ya neti kwa kuwa yanawapunja wakulima na kuagiza magunia ya pamba pekee ndio yatumike.

"Nimeruhusu magunia hayo, baada ya kujiridhisha pia kujenga imani kwa mkulima wa kawaida anayeamini kipimo hicho, lakini nasisitiza lazima kila gunia la vitunguu lipimwe kwenye mizani wakati wa mauziano ya biashara hiyo," alisema.

Aliongeza: "Ili kuhakikisha zoezi hili linafanikiwa nitawasiliana na mamlaka husika kupiga marufuku kipimo cha neti nchi nzima, lengo ni kumsaidia mkulima aondokane na adha ya kunyonywa jasho lake."

Kwa upande wake, mkulima Isihaka Majaliwa, alishukuru hatua ya serikali na kudai kuwa uamuzi huo utasaidia kumaliza utata na hivyo kumnufaisha mkulima wa kawaida wa kijijini.

# Wanaobadili matumizi fedha za miradi waonywa

**Na Ibrahim Joseph,**
DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imewaonya watendaji wa mamlaka za serikali za mitaa kuacha tabia ya kubadili matumizi kwenye fedha za miradi kwa kuwa ni kinyume na miongozo waliyopewa. Onyo hilo lilitolewa jana na Naibu Katibu Mkuu wa ofisi hiyo, Tixon Nzunda, alipokuwa akifungua mkutano wa siku mbili wa wadau wa elimu Tanzania wanaotekeleza mradi wa Equip Tanzania uliofanyika jijini hapa.

Alisema serikali haitawaonea aibu watumishi waliopewa jukumu la kusimamia fedha za miradi na kuzihamisha kwa matumizi mengine.

"Kwa wale watakaotumia vibaya au kubadilisha matumizi ya fedha za miradi mbalimbali zilizotolewa hatua kali za kinidhamu na sheria zitachukuliwa kwa wahusika bila kumwonea aibu," alisema. Alisema serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli imekuwa ikisisitiza kuwa kila rasilimali fedha inayotolewa inaenda kuimarisha eneo husika, hivyo fedha zitumike kwa malengo yaliyokusudiwa.

"Kwa mfano wa hivi karibuni kuna watumishi wawili mmoja kutoka Wilaya ya Butiama mkoani Mara na mwingine kutoka Mkoa wa Iringa walihamisha matumizi ya fedha na serikali imewasimamisha mpaka wahakikishe wanazirudisha fedha hizo kabla ya Machi 30, mwaka huu," alisema.

Aidha, alisema mradi wa Equip Tanzania umesaidia kiwango cha ufaulu wa wanafunzi kuongezeka.

Alisema mradi huo umemalizia ujenzi wa vyumba vya madarasa 251 yanayotokana na nguvu ya wananchi katika mikoa tisa.

Aliongeza kuwa mradi huo umewezesha mafunzo kwa walimu 61,000 kwa kufundishwa njia bora za ufundishaji katika madarasa yenye idadi kubwa ya wanafunzi. "Katika kuimarisha mahudhurio ya wanafunzi na kupenda shule mradi huu umetoa hamasa kwa watoto yatima na wanaoishi kwenye mazingira magumu kuandikishwa shule," alisema.

Nzunda alisema mradi huo umewezesha kuandaa takwimu na kuweka mfumo wa ufuatiliaji kwa mikoa 13 kuanzia ngazi ya kata hadi kufikia mkoa.

Kwa upande wake, Mkuu wa kitengo cha Huduma za Jamii Shirika la Uingereza linalofadhili mradi huo (DFID), Getridi Mapunda, alisema shirika hilo lilitoa Sh. bilioni 180 kwa ajili ya kufadhili mradi kwa miaka sita.

Mapunda alisema mradi wenye lengo la kusaidia kuinua elimu nchini ulianza mwaka 2016 na unatarajiwa kufikia mwisho mwaka 2020. Alisema lengo la kukutana na watekelezaji wa mradi pamoja na wafadhili ni kujadili mafanikio na changamoto zinazojitokeza kwenye utekelezaji wa mradi huo.

Hata hivyo, alisema wafadhili wamefurahishwa kutokana na serikali kuwawajibisha watumishi waliohamisha fedha za mradi kwa matumizi mengine. "Sio kwamba fedha zimeibiwa, hapana, ila isipokuwa zilihamishwa na kutumika kwa shughuli zingine nje ya malengo ya mradi wa Equip Tanzania," alisema.



Baadhi ya watumishi wa jiji na wafanyabiashara wa Soko Kuu la Majengo Dodoma, wakifanya usafi kwenye eneo la korongo lililopo katikati ya sokoni hapo. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mavunde ataka maombi awe na nidhamu ya uongozi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, ameendelea kutekeleza ahadi zake mbalimbali alizozitoa wakati wa kampeni, huku akiwaomba wananchi kuendelea kumwombea awe na nidhamu ya uongozi.

Mavunde ambaye pia ni Naibu Waziri wa Vijana, Kazi na Ajira, aliitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki wakati akizindua mradi wa maji na kukabidhi mashine ya kuchuja maji katika Shule ya Sekondari Mpunguzi jijini hapa.

Alisema anataka awe mtumishi wa watu ambaye ataziishi kero na shida zinazowakabili hivyo wamwombee.

"Wananchi wangu mniombee ili Mungu anijalie hekima, busara na nidhamu ya uongozi niwe mtumishi wa watu ambaye nitaziishi kero na shida zinazowakabili," alisema.

Mavunde alisema yeye hawezi kuwasimamisha watu na kuwapa ahadi za uongo kwa kuwa anataka kuchaguliwa.

Alifafanua kuwa yeye si kama wanasiasa wengine ambao wana tabia ya kuahidi vitu kwa wananchi, lakini hawatimizi na kwamba kwa umri alionao hawezi kuwaongopea wananchi wa jimbo lake.


"Mimi kwangu nilisema uongozi mlionipa ni utumishi wa kuwatumikia watu na moja kati ya sehemu ya kuwatumikia watu, eneo la Mpunguzi ilikuwa ni hatari sana wanafunzi walikuwa wanaenda kuchota maji korongoni wakati mwingine chakula kinachelewa ndio maana nikasema jambo hili nijitahidi kulitatua ndani ya wakati," alisema.

Alisema pia maji waliyokuwa wakichota wakati mwingine yalisababisha homa za matumbo.

Naye, Mkuu Shule ya Mpunguzi, Mshamu Hai, alisema kuwa shule hiyo ina wanafunzi 808, wa kike ni 353, huku wa kiume ni 458.

Alisema awali shule hiyo ilikuwa na changamoto ya maji kutokana na kisima kilichochimbwa kusombwa na mafuriko na kwamba anamshukuru mbunge amerudisha hali ya upatikanaji wa majisafi na salama.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi wa shule hiyo, Nivad Mtewele, aliziomba taasisi mbalimbali kuleta fursa kwenye shule hiyo ili kutatua changamoto ya uhaba wa madarasa na maabara.





Sheha wa Shehia ya Tumbatu Uvivini, Hassan Mwadini, akiwa katika wodi ya wzazi ambayo haijaanza kufanya kazi kutokana na kukosa wataalamu wa afya tangu ilipofunguliwa mwaka jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Huduma za uzazi zakwama kisiwa cha Tumbatu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KUKOSEKANA kwa wataalamu wa afya, huduma ya majisafi na salama na nishati ya umeme kumekwamisha huduma za afya ya uzazi katika kituo cha afya kisiwa cha Tumbatu Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Akizungumza na waandishi wa habari, msaidizi wa kituo hicho, Mcha Haji Makame, alisema vifaa vyote muhimu kwa ajili ya afya ya uzazi kituoni hapo vipo, lakini wakunga na wauguzi hakuna katika wodi ya kinamama kituoni hapo.

Alieleza kuwa tangu kufunguliwa kwa wodi ya wazazi kwa kinamama kituoni hapo mwanzoni mwa mwaka jana, bado haijaanza kutoa huduma za uzazi kutokana na changamoto hizo.

Alisema kutokana na kuwapo kwa upungufu huo kituoni hapo, bado wajawazito wa kisiwa cha Tumbatu wanaendelea kujifungua kwa wakunga wa jadi. Aidha, alisema licha ya serikali kusisitiza umuhimu wa wajawazito kujifungulia hospitali, wananchi wa kisiwa cha Tumatu wanajifungua kwa wakunga wa jadi kutokana na jiografia ya kisiwa hicho kuzungukwa na bahari na kutokuwapo kwa huduma hiyo.

"Kumtoa mjamzito wa kisiwa hiki aende kujifungulia hospitali inabidi avuke bahari, ili anende Hospitali ya Kivunge au Mnazimmoja na usafiri wenyewe ni shida, hivyo hulazimika kujifungua kwa wakunga wa jadi," alisema. Aidha, aliomba serikali kuhakikisha inaongeza wahudumu wa afya kituoni hapo na kurekebisha kasoro zilizopo ili wodi hiyo ya kinamama iweze kutoa huduma ya afya ya uzazi.

Alisema kuharakisha kufanya hivyo kutasaidia vifaa vilivyokuwamo katika wodi hiyo kutoharibika kwa sababu kwa sasa havitumiki.

Aliiomba serikali kuweka usafiri wa boti ya uhakika kisiwani hapo ili waweze kuwahi mapema kufika kazini na kutoa huduma kwa wakati na inapotokea mgonjwa wa dharura awahishwe hospitali nyingine.

Alieleza kuwa zipo baadhi ya kesi za wajawazito kupoteza maisha kutokana na kutowahishwa hospitali wanapopatwa na tatizo.

Naye Sheha wa Shehia ya Tumbatu Uvivini, Hassan Mwadini, alisema kuwa anasikitika kuona kuwa serikali imegharamika kujenga wodi ya kinamama katika kituo cha afya Tumbatu, lakini haitumiki.

# Naibu Waziri asisitiza viwanda kuwa endelevu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Biashara na Viwanda, Hassan Khamis Hafidh, amesema sekta ya viwanda vidogo na vya kati inahitaji usaidizi na usimamizi wa karibu kwa lengo la kuvilea na kuvifanya viwe endelevu.

Aliyasema hayo wakati akifungua kongamano na mafunzo ya ubora, usalama na udhibiti wa bidhaa za viwanda vidogo na vya kati, katika ukumbi wa sanaa Rahaleo mjini Zanzibar.

Alisema, serikali ya awamu ya saba imelenga kukuza na kuwekeza katika viwanda hivyo na kuwajali wajasiriamali wadogo ili kuwaenzi, lakini kuwapa fursa za kiuchumi.

"Serikali ya awamu ya saba imepanga kuviinua viwanda ili iweze kukuza uchumi, wajasiriamali na wazalishaji wa bidhaa lazima tuunge mkono jitihada kwa maendeleo yetu," alisema.

Alisema ili kupata maendeleo endelevu, uwekezaji kwenye viwanda umekuwa ukitumiwa na nchi nyingi duniani na Zanzibar na Bara zimeamua kujipanga upya kiuchumi kufikia huko.

Aidha, aliwataka wazalishaji na wajasiriamali kuzitambua fursa zilizopo, ikiwamo upatikanaji wa mikopo yenye masharti nafuu na huduma nyingine za kifedha na zisizo za kifedha kwa ajili ya kuendeleza sekta hiyo.

Alisema, serikali imekuwa ikichukua jitihada za makusudi kuhakikisha viwanda vidogo na vya kati vinakua na kuimarika na vingine vinaanzishwa katika kufikia kaulimbiu ya serikali zote mbili ya 'Tanzania ya Viwanda' ili wananchi waongeze kipato na kuliinua taifa kwa ujumla.

Naye Ofisa kutoka Wakala wa Viwanda Vidogo (SMIDA), Zeyana Hamad Kassim, alisema, wajasiriamali wenye viwanda vidogo wanakabiliwa na changamoto nyingi zinazowakwamisha na kuwafanya kukata tamaa ya kuendesha shughuli zao.

Alizitaja baadhi ya changamoto hizo kuwa ni pamoja na ughali wa malighafi, upatikanaji wa masoko, ukosefu wa vifungashio na usalama wa bidhaa wanazozizalisha.

Hata hivyo, alisema mbali na changamoto nyingi, sekta hiyo imekuwa na mchango mkubwa kwenye ukuaji wa uchumi na kutoa ajira katika kufikia malengo ya serikali hasa kwa vijana.

Ofisa Uhusiano wa SMIDA, Omar Salim Mbarouk, alisema dhamira ya kongamano hilo ni kutoa uelewa kwa wajasiriamali na wazalishaji wa bidhaa juu ya ubora wanazozilisha ili waweze kufikia malengo.

"Bado uelewa kwa wajasiriamali unahitajika katika kuwainua na kuwatengenezea mazingira mazuri yatakayoendana na mihitaji ya soko," alisema.

# Mkoa wa Magharibi kudhibiti mmomonyoko wa maadili

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, amesema kuwa ofisi yake itaendelea kufanya operesheni za mara kwa mara kudhibiti vitendo vinavyoashiria mmomonyoko wa maadili kama njia ya kudhibiti kasi ya maambukizi mapya ya virusi vya Ukimwi.

Akifungua kikao cha pamoja cha kamati za kupambana na Ukimwi za Wilaya na Makamshna wa Tume ya Ukimwi Zanzibar (ZAC), alisema ili kupunguza maambukizi hayo lazima kuanza kuviangalia viashiria vinavyosababisha maradhi hayo.

Alisema kikawaida miji mikuu ulimwenguni inakuwa na shughuli nyingi zikiwamo zinazochochea mmomonyoko wa maadili na vitendo viovu, hivyo operesheni hizo zinalenga kupunguza madhara ya matendo hayo.

Alisema kuwa katika operesheni hizo, mkoa uligundua kuwapo kwa nyumba za kulala wageni na za watu binafsi zinazoendesha au kuhamasisha biashara ya ngono jambo ambalo ni kichocheo cha kusambaa kwa maradhi ya kuambukiza na vitendo vya udhalilishaji.

Aidha, alikemea tabia ya baadhi ya watendaji wa serikali na vyombo vya ulinzi na usalama kwa kushirikiana na watu wanaojihusisha na vitendo hivyo jambo linalopunguza ufanisi wa kazi.

Hata hivyo, alipongeza juhudi zinazochukuliwa na Tume ya Ukimwi Zanzibar kutoa elimu na usaidizi kwa watu wanaoishi na virusi vya ugonjwa huo na kusababisha kudhibitiwa kwa kasi ya maambukizi ya ugonjwa huo.

Aliwashauri wajumbe wa tume hiyo wanaotokana na taasisi za dini kuanzisha utaratibu wa kukutana na viongozi wenzao na kupanga mikakati ya kueneza elimu ya kupambana na maradhi hayo ili kujenga uelewa wa pamoja kwa jamii.

Akitoa muhtasari wa mambo yaliyofanywa na mkoa huo katika mwaka uliopita, Katibu Tawala wa mkoa huo, Hamida Khamis Mussa, alisema pamoja na kutoa elimu kwa watendaji na viongozi wa mkoa, bado kunahitajika mkakati mahsusi wa kudhibiti kasi ya maambukizi ya maradhi hayo.

Alisema ofisi yake imeanzisha utaratibu wa kufuatilia mienendo ya watendaji wake ili kulinda maadili yao wakiwa ndani na nje ya ofisi, jambo ambalo litasaidia kuwadhibiti watendaji wenye tabia mbaya na zisizoendana na maadili ya jamii na utumishi wa umma.

Naye Kamishna wa Tume ya Ukimwi, Nuhu Salanya, alisema tume imekuwa na utaratibu wa kukutana na taasisi mbalimbali ili kuweka mikakati ya pamoja, hivyo watendaji wa ofisi hiyo wanapaswa kujipanga kimkakati kutimiza wajibu na malengo yaliyowekwa.

# RATIBA

## CAPITAL TELEVISION

**Mon 04 March**
- 06:00 Al jazera
- 08:00 CNN International News
- 09:00 Al Jazeera
- 10:00 Kumekucha
- 10:30 Kumekucha Michezo
- 11:30 Kumekucha Kishindo
- 12:00 Turning the spotlight rpt:
- 12:30 Drive it rpt
- 13:00 Series rpt : Grapes of justice
- 13:45 Series rpt: Ode To Joy
- 14:30 Usafiri wako rpt
- 15:00 Cookery rpt: Culinary Delight
- 15:30 Toyota world of wildlife rpt
- 16:00 CNN International
- 17:00 Eco@Africa rpt
- 17:30 Meza huru
- 19:00 Sauti za busara
- 19:30 Business edition
- 20:00 Series: Grapes of Justice
- 20:45 The Monday Agenda
- 21:30 Capital Prime News
- 22:00 Kipima Joto
- 00:00 Al Jazeera

**Tues 05 March**
- 06:00 Al Jazeera
- 08:00 CNN International News
- 09:00 Al Jazeera
- 10:00 Kumekucha
- 10:30 Kumekucha Michezo
- 11:30 Kumekucha Kishindo
- 12:00 The Decor rpt
- 12:30 Sauti za busara rpt
- 13:00 Series rpt: Grapes of justice
- 13:45 Series rpt: Ode To Joy
- 14:15 Local pgm rpt: Business Edition
- 15:00 Bundesliga kick off
- 15:30 Out and About rpt
- 16:00 Capchat rpt
- 17:00 Ripoti Maalum rpt
- 17:30 Meza huru
- 19:00 Innovation
- 19:30 Sauti za busara
- 20:00 Series: Grapes of Justice
- 20:45 Series: Brilliant legacy
- 21:30 Capital Prime
- 22:00 Turning the Spotlight rpt
- 22:30 Iron Chef rpt
- 23:30 Al Jazeera

**Wed 06 March**
- 06:00 Al jazeera
- 08:00 CNN International News
- 06:00 Al Jazeera
- 08:00 CNN International News
- 09:00 Al Jazeera
- 10:00 Kumekucha
- 10:30 Kumekucha Michezo
- 11:30 Kumekucha Kishindo
- 12:00 Turning the Spotlight rpt
- 12:30 Sauti za busara rpt
- 13:00 Series rpt: Grapes of Justice
- 13:45 Series rpt: Brilliant legacy
- 14:30 Local Pgm: The Monday Agenda Rpt
- 15:15 Capchat rpt
- 16:15 CNN International
- 17:00 Innovation rpt
- 17:30 Meza Huru
- 19:00 Sports Gazette
- 19:30 Sauti za busara
- 20:00 Series: Grapes of Justice
- 20:45 Series: Brilliant legacy
- 21:30 Capital Prime News
- 22:00 Dakika 45:
- 22:45 The Décor
- 23:15 Al Jazeera

**Thurs 07 March**
- 06:00 Al Jazeera
- 08:00 CNN International News
- 09:00 Al Jazeera
- 10:00 Kumekucha
- 10:30 Kumekucha Michezo
- 11:30 Kumekucha Kishindo
- 12:00 Sports Gazette
- 12:30 Sauti za busara rpt:
- 13:00 Series rpt: Grapes of Justice
- 13:45 Series rpt: Brilliant legacy
- 14:30 Business Edition rpt
- 15:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
- 16:00 Dakika 45 rpt
- 17:00 In good shape
- 17:30 Meza Huru
- 19:00 Turning the spotlight
- 19;30 Sauti za busara
- 20:00 Series: Grapes of Justice
- 20:45 Series: Brilliant legacy
- 21:30 Capital Prime News
- 22:00 Capchat rpt
- 23:00 Al Jazeera

**Frid 08 March**
- 06:00 Al Jazeera
- 08:00 CNN International News
- 09:00 Al Jazeera
- 10:00 Kumekucha
- 10:30 Kumekucha Michezo
- 11:30 Kumekucha Kishindo
- 12:00 Innovation rpt
- 12:30 Sauti za busara rpt
- 13:00 Series rpt: Grapes of Justice
- 13:45 Series rpt: Brilliant legacy
- 14:30 Ripoti Maalum rpt
- 15:00 Korean Dram rpt: Emperor of the sea
- 16:00 CNN International
- 16:30 The Monday Agenda rpt
- 17:30 Meza Huru
- 19:00 Drive it
- 19:30 Sauti za busara
- 20:00 Aibu yako
- 20:15 Local Pgm: Business Edition
- 20:45 Series: Brilliant legacy
- 21:30 Capital Prime News
- 22:00 Malumbano ya hoja rpt
- 00:00 Al Jazeera

**Sat 09 March**
- 08:00 CNN International
- 09:00 Drive It rpt
- 09:30 Turning the Spotlight rpt
- 10:00 Culinary delight rpt
- 10:30 Sauti za busara rpt
- 13:30 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
- 14:30 Telenovela rpt: Brilliant legacy
- 17:15 Ripoti Maaalum rpt
- 17:45 Bundesliga kick off
- 18:15 Capchat rpt
- 19:15 Mizengwe
- 19:30 The Decor
- 20:00 Iron Chef.
- 21:00 Out n' about
- 21:30 Movie: The four horsemen
- 23:00 Grapes of Justice rpt
- 01:00 Al Jazeera

**Sun 10 March**
- 08:00 CNN International
- 09:00 In good shape
- 10:00 Capchat rpt
- 11:00 Sports Gazette rpt
- 11:30 Iron chef rpt
- 12:00 Out n about rpt
- 12:30 Bundesligga Kick Off rpt
- 13:00 Ripoti Maalum
- 13:30 Series rpt: Grapes of Justice
- 15:15 Aibu yako
- 15:30 Drive it rpt
- 16:00 Dakika 45 rpt
- 16:45 Mizengwe rpt
- 17:00 The Decor rpt
- 17:30 Meza huru
- 19:00 Turning the Spotlight rpt
- 19:30 Cookery pgm:Culinary Delights
- 20:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
- 21:00 Shift
- 21:15 Capchat live
- 22:15 Telenovela: Brilliant legacy
- 00:00 Al Jazeera

## ITV Daima WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY 04 March**
- 05:30 Uwanja wa Mazoezi
- 06:00 Habari
- 06:40 Kumekucha
- 07:30 HABARI
- 08:00 Kumekucha Michezo
- 08:55 Habari za saa
- 09:00 Kumekucha Kishindo
- 09:30 Isidingo
- 09:55 Habari za saa
- 10:00 Watoto wetu
- 10:30 Igizo: Hatua
- 10:55 Habari za saa
- 11:00 Kimya Milele
- 11:55 Habari za saa
- 12:00 Al Jazeera
- 12:30 Jungu kuu rpt
- 12:55 Habari za saa
- 13:00 Mjue Zaidi
- 13:55 Habari za saa
- 14:00 Telenovela: Destiny (Destino)
- 14:55 Habari za saa
- 15:00 Meza Huru
- 16:30 Watoto Wetu
- 17:00 The Base
- 18:00 Jiji Letu
- 18:10 Aibu yako rpt
- 18:15 Huduma ya kwanza
- 18:30 Shamba shape up
- 19:00 Afya ya Jamii
- 19:30 Isidingo
- 20:00 Habari
- 21:05 Dakika 45
- 22:00 Telenovela: Destiny (Destino)
- 23:00 Habari
- 23:30 The Base
- 00:30 Al Jazeera
- 02:00 CNN International

**TUESDAY 05 March**
- 05:30 Uwanja wa Mazoezi
- 06:00 Habari
- 06:40 Kumekucha
- 07:30 HABARI
- 08:00 Kumekucha Michezo
- 08:55 Habari za saa
- 09:00 Kumekucha Kishindo
- 09:30 Isidingo
- 09:55 Habari za saa
- 10:00 Watoto wetu
- 10:30 Hawavumi lakini wamo
- 10:55 Habari za saa
- 11:00 Hawavumi lakini wamo
- 11:15 Igizo: Mtego
- 11:55 Habari za saa
- 12:00 Al Jazeera
- 12:30 Afya ya jamii rpt
- 12:55 Habari za saa
- 13:00 Uchumi na biashara
- 13:30 Kipindi Maalum rpt : TFDA
- 13:55 Habari za saa
- 14:00 Huduma ya kwanza
- 14:15 Telenovela: Destiny (Destino) rpt:
- 14:55 Habari za saa
- 15:00 Meza Huru
- 16:30 Watoto wetu
- 17:00 The Base
- 18:00 Jiji Letu
- 18:15 Korean drama rpt: The Great Queen Seonduk
- 19:00 Jarida la wanawake
- 19:30 Isidingo
- 20:00 Habari
- 21:00 Kipindi maalum:
- 22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
- 23:00 Habari
- 23:30 The Base
- 00:30 CNN International

**WEDNESDAY 06 March**
- 05:30 Uwanja wa Mazoezi
- 06:00 HABARI
- 06:40 Kumekucha
- 07:30 HABARI
- 08:00 Kumekucha Michezo
- 08:55 Habari za saa
- 09:00 Kumekucha Kishindo
- 09:30 Isidingo
- 09:55 Habari za saa
- 10:00 Watoto wetu
- 10:30 Shamba shape up
- 10:55 Habari za saa
- 11:00 Korean: The Great Queen Seonduk
- 11:55 Habari za saa
- 12:00 Al Jazeera
- 12:30 Jarida la wanawake rpt
- 12:55 Habari za saa
- 13:00 Dakika 45
- 13:55 Habari za saa
- 14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino):
- 14:55 Habari za saa
- 15:00 Meza Huru
- 16:30 Watoto Wetu
- 17:00 The Base
- 18:00 Jiji Letu
- 18:15 Mapishi rpt
- 18:30 Ijue Sheria
- 19:00 Kipindi Maalum: TFDA
- 19:30 Isidingo
- 20:00 Habari
- 21:00 Aibu Yako! Hata wewe?
- 21:10 Kipindi Maalum : Uongozi
- 21:40 Kipindi Maalum: Tanesco
- 22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
- 23:00 Habari
- 23:30 The Base
- 00:30 Al Jazeera
- 02:00 CNN International

**THURSDAY 07 March**
- 05:30 Uwanja wa Mazoezi
- 06:00 HABARI
- 06:40 Kumekucha
- 07:30 HABARI
- 08:00 Kumekucha Michezo
- 08:55 Habari za saa
- 09:00 Kumekucha Kishindo
- 09:30 Isidingo
- 09:55 Habari za saa
- 10:00 Watoto wetu
- 10:30 Igizo: Elininyo
- 10:55 Habari za saa
- 11:00 Igizo: Elininyo
- 11:15 Usafiri wako
- 11:55 Habari za saa
- 12:00 Al jazeera
- 12:30 Ijue Sheria
- 12:55 Habari za saa
- 13:00 Sanaa na wasanii rpt
- 13:30 Jungu Kuu
- 13:55 Habari za saa
- 14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
- 14:55 Habari za saa
- 15:00 Meza Huru
- 16:30 Watoto Wetu
- 17:00 The Base
- 18:00 Jiji Letu
- 18:15 Igizo: Riziki
- 19:00 Usafiri wako
- 19:30 Isidingo
- 20:00 Habari
- 21:00 Malumbano ya hoja
- 23:00 Habari
- 23:30 The Base
- 00:30 CNN International

**FRIDAY 08 March**
- 05:30 Uwanja wa Mazoezi
- 06:00 HABARI
- 06:40 Kumekucha
- 07:30 HABARI
- 08:00 Kumekucha Michezo
- 08:55 Habari za saa
- 09:00 Kumekucha Kishindo
- 09:30 Isidingo
- 09:55 Habari za saa
- 10:00 Watoto wetu
- 10:30 Hawavumi lakini wamo
- 10:55 Habari za saa
- 11:00 Hawavumi lakini wamo
- 11:20 Usafiri wako
- 11:55 Habari za saa
- 12:00 Al Jazeera
- 12:30 Kipindi Maalum rpt: TCRA
- 12:55 Habari za saa
- 13:00 Mjue Zaidi rpt
- 13:45 Kipindi Maalum rpt - Uongozi
- 13:55 Habari za saa
- 14:00 Kipindi Maalum rpt: Uongozi
- 14:15 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
- 14:55 Habari za saa
- 15:00 Meza huru
- 16:30 Watoto wetu
- 17:00 The Base
- 17:30 Ibada ya kiislamu
- 18:00 Jiji Letu
- 18:15 Igizo: Mizengwe
- 18:30 Uchumi na biashara
- 19:00 Kipindi maalum: TCRA
- 19:30 Isidingo
- 20:00 Habari
- 21:05 Kipima joto
- 23:00 Habari
- 23:30 The Base
- 00:30 CNN International

**SATURDAY 09 March**
- 05:30 Uwanja wa Mazoezi
- 06:00 HABARI
- 06:40 Kumekucha
- 07:00 Habari
- 08:00 Al Jazeera
- 09:00 Watoto wetu
- 10:00 Mjue Zaidi rpt
- 11:00 Jungu kuu rpt
- 11:30 Usafiri wako
- 12:00 Shamba Shape up
- 12:30 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
- 14:45 Igizo rpt: Riziki
- 15:15 Igizo rpt: Elininyo
- 15:45 Igizo rpt: Mizengwe
- 16:00 Igizo rpt: Kimya Milele
- 16:30 Igizo: Mtego rpt
- 17:00 Shamsham za Pwani
- 18:00 Jiji Letu
- 18:15 Mapishi
- 18:30 Igizo: Riziki
- 19:00 Sanaa na wasanii
- 19:30 Jungu Kuu
- 20:00 Habari
- 21:00 Igizo: Kimya Milele
- 21:30 Hawavumi lakini wamo
- 22:30 Isidingo rpt
- 01:00 CNN International

**SUNDAY 10 March**
- 05:30 Uwanja wa Mazoezi
- 06:00 HABARI
- 06:40 Kumekucha
- 07:00 Habari
- 08:00 Al jazeera
- 09:00 Watoto Wetu
- 10:00 Isidingo
- 11:45 Aibu Yako
- 11:50 Hawavumi lakini wamo rpt
- 12:50 Bongo Movie rpt: Kisasi cha utata 2
- 14:00 Tamasha la Michezo
- 15:00 Mwangaza
- 16:00 Korean drama: The great queen Seonduk
- 16:45 Mjue zaidi
- 17:30 Kipindi cha kikristo
- 18:00 Jiji Letu
- 18:15 Mapishi
- 18:30 Mizengwe rpt
- 18:45 Matukio ya wiki
- 19:30 Igizo: Mtego
- 20:00 Habari
- 21:05 Mizengwe
- 21:00 Bongo Movie: Hard Price
- 22:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)


5 EATV



UJENZI

LEO USIKU SAA 3:00



**JUMATATU**

11:00 DADAZ (live)
15:00 FUNGUKA
16:00 UTAKE
16:30 #HASHTAG
17:00 5SELEKT
17:55 KURASA
18:00 eNewz
18:30 Music
19:00 EATV SAA 1
19:30 MJADALA
21:00 UJENZI
21:30 5SPORTS LIVE
22:30 BONGO HITS

*Ujenzi Fahamu mambo mbalimbali kuhusu ujenzi, mapambo ya nyumba nje na ndani, mitindo na teknolojia tofauti zitumikazo kwenye ujenzi.*



eastafrica RADIO

05:00 EA Breakfast
09:00 Supamix
12:00 Kipenga Xtra
13:00 Planet Bongo
16:00 EA Drive
20:00 Kipenga
21:00 The Cruise

88.1FM DAR ES SALAAM


## RADIO One WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | RADIO ONE DOCTOR |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DAKIKA 45 |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 -03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | DK 45 ( MARUDIO ) |
| 23.00 HRS | |

**TUESDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA SHERIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 - 03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**WEDNESDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA MICHEZO |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**THURSDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA UKIMWI |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | MALUMBANO YA HOJA |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**FRIDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | HIZI NAZO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18:30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.0O HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05HRS | KIPIMA JOTO |
| 23.00 HRS | WEEKEND SHOW |
| 01:00 - 03:00HRS | HIZI NAZO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**SATURDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA KISWAHILI |
| 09.00 AM | WATOTO SHOW |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | MIWANI YA MAISHA |
| 11:00 AM | MTAA WA MAGOMA |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | CHAGUO LAKO |
| 15:00 HRS | MUZIKI NA MICHEZO |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.15 HRS | MIDUNDO MOTOMOTO |
| 18:00 HRS | BONGO TEN |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.15 HRS | CHEMSHA BONGO |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | WEEK END SHOW I |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | WEEK END SHOW II |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | WEEK END SHOW III |
| 01:00-03:00HRS | KISWAHILI ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | MUZIKI & MICHEZO ( MARUDIO ) |

**SUNDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA - FAMILIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | SUNDAY SPECIAL |
| 11: 00 HRS | TOP 20 |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13.30 HRS | NANI ZAIDI |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | MAMBO YA PWANI |
| 18:00 HRS | AFRICAN PANORAMA |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20:10 HRS | MBAVU ZANGU |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | MAMBO MSETO |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | RAFIKI I |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | RAFIKI II |
| 01:00 - 03:00 | FAMILIA ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00 HRS | RED CARPET ( MARUDIO ) |

## CAPITAL RADIO

### CAPITAL RADIO 2017 101.3 FM
### FAHARI YA MSIKILIZAJI/THE LISTENERS PRIDE

**MONDAY**
- 05:00-09:00HRS MORNING JAM
- 09:00-13:00HRS LETE RAHA
- 13:00-14:00HRS DW-RADIO
- 14:00-16:00HRS CLUB 101
- 16:00-18:00HRS DALA DALA
- 18:00-18:10HRS HABARI
- 18:10-20:00HRS BOZOUK TIME
- 20:00-21:00HRS HALI HALISI
- 21:00-22:00HRS SPORTS
- 22:00-01:00HRS LADHA LAINI

**TUESDAY - FRIDAY**
- 05:00-09:00HRS MORNING JAM
- 09:00-13:00HRS LETE RAHA
- 13:00-14:00HRS DW-RADIO
- 14:00-16:00HRS CLUB 101
- 16:00-18:00HRS DALA DALA
- 18:00-18:10HRS HABARI
- 18:10-21:00HRS BOZOUK TIME
- 21:00-21:30HRS SPORTS
- 21:30-01:00HRS LADHA LAINI
- 01:00-05:00HRS MUSIC & JINGLES

**SATURDAY**
- 05:00-07:30HRS MUZIKI
- 07:30-09:00HRS DK 90 DUNIANI
- 09:00-10:00HRS MUZIKI
- 10:00-12:00HRS KADOGOO
- 12:00-13:00HRS BONGO HITS 1
- 13:00-14:00HRS DW RADIO
- 14:00-15:00HRS BONGO HITS 2
- 15:00-16:00HRS ZAIDI YA UMJUAVYO
- 16:00-18:00HRS THE SPLASH
- 18:00-21:00HRS LAID BACK
- 21:00-21:30HRS SPORTS
- 21:30-01:00HRS AK 47 LIVE
- 01:00-05:00HRS MUSIC

**SUNDAY**
- 05:00-07:30HRS MUZIKI
- 07:30-09:00HRS GOSPEL MUSIC
- 09:00-11:00HRS THE SUNDAY
- 11:00-13:00HRS TOP TWENTY
- 13:00-14:00HRS DW RADIO
- 14:00-15:00HRS CAPITAL MICHEZONI
- 15:00-16:00HRS UKURASA WA MBELE
- 16:00-18:00HRS UNLIMITED REQUEST
- 18:00-21:00HRS JIACHIE
- 21:00-21:30HRS SPORTS
- 21:30-01:00HRS LADHA LAINI

HABARI KIMATAIFA

# Somalia yaapa kulimaliza kundi la Al Shabab

**MOGADISHU, Somalia**

SERIKALI ya Somalia imesema watu 20 wamefariki mwishoni mwa wiki mjini Mogadishu, baada ya kundi la kigaidi la Al Shabab kutekeleza shambulizi ndani ya mgahawa maarufu.

Idadi hiyo imetolewa na serikali ya Mogadishu ambayo imesema, itawasaka magaidi hao na kulipiza kisasi baada ya shambulizi hilo.

Maofisa wa usalama nchini humo kwa saa kadhaa, walipambana na magaidi hao waliokuwa wamewateka baadhi ya watu ndani ya mgahawa huo.

Waziri Mkuu, Hassan Ali Khaire, alisema kuwa, serikali yake haitachoka kupambana na Al Shabab, kwa gharama yoyote ile.

Mbali na kusababisha maafa na majeraha, mali kama magari ya watu yaliharibiwa katika shambulizi hilo.

Kundi la Al Shabab limeendelea kuisumbua serikali ya Somalia, kwa miaka zaidi ya 10 sasa, ikataka kuchukua uongozi wa nchi hiyo.

Juzi, milipuko na milio ya risasi ilisikika usiku kucha mjini Mogadishu, huku taarifa kutoka Jeshi la Polisi ikieleza kuwa hadi kufikia Ijumaa asubuhi, idadi ya watu waliokufa ilikaribia watu 30 na majeruhi 80 waliripotiwa kupelekwa katika hospitali mbalimbali. Idadi ya vifo ilitarajiwa kuongezeka kutokana na mapambano yaliyokuwa yakiendelea katika eneo la hoteli ya Al Mukarama iliyozungukwa na maduka, migahawa na hoteli nyingine.

Ofisa wa polisi, Meja Mohammed Hussein, alieleza kuwa vikosi vya polisi viliwaokoa raia wengine waliokuwa kwenye hoteli na majengo jirani.

Aliongeza kuwa wanamgambo wa Al Shabaab walikuwa wamenasa ndani ya hoteli, huku mapigano yakiendelea.

Ofisa huyo alisema ilikuwa vigumu kwa vikosi vya ulinzi kuingia kwenye jengo la hoteli walimokuwamo wanamgambo hao Alhamisi usiku kwa sababu ya giza baada ya umeme kukatika kutokana na mlipuko wa bomu.

Ofisa huyo alieleza matumaini ya kumalizika kwa operesheni hiyo ya kuwakamata wanamgambo hao na kuwaokoa raia.

*RFI*

# Tshisekedi kuwaachilia wafungwa wa kisiasa

**KINSHASA, Congo**

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Felix Tshisekedi, ameahidi kuwaachilia huru wafungwa wote wa kisiasa na kuwarudisha wote waliokimbia ng'ambo kutokana na sababu za kisiasa.

Akizungumza katika sherehe za kuzindua malengo yake ya kisiasa, usalama na uchumi siku 100 za kwanza za utawala wake kwenye uwanja wa Mabadilishano ya Mawazo, mtaa wa Limete, mjini Kinshasa, Rais Thisekedi alisema atahakikisha wizara ya sheria na mfumo wa mahakama zinaendeshwa na watu waaminifu na wenye maadili yasiyo na dosari.

"Mnamo siku kumi zijazo nitatoa msamaha wa Rais kuachiliwa huru wafungwa waliohukumiwa na mahakama. Na katika kuimarisha utaratibu wa kidemokrasia nchini mwangu, nimeamua kwamba lengo langu kuu mnamo siku 100 za kwanza kupunguza mvutano wa kisiasa," alisema Rais Tshisekedi.

Alisema atamwambia waziri wa sheria kuwaachilia huru wale wote waliokamatwa kwa sababu za kueleza maoni yao, hasa wakati wa mikutano ya kisiasa kabla ya uchaguzi wa Desemba 30.

Kuhusiana na utawala bora kiongozi huyo aliyechukua madaraka Januari 24, aliahidi kutayarisha kanuni za maadili ya vyombo vya serikali na kusimamia utekelezaji wake.

Tshisekedi alitoa pia ahadi ya kufanya marekebisho makubwa katika mazingira ya biashara kwa kutoa kanuni mpya za uchimbaji madini na kuhakikisha kuna mikataba ambayo pande zote husika zinanufaika kwa usawa.

Alisema anahitaji ushirikiano na Wakongo wote kwa kubadli maadili na mawazo yao kwa kuheshimu haki za binadamu, haki za kiraia, na uhuru wa kila aina kwa kila mtu.

*VOA*



Wanajeshi wa Marekani wakiwa katika mazoezi ya kivita. **PICHA: REUTERS**

# Bouteflika abadilisha meneja kampeni urais

**ALGIERS, Algeria**

RAIS wa Algeria, Abdelaziz Bouteflika, amembadilisha meneja wake wa kampeni kwa ajili ya uchaguzi mkuu utakaofanyika Aprili na anatarajiwa kuwania muhula wa tano madarakani.

Bouteflika amemteua Abdelghani Zaalane kuwa meneja wake mpya wa urais akishika nafasi ya Abdelmalek Sellal.

Uteuzi huo umekuja ikiwa ni siku moja baada ya maelfu ya Algeria kuandamana kumpinga Rais Bouteflika kuwania muhula wa mwingine wa urais. Kwa sasa Bouteflika (82) yuko nchini Uswis kwa uangalizi wa afya yake.

Shirika la habari la APS halikutoa sababu yoyote kuhusiana na uamuzi huo wa Bouteflika kumbadilisha Abdelmalek Sellal. Wapinzani nchini Algeria walisema Rais Bouteflika ambaye aliugua kiharusi mwaka 2013 na kuonekana mara chache hadharani hawezi tena kuliongoza taifa hilo la Afrika Kaskazini ambalo ni mzalishaji mkubwa wa mafuta.

Wapinzani hao wameeleza kuwa katika ishara ya udhaifu kuweza kutoa changamoto ya kupambana dhidi ya chama tawala cha National Liberation Front, na kumtaka Rais Bouteflika kujiondoa.

Mwishoni mwa wiki kulijitokeza kundi kubwa la wananchi lililoandamana kuipinga serikali ya Rais Bouteflika, lakini bado hajazungumzia moja kwa moja maandamano hayo.

Maofisa wa jeshi na wafanyabiashara matajiri bado wanamuunga mkono Rais Bouteflika.

Rais Bouteflika ni mpiganaji mkongwe wa vita vya kuwania uhuru nchini Algeria dhidi ya Ufaransa kuanzia mwaka 1954 hadi 1962 na amekuwa madarakani tangu mwaka 1999.

*DW*

# Marekani, Korea Kusini kusitisha mazoezi ya kivita

**WASHINGTON, Marekani**

MAREKANI na Korea Kusini zimetangaza kuwa zinasitisha kufanya mazoezi ya kijeshi ya pamoja ambayo hufanyika mara mbili kila mwaka.

Hatua hiyo ni juhudi za kufufua mazungumzo ya kidiplomasia yatakayowezesha Korea Kaskazini kuachana na mpango wake wa silaha za nyuklia.

Waziri wa Ulinzi wa Korea Kusini, Jeong Kyeong Doo na Kaimu Waziri wa Ulinzi wa Marekani, Patrick Shanahan, wamekubaliana kuwa nchi hizo mbili zitafanya mazoezi madogo ya kijeshi baadaye mwezi Machi.

Wizara ya Ulinzi ya Marekani imesema uamuzi huo unatoa ishara ya juhudi za pamoja kati ya Marekani na Korea Kusini za kupunguza wasiwasi uliopo na badala yake kuunga mkono juhudi za kidiplomasia zitakazowezesha kuondoa silaha za nyuklia kwenye rasi ya Korea.

Rais wa Marekani, Donald Trump, amewahi kukosoa mazoezi hayo ya kijeshi, akisema kuwa ni ghali na ni ya uchokozi kwa Korea Kaskazini.

Korea Kaskazini imekuwa ikiyazingatia mazoezi hayo ya kivita kama njama ya Marekani na Korea Kusini kuivamia nchi hiyo kijeshi.

*DW*

# Mashindano Mbio za Nyika Afrika kufanyika Moshi 2020

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

RAIS wa Shirikisho la Riadha Tanzania (RT), Anthony Mtaka, ametangaza rasmi kuwa mshindano ya Mbio za Nyika katika Bara la Afrika yatafanyika katika mji wa Moshi mwakani.

Mtaka ambaye pia ni Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, alitangaza jana mbele ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, kwamba mashindano hayo makubwa ya kimataifa yatafanyika Tanzania mwaka 2020.

"Napenda pia kuwatangazia Watanzania kwamba mashindano ya Mbio za Nyika Afrika mwaka 2020 yanafanyika Tanzania na tumeshakubaliana na serikali kwa maana ya wizara husika mashindano haya makubwa yafanyikie katika viwanja vya Gof mjini Moshi," alisema Mtaka.

Kwa mujibu wa Rais huyo wa RT, mashindano hayo yatazishirikisha nchi 54 za Afrika ambazo zitakuwa katika mji wa Moshi kimichezo na kwamba kutokana na ujio huo wa wanamichezo wa kimataifa ameiomba serikali kusaidia kukamilika kwa maandalizi hayo.

Alisema wageni wote hao watalala katika nyumba za wageni zilizoko katika mji wa kitalii wa Moshi na watakula katika hoteli zao.

Ujio wa mashindano hayo, utawalazimisha wanariadha kutoka mikoa yote ya Tanzania kuanza maandalizi ya kufukuza upepo kwa ajili ya kuwania nafasi ya kuwamo katika timu ya taifa itakayowakilisha nchi kwenye michuano hiyo mikubwa ya Afrika.

Kutokana na Tanzania kuwa mwenyeji wa mashindano hayo mwakani, Tanzania itanufaika katika sekta ya utalii kupitia mashindano hayo na kupata fedha kupitia watalii watakaokuja nchini kushiriki mashindano hayo.

Shirikisho la Kimataifa (IAAF) na Afrika (CAAA) limeichagua Tanzania, baada ya kuvutiwa na amani na utulivu.



Mafundi na baadhi ya wakazi wa kijiji cha Kakisheri Kata ya Nyakatende, Musoma Vijijini mkoani Mara, wakijenga msingi wa zahanati ya kijiji hicho ikiwa ni sehemu ya kutimiza mkakati wa serikali wa kujenga zahanati kila kijiji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mamlaka zahimizwa uhifadhi vyanzo vya maji

**Na Dege Masoli, TANGA**

MAMLAKA za maji nchini zimetakiwa kutumia sheria za uhifadhi wa mazingira katika kutunza vyanzo vya maji ili kutoruhusu uharibifu na uvamizi wa maeneo hayo muhimu unaofanywa na wananchi.

Agizo hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na Waziri wa Maji, Makame Mbarawa, mapema wiki hii alipotembelea chanzo cha maji cha Mto Sigi kilichoko Mabayani nje kidogo mwa Jiji la Tanga.

Mbarawa katika ziara ya siku nne mkoani hapo ya kutembelea miradi ya maji inayotekelezwa kwa fedha za serikali, alieleza kuwa suala la uvamizi wa vyanzo vya maji litamalizwa kwa kusimamia na kutumia sheria zilizopo.

"Uvamizi wa wakazi kwenye mabwawa ya maji ambayo ni vyanzo vya maji, ni suala la mamlaka kusimamia sheria pamoja na kuwekwa alama za umbali baina ya makazi na hifadhi, ili kuepusha uvamizi ikiwamo ulinzi wa mitambo ya kuzalishia maji," alisisitiza Mbarawa.

Awali Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (Tanga Uwasa), Mhandisi Geofrey Hully, sambamba na mambo mengine alitoa taarifa ya namna ya mamlaka hiyo ilivyotunza mazingira na kupunguza gharama za umeme katika kituo chake cha kusukuma maji cha Mowe.

Hully alieleza kuwa mbinu iliyotumika kulinda vyanzo hivyo ni kuunda kamati za mazingira na kuwawezesha wakazi wanaovizunguka kwa kuwapa shughuli mbadala za kufanya badala ya zile zinazokuwa kikwazo cha uhifadhi huo.

Kwa upande wa kupunguza gharama za umeme ni mamlaka hiyo kufunga kifaa maalumu kilichojulikana kwa jina la Variable Speed Driver ambacho kilisaidia kwa asilimia 20 ya gharama za awali.

**"Uvamizi wa wakazi kwenye mabwawa ya maji ambayo ni vyanzo vya maji, ni suala la mamlaka kusimamia sheria pamoja na kuwekwa alama za umbali baina ya makazi na hifadhi, ili kuepusha uvamizi ikiwamo ulinzi wa mitambo ya kuzalishia maji," alisisitiza Mbarawa.**

# DC atangazia vita wazazi, mafataki

**Na Steven William, MUHEZA**

MKUU wa Wilaya ya Muheza, Mwanasha Tumbo, amewatangazia vita wazazi watakaobainika kuwaozesha watoto wao wa kike walioko shuleni na kwamba wajue gereza linawahusu wao na wanaume waliowaoza.

Tumbo alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na waumini wa Kanisa la Katoliki Parokia ya Majengo Shimoni wakati wa ibada iliyoendeshwa na Padri Martin Kihiyo.

Alisema kuna wazazi wamekuwa wakiwakatisha masomo watoto wao wa kike kwa kuwaozesha kwa wanaume na kwamba anatoa onyo kwa mzazi atakayebainika kufanya hivyo, atakamatwa na kufikishwa mahakamani pamoja na yule mwanaume aliyeozeshwa mtoto huyo.

Tumbo alisema serikali ya awamu ya tano inasisitiza uadilifu na kumwogopa Mungu, kwa kuwa wakijua hilo basi hata hali ya usalama katika Wilaya ya Muheza itakuwa nzuri.

Alisema wazazi wanatakiwa wawajenge watoto wao katika hali ya uadilifu na kumwogopa Mungu, kwa kuwa wako baadhi ya watoto wana tabia mbaya katika familia zao.

Mkuu huyo wa wilaya alisema miaka iliyopita Wilaya ya Muheza ilikuwa inaongoza katika elimu, lakini hivi sasa imekufa kwa sababu wazazi hawashughuliki na watoto wao katika elimu.

Alisema watoto wa kike wanabakwa na kupewa mimba, huku akionya wanaume mafataki ambao watabainika kuwapa ujauzito wanafunzi kuwa watakiona cha moto na hataki utani.

Tumbo aliwataka wazazi kuwalinda watoto wao kwa kuwa ulinzi wa mtoto ni wajibu wa mzazi na kwamba wakiona watoto wanafanyiwa matendo mabaya basi watoe taarifa katika vyombo vya dola.

Katika hatua nyingine, alisema katika Wilaya ya Muheza walifanya sensa na kwamba waligundulika watoto yatima 700 wanaosoma, lakini hali zao mbaya na kwamba kuna mikakati mikubwa ya kuwasaidia kuwapatia vifaa mbalimbali vya elimu.

Pia alisema katika Wilaya ya Muheza wako watoto walemavu wa viungo na akili 244 na wanajengewa mabweni katika shule za msingi Mbaramo na Masuguru ili kuwawezesha kukaa hapo hapo shuleni kwa kuwa wengine wanashindwa kusoma kutokana na kukaa mbali kwa sababu ya ulemavu walio nao.

Aliwataka wazazi na wananchi kwa ujumla katika Wilaya ya Muheza kujitokeza kusaidia ujenzi wa mabweni hayo pamoja na madarasa katika shule za msingi na sekondari wilayani humo. Oooo

MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MASHAMBA/VIWANJA**

**LEYLAND DAF ZINAUZWA**, DAF TANKI YA MAJI LITA 10,000, DIESEL CC 5880. DAF PICK UP DIESEL CC 4200 TANI 4.5. MAGARI YAPO KWENYE HALI NZURI ZOTE ZINATEMBEA. MAWASILIANO: 0657 370655 DAR ES SALAAM.

**NAFASI ZA KAZI**

**TUNAAJIRI WASICHANA WA MAUZO (SALES).** SIFA KIDATO CHA NNE. UMRI KUANZIA MIAKA 25 - 38 AWE MTANZANIA. MASLAHI MAZURI. PIGA SIMU NAMBA 0714 634046.

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311

**CHETI KIMEPOTEA**



**HILDA ANTIPAS** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0332-0083** kilichotolewa na **MOROGORO SEKONDARI mwaka 2001.**

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **URP/RB/6687/2017.**

**CHETI KIMEPOTEA**



**LAURA ABASS SALUM** wa Mombasa Zanzibar anatangaza kupotelewa na Cheti cha Masomo ya Bima Ngazi ya Cheti chenye namba ya usajili **CI/16256/06** kilichotolewa na chuo cha Institute of Finance Management , Dar es Salaam mwaka 2006/2007. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa: **MAZ/LF.13/2016**

*Kwa Habari Motomoto*

*usikose Gazeti lako la The Guardian*

*Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,*

*au piga simu: 0767 223311*

## JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

# Nipashe

NI JIBU LAKO NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, Tupigie 0767 223311

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# GATTUSO
## ASHANGAA KIWANGO AC MILAN

**MILAN, Italia**

KOCHA wa AC Milan, Gennaro Gattuso, amekataa kuwalaumu wachezaji wa kikosi chake kwa kuonyesha kiwango duni wakati wakiibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Sassuolo nyumbani kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A.

Ushindi huo umewavuta hadi nafasi ya tatu Rossoneri hao na kuwa juu dhidi ya wapinzani wao, Inter Milan.

Bao la kujifunga la beki wa Sassuolo, Pol Lirola, lilitosha kuwapa ushindi Milan na hivyo kujiweka kwenye mazingira mazuri ya kufuzu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Gattuso amebainisha kwamba, Milan inatakiwa kuimarika zaidi kiuchezaji kama inataka kuendelea kupata ushindi kwenye ligi hiyo na kubakia katika nafasi za juu, huku kukiwa na mechi 12 zimebaki kabla ya kumalizika kwa ligi hiyo.

Gattuso aliiambia Sky Sport Italia: "Usiku tulicheza vizuri na kuwa na matokeo mazuri, lakini tunatakiwa kucheza kwa ubora zaidi. Sitaki kusikia kuhusu kuchoka, nataka kuelewa kwa nini hatuchezi soka la kuvutia.

"Tulikuwa na wakati mgumu dhidi ya Sassuolo, ambao walifanya vizuri kwenye safu yao ya ulinzi. Tunaweza kucheza vizuri zaidi wakati tukiwa na mpira.

"Sasa tunatakiwa kuwa vizuri. Tunatakiwa kucheza mechi 12 za mwisho za Serie A. Sitaki mtu yeyote aanze kusherehekea kwa kuwa nafasi ya tatu, si mashabiki wala wachezaji. Kile tunachofanya kinatosha, tunahitaji kufanya zaidi."

## EMERY ATAKA VAR LIGI KUU ENGLAND

**LONDON, England**

KOCHA wa Arsenal, Unai Emery, amedai kwamba VAR itawasaidia waamuzi kufanya maamuzi sahihi kwenye mchezo unaofuata baada ya kushuhudia kikosi chake kikitoka sare ya kufungana bao 1-1 na Tottenham juzi Jumamosi.

'Washika Bunduki' hao pengine wangeweza kupata pointi zote tatu kama wangefunga penalti ya dakika za mwisho katika mchezo huo uliopigwa kwenye Uwanja wa Wembley.

Mshambuliaji wa Tottenham, Harry Kane, alionekana kuwa ameotea wakati Spurs walipopewa penalti katika kipindi cha pili.

Baada ya mchezo huo, Emery alikataa kuwalaumu waamuzi kwenye mechi hiyo kwa kusema kwamba inatakiwa kuletwa mfumo wa maamuzi kwa njia ya video ili kuweza kupata maamuzi sahihi.

"Nafikiri VAR inakuja kuwasaidia waamuzi," alisema Emery akiwaambia waandishi wa habari akinukuliwa na Sky Sports.

"VAR inatakiwa kuja kwa mechi kama ya leo (juzi). Kwa upande wangu waamuzi ni binadamu, lakini huwa hawaoni kila kitu uwanjani.

Aliongeza: "Mwezi mmoja uliopita nilisema kuhusu maoni yangu juu ya VAR kwamba ije kuwasaidia waamuzi."

# Kovac aanza kuona ubora Bayern Munich

**MUNICH, Ujerumani**

KOCHA wa Bayern Munich, Niko Kovac, anaamini kwamba kikosi chake kilicheza kwa kiwango bora wakati kikiibuka na ushindi wa mabao 5-1 dhidi ya Borussia Mönchengladbach kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, Jumamosi.

Mabao mawili ya Robert Lewandowski - ambaye amekuwa mfungaji bora wa tatu kwenye Bundesliga na mabao ya Javi Martinez, Thomas Muller na Serge Gnabry, yaliisaidia timu hiyo kupata ushindi huo kwenye Uwanja wa Borussia-Park.

"Tumecheza vizuri kwenye Bundesliga msimu huu," alisema Kovac akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Nina furaha kubwa na mchezo walioucheza na walicheza vizuri zaidi, lakini tungeweza kufunga mabao mengi zaidi."


Ushindi huo mkubwa, ambao ulikuwa ni wa tano kwa Bayern katika mechi sita zilizopita kwenye mashindano yote, hivyo maana yeke ni kwamba wanatofautiana kwa mabao na Dortmund katika mechi 10 zilizobaki msimu huu.

Aliongeza: "Sasa kila kitu kimefunguka tena. Mbio za ubingwa zimeendelea kuwa kwenye kasi tena na ushindani mkubwa kwa upande wetu, lakini tunahamasa kubwa.

"Timu inafanya vizuri kwa uhakika, kuna hali nzuri na tuko imara kwenye kila idara."



## HABARI MICHEZO



# Zidane
## azua vita Chelsea, Juventus

**LONDON, England**

TIMU za Chelsea na Juventus ziko kwenye mbio moja za kuwania saini ya kocha wa zamani wa Real Madrid, Zinedine Zidane.

Kwa mujibu wa Sky Sports, Chelsea imekuwa kwenye harakati za kutaka kumwajiri kocha mpya, baada ya Maurizio Sarri kuonekana kwamba, uwezo wake umefikia tamati kwa kushindwa kuipaisha timu hiyo.

Chelsea imekuwa na matokeo mabaya katika mechi za hivi karibuni na hivyo kumuweka kwenye wakati mgumu kocha, Sarri ambaye inatabiriwa kwamba, siku zake hapo kwenye dimba la Stamford Bridge zinahesabika.

Awali Chelsea walionyesha nia ya kutaka kumsajili Zidane muda mrefu, lakini haikuweka wazi.

Na sasa inakumbana na shinikizo linalotokana na ukweli kuwa Juventus inataka kumchukua Zidane kwa ajili ya msimu ujao wa soka.

Kuna taarifa kuwa kocha wa sasa wa Juventus, Massimiliano Allegri, anatazamiwa kuondoka mwishoni mwa msimu huu.

Allegri inasemekana anataka kuachana na timu hiyo baada ya kuisaidia kutwaa taji la Serie A kwa mara ya tano mfululizo.

Chelsea katika siku za karibuni inasemekana imekuwa inafanya mawasiliano na Zidane kwa ajili ya kumchukua.

Hali hiyo inatokana na mwenendo wa sasa wa kusuasua kwa timu hiyo inayonolewa na Maurizio Sarri.

Juventus, hata hivyo, inasemekana inataka kumchukua Zidane, ambaye aliwahi kuchezea timu hiyo katika miaka ya nyuma.

Maana yake ni kuwa Chelsea inaweza kumkosa kama isipoongeza spidi ya kumnyakua.

Hata presha ya kutimuliwa kwa Sarri imepoa kidogo baada ya kuisaidia Chelsea kuishinda Tottenham Hotspur mabao 2-0 kwenye mechi ya Ligi Kuu England, Jumatano iliyopita.

## SOLSKJAER AZIDI KUWATIA 'NDIMU' WACHEZAJI WAKE



**MANCHESTER, England**

OLE Gunnar Solskjaer amesifia wachezaji wake baada ya Manchester United kuibuka na ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Southampton Jumamosi.

Man United ilitoka nyuma kuweza kupata ushindi huo, kabla ya kushindi dhidi ya Southampton juzi Jumamosi.

Mabao mawili ya Romelu Lukaku yaliiwezesha United kushinda katika mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Old Trafford juzi.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya mchezo huo, Solskjaer amesema kwamba: "Nimefurahia namna wachezaji wangu walivyocheza.

"Inafurahisha unapoona vijana wako wanacheza kwa kiwango cha juu na wanastahili kucheza kwa staili ambayo mimi nilitaka wachezaji wangu wacheze. "Tulizungumza baada ya kipindi cha pili na wazi kuwa ilionyesha wachezaji wangu wapo kwenye kiwango kinachotakiwa.

"Tulionyesha tabia yetu ya asili kwenye mchezo wetu na tulitaka kuendelea kucheza vizuri na sasa tunaungalia mchezo wetu wa Jumatano."

United Jumatano itasafiri kwenda jijini Paris kucheza na miamba wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, PSG kwenye mchezo wa pili wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya mtoano ya 16-bora.

Kwenye mchezo wa kwanza 'Mashetani Wekundu' hao walifungwa 2-0.



## SANTIAGO AISIFU MADRID IKICHARAZWA NA BARCA

**MADRID, Hispania**

SANTIAGO Solari amesisitiza kwamba timu yake ya Real Madrid ilicheza vizuri licha ya kufungwa bao 1-0 na wapinzani wao wakubwa, Barcelona kwenye mechi ya La Liga iliyopigwa Uwanja wa Santiago Bernabeu juzi, Jumamosi.

Ikiwa imetoka kufungwa na Barcelona ndani ya siku tatu kwenye Kombe la Mfalme ['Copa del Rey'], Real ilitarajiwa mchezo huo kama ungekuwa wa kulipa kisasi, lakini wakajikuta wakifungwa kwa bao la Ivan Rakitic.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Solari amesisitiza alihisi kuona timu yake ikicheza kwa kiwango kizuri, lakini akakubali kwamba hawakuweza kutumia vizuri nafasi walizozipata.

Alisema: "Tulijaribu kucheza kwa kiwango cha juu na hatukuweza.

"Ulikuwa mchezo mgumu kwa upande wetu, lakini tulicheza kwa kiwango cha juu ila tukashindwa kufunga. Kama hufungi mabao huwezi kushinda.

"Tulicheza soka vizuri na tulijibu maswali ya watu wengi wanaotushutumu na hatukuweza kupata mabao," alisema.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# AUBAMEYANG, LACAZETTE WATETEWA KUVURUNDA

●●● Alikuwa na dakika 35 za kutusaidia kupata ushindi kwa penalti, unaweza kufunga ama la. Siyo kosa, ni kitendo...

**LONDON, England**

KOCHA Mkuu wa Arsenal, Unai Emery, amesema hana sababu ya kumlaumu Pierre-Emerick Aubameyang ama Alexandre Lacazette kwa kukosa nafasi Jumamosi wakati wakitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Tottenham Jumamosi.

Lacazette tayari alishakosa nafasi muhimu kabla ya kumtengenezea bao Aaron Ramsey aliyeifungia la kwanza kwenye mchezo huo wa Ligi Kuu uliopigwa Uwanja wa Wembley, na kisha Mfaransa huyo kukosa tena bao mwanzoni mwa kipindi cha pili.

Haraka alitolewa na kuingizwa Aubameyang, ambaye baada ya Harry Kane kuisawazishia Spurs kutokana na mkwaju wa penalti, naye alishindwa kuzamisha tuta kimyani kufuatia kipa Hugo Lloris kuokoa.

"Nimezungumza naye [Aubameyang]. Alikuwa na dakika 35 za kutusaidia kupata ushindi," Emery aliuambia mkutano wa wanahabari.

"Alifanya kitendo hiki na kuzawadiwa penalti. Baada ya hapo unaweza kufunga ama la. Siyo kosa, ni kitendo kimoja.

"Kama ilivyo kwa Laca. Alikuwa na nafasi nzuri, lakini hakuna tatizo. Leo tumetengeneza baadhi ya nafasi nzuri lakini leo haitoshi."

Emery pia alimpongeza sana Sokratis Papastathopoulos baada ya kukunwa na uchezaji wa beki huyo wa kimataifa wa Ugiriki.

"Maendeleo yake ni muhimu sana," Emery aliongeza.

"Leo amecheza vizuri, lakini mechi ya mwisho amekuja na kujiamini mwenyewe kutumia ujuzi wake na uwezo wa kutusaidia.

"Pia ana uzoefu wa kuendelea na mchakato wake na sisi. "

## KWA UFUPI

**SANCHO VITANI UNITED, PSG**

Manchester United inakabiliwa na upinzani mgumu kutoka Paris St-Germain katika mbio za kumsajili winga wa Borussia Dortmund na England, Jadon Sancho, 18. ***(Mirror)***

**BALE CHAMBO YA ERIKSEN**

Real Madrid ipo tayari kumtumia mshambuliaji wa Wales, Gareth Bale, 29, kama chambo ya kumsajili kiungo wa Tottenham na Denmark, Christian Eriksen, 27. ***(Mirror)***

**CONTE KUMRITHI ALLEGRI JUVE**

Juventus inaweza kumgeukia kocha wa zamani wa Chelsea, Antonio Conte kama Massimiliano Allegri ataachana na miamba hiyo ya Serie A majira haya ya joto. ***(Corriere Dello Sport - in Italian)***

**LUKAKU KUPISHANA ICARDI**

Manchester United itapewa ofa ya kumnunua straika Muargentina Mauro Icardi, 26, kufuatia Inter Milan kumtolea macho mshambuliaji Mbelgiji Romelu Lukaku, 25, ikitaka wabadilishane. ***(Express)***

**NEWCASTLE YAONDOLEWA SOKONI**

MMILIKI wa Newcastle United, Mike Ashley, hatazamii tena kuiuza klabu hiyo baada ya kutoona ofa ya kuridhisha tangu alipoiweka sokoni miezi 17 iliyopita. ***(Times)***

**RODGERS AMHAKIKISHIA VARDY**

KOCHA mpya wa Leicester, Brendan Rodgers, amemwambia mshambuliaji wa kimataifa wa England, Jamie Vardy, 32, atajijenga timu hiyo kumzunguka. ***(Telegraph)***

**'SILVA KUFUNGWA MIAKA SITA'**

KIUNGO wa Manchester City, Mreno Bernardo Silva, atapewa mkataba mpya wa miaka sita. ***(Mail)***

**CABALLERO KUPEWA MWAKA CHELSEA**

Chelsea itamwongeza mkataba wa mwaka mmoja kipa Muargentina Willy Caballero, 37. ***(Sun)***

**FIFA KIKWAZO ZIDANE CHELSEA**

Fifa huenda ikazuia mpango wa Chelsea kutumia pauni milioni 200 kwenye usajili wa majira ya joto, jambo ambalo linaweza pia kuizuia kumpata Zinedine Zidane kama kocha mpya. ***(Sun)***

**GUARDIOLA KWA FUJO SOKONI**

Manchester City itatumia pauni milioni 350 majira ya joto wakati huu kocha Pep Guardiola akitaka kuongeza majembe manne mapya. ***(Star)***

**ALCANTARA AWINDWA CITY**

pep Guardiola anataka kusajili kutoka klabu yake ya hivi karibuni Bayern Munich - huku kiungo Mhispania Thiago Alcantara, 27, akiwa ndiye anayemtolea macho. ***(Mirror)***

**UNITED KUIBOMOA BENFICA**

Manchester United ipo tayari kutoa ofa kiasi cha euro milioni 180 kwa Benfica ili kumsajili beki Mreno Ruben Dias, 21, na kiungo mshambuliaji Joao Felix, 19. ***(Record - in Portuguese)***

**SHELVEY KUTUA WEST HAM**

West Ham inajiandaa kumsajili kiungo Muingereza Jonjo Shelvey, 27, kutoka Newcastle majira haya ya joto. ***(Sun)***



## HABARI MICHEZO

# ZAHERA ATOBOA SIRI KUIFUMUA ALLIANCE

**Na Faustine Feliciane, Shinyanga**

KOCHA wa Yanga, Mwinyi Zahera, amesema moja ya siri ya kufanikiwa kuibuka na ushindi kwenye michezo miwili ya karibuni wakiwa ugenini ni wachezaji wake kuwaheshimu wapinzani wao na kucheza kwa nidhamu, huku wakijituma muda wote wa mchezo.

Yanga juzi ilifanikiwa kuibuka na ushindi wa bao 1-0 mbele ya Alliance kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza, huo ukiwa ushindi wao wa pili mfululizo wakiwa ugenini. Akizungumza na gazeti hili jana, Zahera, alisema aliwapongeza wachezaji wake kwa namna wanavyojituma uwanjani licha ya upinzani mkubwa wanaoupata.

"Bila kuficha niwapongeze wachezaji wangu kwa namna wanavyopambana uwanjani, mfano wa hili ni mchezo na Alliance... mechi ilikuwa ngumu, wapinzani wetu walicheza vizuri sana, lakini kama ninavyosema wachezaji wangu walipambana na kujituma kuhakikisha tunapata ushindi," alisema Zahera. Alisema baada ya mchezo huo sasa wanaenda kujipanga kwa ajili ya mchezo unaofuata.

"Nawapa mapumziko wachezaji wangu, tukirejea Dar es Salaam tutaendelea na mazoezi Jumanne kujiandaa na mchezo unaofuata, lengo ni kuhakikisha tunapata ushindi katika kila mechi," alisema Zahera.

Alisema kumalizika kwa mchezo huo wa juzi ni mwanzo wa kujipanga kwa ajili ya mchezo dhidi ya KMC ya Kinondoni utakaochezwa Jumapili Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

"Tunajipanga kwa ajili ya mchezo na KMC, Jumanne tutaanza mkakati wetu kuhakikisha tunapata ushindi kama tulivyofanya Mwanza," alisema.

Ushindi wa juzi wa Yanga umewafanya kuendelea kuongoza ligi wakikusanya pointi 64 baada ya kushuka dimbani mara 26.

**POOZA...**




Meneja Uhusiano na Mawasiliano ya Nje wa Kampuni ya Tanga Cement, Mtanga Noor (kulia), akimpa maji ili kupooza kiu mmoja wa wakimbiaji wa mbio za Kilimanjaro Marathon mjini Moshi mkoani Kilimanjaro jana. Kampuni hiyo imetumia zaidi ya Sh. milioni 37 kudhamini mbio hizo ikiwa ni pamoja na kituo cha maji na wakimbiaji wake 35. **MPIGAPICHA WETU**

# Serengeti Boys kibaruani Uturuki

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Taifa ya Vijana wa umri chini ya miaka 17 maarufu Serengeti Boys, inatarajia kuwakabili Yoso wenzao wa Guinea katika mechi ya kwanza ya kuwania ubingwa wa mashindano ya UEFA Assist itakayoanza leo nchini Uturuki.

Katika mashindano hayo, Serengeti Boys imepangwa Kundi namba 1, ikiwa pamoja na wenyeji Uturuki, Guinea na Australia.

**Akizungumza na gazeti hili, Kocha Mkuu wa Serengeti Boys, Oscar Milambo, alisema kikosi chake kiliwasili salama nchini humo juzi na jana walifanya mazoezi kwa ajili ya kuanza kampeni ya kushinda kombe la michuano hiyo wanayoshiriki kwa mara ya kwanza.**

Milambo alisema ameridhishwa na mazingira ya kambi na anaamini wachezaji wake watapata nafasi ya kujiimarisha na hatimaye kutimiza malengo yao kabla ya kurejea nyumbani.

"Nilitamani kupangwa katika kundi lenye timu nyingi za Afrika, lakini hata hapa tulipowekwa si pabaya, wachezaji wangu watajifunza vitu vipya kutoka kwa wenzao wa Ulaya, tuko tayari kufanya kile kilichotuleta," alisema Milambo.

Kocha huyo aliongeza kuwa hali ya hewa ya baridi kali iliyoko Uturuki si tatizo kwa wachezaji wake kutokana na mazingira ya jiji la Arusha walipokuwa wameweka kambi ya wiki mbili kabla ya kutua nchini humo.

Serengeti Boys ambao ni wenyeji wa Fainali za Vijana za Afrika (AFCON -17) zitakazofanyika mwezi ujao, wanatumia michuano hiyo kujiandaa na fainali hizo zitakazofanyika kwa mara ya kwanza kwenye ardhi ya Tanzania.

Katika michuano ya AFCON -17, Serengeti Boys imepangwa Kundi A pamoja na Uganda, Angola na Nigeria.

**MSIMAMO LIGI KUU BARA**

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.YANGA | 26 | 20 | 4 | 2 | 43 | 17 | 64 |
| 2.AZAM | 26 | 15 | 8 | 3 | 36 | 17 | 53 |
| 3.SIMBA | 20 | 16 | 3 | 1 | 43 | 7 | 51 |
| 4.KINONDONI MC | 28 | 9 | 14 | 5 | 31 | 18 | 41 |
| 5.LIPULI | 28 | 9 | 11 | 8 | 24 | 24 | 38 |
| 6.ALLIANCE | 29 | 9 | 9 | 11 | 23 | 30 | 36 |
| 7.MBAO | 28 | 9 | 9 | 10 | 19 | 26 | 36 |
| 8.MTIBWA SUGAR | 26 | 10 | 5 | 11 | 26 | 21 | 35 |
| 9.JKT TANZANIA | 28 | 8 | 11 | 9 | 16 | 17 | 35 |
| 10.COASTAL UNION | 28 | 7 | 13 | 8 | 26 | 30 | 34 |
| 11.RUVU SHOOTING | 29 | 8 | 10 | 11 | 27 | 35 | 34 |
| 12.MBEYA CITY | 26 | 9 | 6 | 11 | 27 | 29 | 33 |
| 13.MWADUI | 29 | 9 | 6 | 14 | 31 | 36 | 33 |
| 14.STAND UTD | 29 | 9 | 6 | 14 | 27 | 37 | 33 |
| 15.TZ PRISONS | 27 | 7 | 11 | 9 | 19 | 22 | 32 |
| 16.NDANDA | 26 | 8 | 8 | 10 | 17 | 27 | 32 |
| 17.KAGERA SUGAR | 26 | 6 | 12 | 8 | 19 | 25 | 30 |
| 18.SINGIDA UNITED | 26 | 7 | 8 | 11 | 18 | 25 | 29 |
| 19.BIASHARA UNITED | 27 | 5 | 9 | 13 | 18 | 29 | 24 |
| 20.AFRICAN LYON | 28 | 4 | 9 | 15 | 17 | 35 | 21 |

# Alliance: Hatuna bahati Kirumba

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya timu yake kupoteza mechi dhidi ya Yanga, Kocha Mkuu wa Alliance FC ya jijini Mwanza, Malale Hamsini, amesema kikosi chake hakina bahati ya kupata ushindi wanapocheza kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Alliance FC juzi ilikubali kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga ambao wameendelea kujiimarisha kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo.

Malale aliliambia gazeti hilo kuwa timu yake ambayo inatumia pia Uwanja wa Nyamagana, imekuwa ikipoteza mechi wanapocheza kwenye uwanja huo hata kama wachezaji wake wataonyesha kandanda la kuvutia ukilinganisha na wapinzani wao.

Kocha huyo alisema pamoja na matokeo hayo, hawajakata tamaa na bado wanaamini wanayo nafasi ya kufanya vizuri katika michezo inayofuata na kujiepusha na janga la kushuka daraja.

**"Tumeshinda mechi zetu tatu mfululizo katika Uwanja wa Ny amagana, naona hatu na bahati na Kirumba, vijana walipambana, lakini siku haikuwa yetu, muda bado upo , tutaendelea kureke bisha makosa kwa ajili ya kufanya vizuri kwe nye mechi zinazokuja," Malale alisema.**

Yanga ndio vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara wakiwa na pointi 64 wakifuatiwa na Azam FC yenye pointi 53, huku mabingwa watetezi Simba wakishika nafasi ya tatu.

1.YANGA
2.AZAM
3.SIMBA
4.KINOND
5.LIPULI
6.ALLIAN
7.MBAO
8.MTIBWA

# Michezo

Jumatatu Machi 4, 2019
Nipashe



**Aubameyang, Lacazette watetewa kuvurunda**

HABARI UK 30

**UMETUTOA...**



Waziri wa Habari Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, akimvisha medali mwanariadhara Emmanuel Giniki, baada ya kushika nafasi ya kwanza katika mashindano ya kilometa 21 maarufu kama Tigo Kili Half Marathon. Pembeni kulia ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa tiGO, Simon Karikari na kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Simiyu na Rais wa RT, Anthony Mtaka. **MPIGAPICHA WETU**

# SIMBA SI YA LIGI HII

## ●●● Yainamisha uwanja Shinyanga na kuibomoa Stand, sasa kuwafuata Walgeria kesho huku...

**Na Faustine Feliciane, SHINYANGA**

SIMBA imezidi kudhihirisha kuwa ni ya daraja la juu na ndiyo maana inaiwakilisha Afrika Mashariki na Kati kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya jana kuwacharaza wababe wa watani zao Yanga, Stand United kwa mabao 2-0.

Ushindi huo ni watano mfululizo kwenye Ligi Kuu Bara tangu ilipotoka kuichapa Al Ahly kwa bao 1-0 kwenye mechi ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Taifa.

Simba ilirejea Ligi Kuu kwa kuichapa Yanga bao 1-0 kisha ikaifuata African Lyon Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha na kuinyuka 3-0 na kurudi Uwanja wa Taifa kuicharaza Azam FC 3-1 kabla ya kuibuka na ushindi kama huo dhidi ya Lipuli FC kwenye Uwanja wa Samora, Iringa.

Katika mechi ya jana, mabao mawili ya kipindi cha pili ya nahodha John Bocco ndiyo yaliyoiwezesha Simba kuendeleza makali yake kwa kuibuka na ushindi huo wa 2-0 dhidi ya Stand United kwenye Uwanja wa Kambarage mjini hapa.

Stand walionekana kuwabana Simba kipindi cha kwanza kwa kuhimili kasi ya viungo wa Simba, ambapo jana Kocha Patrick Aussems, alimpumzisha kiungo Clatous Chama na nafasi yake kuchukuliwa na Haruna Niyonzima aliyecheza kwa dakika zote 90 huku pia akimwanzisha Adam Salamba na Meddie Kagere kuanzia benchi.

Mpaka kipindi cha kwanza kinamalizika timu hizo hazikufungana.

Kipindi cha pili kilianza kwa kasi, huku Simba wakifanya mashambulizi makali dakika 15 za kwanza na kufanikiwa kupata bao dakika ya 50 kwa mkwaju wa penalti uliotolewa na mwamuzi Emmanuel Mwandembwa baada ya Vicent Maganga kuunawa mpira eneo la hatari.

Kuingia kwa bao hilo kuliifanya Simba kuendelea kulishambulia lango la Stand na dakika moja baadaye walikosa bao kupitia kwa Kagere.

Simba walifanya mabadiliko dakika ya 58 kwa kumtoa Rashid Juma na nafasi yake kuchukuliwa na Jonas Mkude aliyeongeza uhai safu ya kiungo.

Dakika ya 64 Bocco alifunga bao la pili kwa kichwa cha kuparaza akiunganisha shuti la Nicolaus Gyan na kuamsha shangwe kwa mashabiki waliojazana uwanjani hapo.

Ushindi huo unaifanya Simba iliyoshuka dimbani mara 20 kuendeleza kasi yake kwa kufikisha pointi 51 mbili nyuma ya Azam iliyopo nafasi ya pili baada ya mechi 26, huku Yanga ikiwa kileleni na alama 64 kwa michezo sawa na 'Wanalambalamba' hao.

Ushindi huo pia ni kama umemuumbua kocha wa Stand, Hassan Bilal ambaye kabla ya mchezo alisema Simba ni timu ya kawaida na ataifunga.

Simba ambayo ni timu pekee iliyobaki kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kutoka Ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati, sasa inajiandaa kuelekea Algeria kesho kwa ajili ya mechi ya marudiano ya hatua ya makundi dhidi ya JS Saoura itakayopigwa Jumamosi.

# Giniki afunika Tigo Kili Half Marathon

**Na Mwandishi Wetu, MOSHI**

MTANZANIA Emmanuel Giniki ameibuka mshindi wa mbio za kilomita 21 maarufu kama Tigo Kili Half Marathon zilizofanyika mjini Moshi jana.

Giniki amevunja mwiko katika mbio hizo ambazo kwa miaka mingi zimekuwa zikitawaliwa na raia wa kigeni, Wakenya ambao kwa kipindi kirefu wamekuwa wakiibuka washindi.

Giniki alimaliza mbio hizo akitumia muda wa saa 1:03:34, huku akifuatiwa na Bernad Musau wa Kenya aliyetumia saa 1:03:42 na Joseph Njiha (Kenya) aliyemaliza akitumia saa 1:05:13. Kwa upande wa wanawake, aliyeshika nafasi ya kwanza ni mwanariadha wa Kenya, Grace Kimanzi ambaye alitumia saa 1:11:45, akifuatiwa na Failuna Matanga (Tanzania) ambaye alitumia saa 1:14:01 na Esther Kakuri (Kenya) aliyemaliza kwa saa 1:14:42

Akizungumza muda mfupi baada ya kukabidhiwa zawadi ya fedha taslimu Sh. milioni mbili, Giniki alisema anayo furaha kushinda mbio hizo na kuiletea heshima nchi yake jambo ambalo amekuwa akilitamani.

"Pamoja na kwamba mbio hizi zimekuwa zikifanyika hapa nyumbani, tumekuwa tukishindwa kuzitendea haki kwa kuwa wageni ndiyo wamekuwa wakizitawala. Ninayofuraha leo nimeweza kulitoa taifa langu kimasomaso," alisema.

Akizungumza wakati wa halfa ya kukabidhi zawadi, Mkurugenzi Mtendaji wa Tigo, Simon Karikari, alisema kampuni yake inayo furaha kuchangia maendeleo ya michezo nchini na hususan riadha ambayo pia huboresha afya.

Karikari alisema Tigo imekuwa mdhamini wa mbio za nusu marathon kwa kipindi cha miaka minne mfululizo na kuongeza kuwa kampuni yake itaendelea kudhamini pamoja na kuboresha mbio hizo kila mwaka.

Waziri wa Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, aliishukuru Tigo kwa kudhamini mbio hizo na kuwataka wakazi wa Moshi kutumia fursa zitokanazo na mbio hizo kujitengenezea fursa. "Mbio hizi zimeleta wakimbiaji kutoka nchi zaidi ya 50 hapa mjini Moshi. Idadi hii kubwa ya watu itokanayo na mbio hizi ni fursa nzuri ya kibiashara na ni vyema wakazi wa Moshi wakaichangamkia," alisema Waziri Mwakyembe.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >